

**ATHARI YA TAMTHILIA YA *MASHETANI* (1971) JUU YA
TAMTHILIA YA *MASHETANI WAMERUDI* (2016)**

NYANCHAMA FILISTER EUNICE

C50/CE/25426/2014

**TASNIFU YA UTAFITI IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA
KENYATTA IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA**

MEI, 2025

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote.

Sahihi..... *FA* Tarehe..... *23/5/2025*

Nyanchama Filister Eunice

C50/CE/25426/2014

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yangu kama msimamizi aliyeteuliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sahihi..... *Dugi* Tarehe..... *23/5/2025*

DKT. Jesse Murithi

Idara ya Kiswahili Lugha za Kiafrika,

Chuo Kikuu Cha Kenyatta



SHUKRANI

Hakika safari hii imekuwa ndefu tangu nilipoanza kazi hii. Kwanza, natoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia neema ya afya mpaka nilipoikamilisha kazi hii.

Pili, natoa shukrani zangu za dhati kwa Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa kunikuza na kunipa fursa ya kutangamana na wasomi chuoni. Vilevile, nashukuru Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika kwa kunielekeza vyema.

Nawashukuru sana Dkt. Jesse Murithi na Dkt. Richard M. Wafula walionishika mkono na kunielekeza katika ulimwengu huu wa kitaaluma. Wasomi hawa wameshirikiana nami tangu mwanzo hadi mwisho wa kazi hii. Mola awabariki.

Natoa shukrani zangu kwa ndugu zangu Lynet, Robert, Lilian, Morine, Bonne na Jared kwa ushauri wao hasa nilipokuwa nikitafiti kazi hii. Namshukuru mume wangu kwa kunivumilia nilipokuwa nikishughulikia kazi hii.

Nawashukuru walimu wenzangu wa Shule ya Upili ya Gathiga kwa kunitia moyo katika safari hii ya usomi. Nawashukuru rafiki zangu Thananga, Beth, Martha Mutua, Shiphira, Wangeci, Perpetua, Judy, Bundi, Mose na Justin kwa kunihimiza na kunipa msaada nilipohitaji kutoka kwenu.

Nawashukuru Paul Were Opiyo, Bob Rioba na Francis Macharia kwa msaada wenu katika kila hatua ya utafiti huu.

Kwa wote mlionisaidia kwa njia moja au nyingine, Mungu awajalie neema maishani mwenu. Amina.

TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia wazazi wangu Ruphina Nyakundi na Zachariah Nyakundi. Wamejitolea kihali na mali kuhakikisha kuwa nimekamilisha elimu yangu. Mola awape maisha marefu.

YALIYOMO

UNGAMO	ii
SHUKRANI	iii
TABARUKU	iv
YALIYOMO	v
MAELEZO YA ISTILAHU	ix
ORODHA YA VIFUPISHO	x
IKISIRI	xi
ABSTRACT	xii
SURA YA KWANZA	1
UTANGULIZI	1
1.0 Usuli wa Mada	1
1.1 Suala la Utafiti	3
1.2 Malengo ya Utafiti	3
1.3 Maswali ya Utafiti	4
1.4 Sababu za Kuchagua Mada	4
1.5 Upeo na Mipaka	5
1.6 Yalioandikwa Kuhusu Mada	5
1.7 Misingi ya Nadharia	10
1.8 Mbinu za Utafiti	14
1.8.1 Mahali pa Utafiti	14
1.8.2 Muundo wa Utafiti	14
1.8.3 Uteuzi wa Sampuli	15
1.8.4 Ukusanyaji wa Data	15
1.8.5 Uchanganuzi wa Data	15
1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo	16

SURA YA PILI.....	17
ATHARI ZA MAUDHUI YA <i>MASHETANI</i> (1971) KWA MAUDHUI YA <i>MASHETANI WAMERUDI</i> (2016)	17
2.0 Utangulizi.....	17
2.1 Watunzi na Mazingira Yao	19
2.1.1 Ebrahim Hussein: Mwanatamthilia.....	19
2.1.2 Said A. Mohamed: Mwanatamthilia	24
2.2 Muhtasari wa Tamthilia	28
2.2.1 Tamthilia ya <i>Mashetani</i> (1971).....	28
2.2.2 Tamthilia ya <i>Mashetani Wamerudi</i> (2016).....	29
2.3 Athari za <i>Mashetani</i> (1971) Kwa <i>Mashetani Wamerudi</i> (2016) Kimaudhui	31
2.3.1 Elimu ya Kigeni	31
2.3.2 Ukoloni Mkongwe	32
2.3.3 Ukoloni Mamboleo	34
2.3.4 Utabaka	36
2.3.5 Unyanyasaji na Uonevu	37
2.3.6 Kujitoa Mhanga	39
2.3.7 Migogoro katika Jamii	40
2.3.8 Ulevi na Uasherati.....	41
2.4 Nafasi ya Mwanamke katika Jamii	42
2.5 Unafiki	44
2.6 Hitimisho.....	45
SURA YA TATU.....	46
MFANANO NA TOFAUTI YA USAWIRI WA WAHUSIKA KATIKA TAMTHILIA YA <i>MASHETANI</i> (1971) NA <i>MASHETANI WAMERUDI</i> (2016)	46
3.0 Utangulizi wa Utafiti.....	46
3.1 Dhana ya Usawiri.....	47

3.2 Dhana ya Wahusika	48
3.3 Usawiri wa Wahusika Katika Tamthilia ya Mashetani (1971) Unaofanana na Tamthilia ya Mashetani Wamerudi (2016)	53
3. 3.1 Mfanano Baina ya Usawiri wa Wahusika Shetani na Sheta katika Tamthilia Teule	54
3.3.2 Mfanano baina ya Wahusika Binadamu, Kijana 1 na Prof katika Tamthilia Teule	57
3.3.3 Kufanana baina ya Juma na Sheta; Profesa na Sheta.....	61
3.3.4 Watu (Mtu 1, Mtu 2) na Askari kanzu 1 na Askari Kanzu 2	63
3.3.5 Binadamu na Vijana (Kijana 1, 2, 3, 4, 5)	65
3.4 Usawiri wa Wahusika Katika Tamthilia ya <i>Mashetani</i> (1971) Unavyotofautiana na Tamthilia ya <i>Mashetani Wamerudi (2016)</i>	70
3.4.1 Juma, Kitaru na Mzee Jumai na Kitarui.....	70
3.4.2 Mama Kitaru na Msichana.....	72
3.5 Hitimisho.....	74
SURA YA NNE	76
ATHARI ZA TAMTHILIA YA MASHETANI (1971) KWA MASHETANI WAMERUDI (2016) KIMTINDO	76
4.0 Utangulizi wa Utafiti.....	76
4.1 Dhana ya Mtindo.....	78
4.2 Vipengele Vya Mtindo Katika Mashetani (1971)	82
4.2.1 Matumizi ya Jazanda katika <i>Mashetani</i> (1971)	82
4.2.2 Taswira.....	88
4.2.4 Lakabu.....	96
4.2.5 Tashihisi	97
4.2.6 Kuchanganya Ndimi	99
4.2.7 Maswali ya Balagha.....	101
4.2.8 Inkisari	103

4.2.9 Misemo/Nahau	103
4.3 Utofauti wa Mtindo Katika Tamthilia Teule	104
4.3.1 Matumizi ya Lahaja katika Mashetani Wamerudi	105
4.3.2 Matumizi ya Karaha.....	106
4.4 Hitimisho.....	107
SURA YA TANO	108
HITIMISHO.....	108
5.1 Utangulizi.....	108
5.2 Muhtasari wa Utafiti	108
5.3 Matokeo	109
5.4 Umuhimu wa Utafiti	113
5.5 Mapendekezo	113
5.6 Changamoto	113
5.7 Hitimisho.....	114
MAREJELEO	115
VIAMBATISHO	122
KIAMBATISHO A: KIBALI CHA UTAFITI.....	122

MAELEZO YA ISTILAHU

- Drama:** Ni utanzu wa fasihi ambao kimsingi hudhamiriwa kuigizwa mbele ya hadhira.
- Mwingilianomatini:** Ni nadharia ya kifasihi inayoelezea kuwepo kwa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi fulani ya kifasihi.
- Tamthilia:** Hii ni kazi ya kidrama na ya kimaongezi ambayo huigizwa mbele ya hadhira au kazi iliyoandikwa kwa lengo kusomwa.
- Matini:** Ni kifungu cha maandishi au usemi wa lugha.
- Athari:** Ni mabadiliko yanayoletwa na mtu au kitu kwa mtu au kitu kingine.
- Usemazano:** Hii ni nadharia inayotumiwa kuelezea uhusiano kati ya matamko mbalimbali.

ORODHA YA VIFUPISHO

Uk: Ukurasa

FS: Fasihi Simulizi

FA: Fasihi Andishi

Mhr: Mhariri

IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza athari ya tamthilia ya *Mashetani* (1971) juu ya tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Kristeva (1966) anafafanua kuwa hakuna matini yoyote ya kifasihi inaweza kuangaliwa kivyake au kujitegemea. Hivyo basi, ilikuwepo haja kuangazia athari ya dhamira, maudhui, wahusika na mtindo katika tamthilia hizi teule. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Mwingilianomatini ilioasisiwa na Kristeva (1966). Mwingilianomatini ni kutegemeana na kuathiriana kwa tanzu au matini (Kuloba, 2015). Hivyo basi, mwingilianomatini ni wakati ambapo sifa za matini moja huweza kujitokeza katika matini nyingine. Mtafiti aliongozwa na malengo yafuatayo: Kwanza, kubainisha athari ya kimaudhui katika tamthilia ya *Mashetani* na tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Pili, kuchunguza athari ya usawiri wa kiwahusika katika tamthilia ya *Mashetani na Mashetani Wamerudi*. Tatu, kuchanganua athari ya kimtindo katika tamthilia ya *Mashetani* na tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Mbinu ya utafiti iliyotumika ni ya kimaelezo ambapo mtafiti alibainisha matukio au data mbalimbali katika tamthilia ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Data iliyokusanywa iliwasilishwa kwa maelezo na kwa kutoa mifano ya maudhui, usawiri wa wahusika na mtindo kwenye tamthilia zilizoteuliwa. Mtafiti aliteua sampuli kimakusudi ili kufanikisha malengo ya utafiti. Utafiti ulikuwa wa maktabani ambapo mtafiti alisoma tamthilia husika, tasnifu, majarida na vitabu ambavyo vinahusiana na mada.

ABSTRACT

This research aimed at examining the influence of *Mashetani* (1971) play on *Mashetani Wamerudi* (2016). According to Kristeva (1966), there is no piece of literature that can be examined independently. Therefore, there is a need to critique the interdependency of the plays in terms of theme, characterization, and style. The research was guided by intertextuality theory whose leading proponent is Kristeva (1966). Intertextuality implies that one text is anchored in another (Kuloba, 2015). This means that similar characteristics can be depicted in two or more literary texts. This research was guided by the objectives of the research which include: Analyzing the thematic impact of *Mashetani* play to *Mashetani Wamerudi* play, analysing the similarities and differences of characters in *Mashetani* play and *Mashetani Wamerudi* play and analysing how stylistic devices are related in *Mashetani* play and *Mashetani Wamerudi* play. The research questions were deduced from the research objectives. A qualitative method of research was used when writing the criticism of the selected Swahili plays. The research was carried out in the library through the reading of specified books in detail, theses, peer-reviewed journal articles, and other related documents. It is hoped that the findings of this research will be of benefit to upcoming authors of plays; especially those who have a special interest in the history of plays, the development of plays, and the writing of plays.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 Usuli wa Mada

Tamthilia ni kazi ya kidrama na ya kimaongezi ambayo huigizwa mbele ya hadhira. Vilevile, ni kazi ya kidrama iliyoandikwa ili kusomwa. Mlama (1983) anasema kuwa tamthilia ni utungo wa drama ambayo ni aina moja ya maandishi ya maonyesho. Wafula (1999) anaeleza kuwa drama ni somo linalohusu uigizaji wa hali fulani iwe ni vitendo au tabia au hisia za binadamu.

Kwa mujibu wa Wafula (1999) Graham Hyslop alifika Afrika Mashariki mwaka wa 1936 na kuanza kazi ya uigizaji mwaka wa 1944. Mwaka wa 1957 Hyslop alitunga michezo miwili mifupi ambayo ni *Afadhali Mchawi* na *Mgeni Karibu*. Aidha mwaka wa 1974 Hyslop alitunga michezo mingine miwili ambayo ni *Mchimba Kisima* na *Kukopa Harusi*. Mwaka wa 1953 tamthilia ya Kuria *Nakupenda Lakini* iliigizwa na wanafunzi wa Shule ya Upili ya Alliance na kisha baadaye ikachapishwa mwaka wa 1957. Kuanzia mwaka wa 1965 baadhi ya tamthilia zilitungwa moja kwa moja katika lugha za Kiswahili ilhali zingine zikatafsiriwa kutoka lugha zingine za kigeni. Kutokana na mafanikio haya; Bertoncini (1989) anadai kuwa mchezo wa kuigiza wa Kiswahili ulioandikwa ulikuja na wakoloni.

Kulingana na Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja (2011) athari ni mabadiliko yanayoletwa na mtu au kitu kingine. Hali ya kisiasa ulimwenguni ilichangia na kuendeleza athari ya fasihi. Bara la Kiafrika lilitawaliwa na wakoloni wakiwemo Waingereza na Wajerumani. Katika enzi ya ukoloni waandishi wengi wa Kiafrika waliathiriwa na kazi zilizotungwa na baadhi ya wageni kama vile Graham Hyslop aliyefika Afrika mashariki mwaka wa 1936.

Mnamo 1971 tamthilia ya *Mashetani* ilichapishwa. Aidha, katika miaka hii ya sabini kulishuhudiwa tafsiri na uandishi wa tamthilia nyingi za Kiswahili kama vile: *Mfalme Edipode* (1971), *Mfalme Juha* (1971), *Hatia* (1972), *Aliyeonja Pepo* (1973), *Masaibu ya Ndugu Jero* (1974), na *Ngao ya Jadi* (1976). Tangu miaka hii ya sabini hadi sasa tamthilia nyingi za Kiswahili zimetungwa. Tamthilia hizi ni: *Arusi* (1980), *Kilio cha Haki* (1981), *Wingu la Kupita* (1999), *Kifo Kisimani* (2002), *Pango* (2003), *Chamchela* (2007), *Kijiba cha Moyo* (2009), *Mstahiki Meya* (2009), *Kigogo* (2016), *Utangamano Wetu Ushindi Wetu* (2017) na nyinginezo.

Bosire (2016) aeleza kuwa kuna athari ya tamthilia za kitambo kwa tamthilia za hivi karibuni. Anaeleza jinsi tamthilia ya *Mstahiki Meya* (2009) ilivyoathiriwa na tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (1979). Alithibitisha kuwa tamthilia hizi zinaingiliana katika msuko, usawiri wa wahusika, mandhari na maudhui. Tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* ilichapishwa kwa mara ya kwanza 1834 (Okwena, 2019). Vilevile, tamthilia hii ilifanyiwa maigizo ya kwanza mnamo mwaka wa 1836 (Wolff na Bayley, 1986). Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa tamthilia za hapo awali na za hivi punde huingiliana na kuchangizana kwa njia moja au nyingine.

Utafiti huu utachanganua athari ya tamthilia ya *Mashetani* (1971) juu ya tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) ili kubaini jinsi tamthilia ya *Mashetani* imeathiri tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Tulingazia athari ya dhamira na maudhui, wahusika na mtindo. Hii ni kutokana na madai ya Kristeva (1966) ambaye anaeleza kuwa hamna matini yoyote ya kifasihi inaweza kuangaliwa kivyake au kujitegemea. Aidha, anasema kuwa lazima kuwe na matini nyingine inayohusiana nayo kwa mfano katika mtindo, maudhui na wahusika. Mohamed (2016) anasema kuwa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) imelazimika kushikamana na tamthilia halisi ya *Mashetani* (1971) ili iweze kwenda katika usasa na upya kwa kushonana katika

wakati uliopita na wakati wa sasa. Aidha anasema kuwa ameamua kufwatiliza tamthilia ya *Mashetani (1971)* kwa kuandika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi (2016)*. Vilevile anafafanua kuwa kazi ya fasihi hukumbushana, huingiliana, husaidiana na kwa namna nyingine huweka upya kwa kilekile kitu cha zamani.

1.1 Suala la Utafiti

Kazi za fasihi huathiriana, hukumbushana na huingiliana kwa namna moja au nyingine. Hii ni kauli ambayo imesemwa na wahakiki wa kisasaleo kama Kristeva (1966), Bakhtin (1981), na Mohamed (2016). Kuna aina mbalimbali za mtagusano kati ya kazi ya kifasihi; usimilishaji, mwingiliano wa wahusika, vikale au kimtindo. Mohamed (2016) anasema kuwa kazi za fasihi ya sasa ni kazi madhubuti zinazotokana na kazi asili lakini kwa sehemu kubwa ni kazi zinazoandikwa kwa upya wa aina yake. Anasisitiza kuwa mwandishi mkongwe anaweza kumwathiri mwandishi wa sasa. Utafiti huu utaainisha na kuchanganua jinsi tamthilia ya *Mashetani (1971)* inavyoathiri tamthilia ya *Mashetani Wamerudi (2016)* kimaudhui, kiwahasika na kimtindo. Tulilenga kubaini ikiwa kuna upya unaojitokeza kutokana na athari ambazo huenda zinajitokeza. Isitoshe, kwa kadri ya ujuzi wa mtafiti, hakuna utafiti wa kina uliofanywa kuhusu suala hili.

1.2 Malengo ya Utafiti

1. Kubainisha jinsi tamthilia ya *Mashetani* ilivyoathiri tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* kimaudhui.
2. Kuonyesha mwingiliano wa kiwahasika katika tamthilia ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*.
3. Kubainisha jinsi tamthilia ya *Mashetani* ilivyoathiri tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* kimtindo.

1.3 Maswali ya Utafiti

1. Tamthilia ya *Mashetani* iliathiri vipi tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* kimaudhui?
2. Usawiri wa wahusika katika tamthilia ya *Mashetani* unafanana au kutofautiana na tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*?
3. Tamthilia ya *Mashetani* iliathiri vipi tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* kimtindo?

1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Tamthilia ina umuhimu mbalimbali; kuelimisha, kukuza maadili, kuburudisha, kuonya, kukuza ubunifu, kuhifadhi historia na kuhifadhi utamaduni. Tamthilia ya *Mashetani* (1971) inahusu enzi ya ukoloni na ukoloni mamboleo. Katika enzi hii waandishi wengi walitunga tamthilia ambazo zilihusu changamoto walizopitia Waafrika walipotawalwa na wakoloni. Tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) iliandikwa baada ya kipindi cha enzi ya ukoloni, ukoloni mamboleo na utandaradhi. Katika kipindi hiki waandishi wengi wa Kiafrika wametunga tamthilia zinazohusu changamoto wanazozipitia Waafrika licha ya kupata uhuru. Hivyo basi, tamthilia ya *Mashetani* (1971) inastahili kuchunguzwa namna ambavyo imeathiri tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Uchunguzi huu ulilenga vipengele vya maudhui, usawiri wa wahusika na mtindo. Vilevile, utafiti wenye mwelekeo huu kadri tujuavyo hujawahi kufanyiwa tamthilia hizi tulizotajwa.

Mohamed (2016) anakiri kuwa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) ni uendelezo wa tamthilia ya *Mashetani* (1971). Mtafiti aliamua kuthibitisha madai haya kwa kubainisha jinsi tamthilia ya *Mashetani* (1971) ilivyoathiri tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016), kimaudhui, kiwahasika na kimtindo. Mtafiti aliamua kuhakiki matini za waandishi hawa wawili: Hussein (1971) na Mohamed (2016) kwa kuwa ni waandishi stadi wa fasihi ya Kiswahili hasa tamthilia za Kiswahili. Okwena (2019) anaeleza kuwa Hussein ni mtunzi mtajika na maarufu katika kanda ya Afrika

Mashariki kwa sababu amechangia mno katika ukuzaji wa fasihi hasa tamthilia ya Kiswahili.

1.5 Upeo na Mipaka

Kazi za waandishi waliotunga kazi zao katika vipindi tofauti zinaweza kuathiriana kwa njia moja au nyingine katika kipengele kimoja au zaidi. Kutokana na hili, tunachanganua athari ya tamthilia ya *Mashetani* (1971) juu ya tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016).

Isitoshe, tanzu za fasihi andishi ni: Riwaya, Hadithi Fupi, Ushairi na Tamthilia. Mtafiti alijikita na utanzu wa tamthilia kwa kuchunguza athari ya tamthilia ya *Mashetani* (1971) juu ya *Mashetani Wamerudi* (2016) kimaudhui, kiwahasika na kimtindo. Vipengele hivi vya uhakiki vilizingatiwa kwa sababu ujenzi na uimarishaji wa fasihi hutegemea dhamira, maudhui, wahusika na mtindo.

1.6 Yalioandikwa Kuhusu Mada

Kulingana na Mlama (1983), tamthilia za awali katika nchi ya Tanzania zilitungwa kwa ajili ya kutumiwa na serikali ya kikoloni kuwasisimua wahudumu wa serikali na kumsimanga Mwafrika, kwani tamthilia mbalimbali zilimsawiri mwafrika kama kiumbe duni. Wafula (1999) alihakiki tamthilia kumi na nne za Kiswahili. Alionyesha maudhui muhimu yaliyoshughulikiwa na waandishi wa tamthilia pamoja na zilivyo na ukwasi mkubwa kimtindo. Kutokana na mawazo haya, mtafiti alifaidika kubainisha maudhui yanayoshughulikiwa katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016).

Vilevile, Mukobwa (1985) alihakiki “maendeleo ya kimaudhui katika tamthilia tano za Ebrahim Hussein” ambaye ndiye mwandishi wa *Mashetani* (1971). Matokeo ya utafiti yalithibitisha uhusiano wa kimaudhui katika tamthilia. Mtafiti aliamua kuhakiki

mwingilianomatini wa kimaudhui, kiwahusika na kimtindo katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na *Mshetani Wamerudi* (2016) ambao ni mwelekeo tofauti na wa Mukobwa (1985) aliyejikita na tamthilia tano kisha akizingatia kipengele cha uhakiki cha maudhui pekee.

Murithi (2002) alihakiki “usemezano katika tamthilia ya Kiswahili.” Tamthilia alizohakiki ni; *Mashetani* (1971), *Kilio cha Haki* (1981) na *Amezidi* (1995). Nadharia ya Usemezano iliyoasisiwa na Bakhtin (1978) ilitumika kama msingi wa utafiti wake. Matokeo ya utafiti wake yalithibitisha uwepo wa usemezano katika tamthilia kinyume na madai ya Bakhtin kuwa usemezano hupatikana katika riwaya pekee. Utafiti huu ulitufaa kwa sababu mojawapo ya tamthilia iliyohakikiwa na mtafiti ni tamthilia ya *Mashetani* (1971). Kuongezea, utafiti wake ulituwezesha kuelewa nadharia ya Mwingilianomatini iliyoasisiwa na Kristeva (1966) kwa sababu ina misingi katika nadharia ya Usemezano ya Mikhail Mikhailovich Bakhtin (1895-1975).

Nzuki (2003) alishughulikia “mwingilianomatini wa fani na maudhui katika ushairi wa Mberia.” Alitathmini mwingilianomatini katika diwani ya *Mchezo wa Karata* (1997) na *Bara Jingine* (2001). Isitoshe, mtafiti aliongozwa na nadharia mseto; Nadharia ya Umuundo iliyoasisiwa na Ferdinand de Saussure (1857-1913) na Nadharia ya Kisosholojia iliyoasisiwa na Hippolyte Adolphe Taine (1828-1893). Alionyesha umuhimu wa vipengele vya kifani pamoja na athari za kimazingira katika kujenga fahiwa. Kazi hii ilitufaa katika kuchunguza mwingiliano wa kifani na kimaudhui katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016).

Aidha, Njoroge (2007) alichunguza “mwingilianomatini katika fasihi ya Kiswahili.” Riwaya alizohakiki ni *Rosa Mistika* (1971) na *Tata za Asumini* (1990). Mtafiti alidhibitisha kuwepo kwa mwingilianomatini katika riwaya za Kiswahili. Kwanza,

kazi hii ilitufaa katika uhakiki wa vipengele vya kifani katika tamthilia za *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016) kwa sababu mtafiti alishughulikia vipengele hivi katika utafiti wake. Pili, utafiti wake ulitusaidia na baadhi ya maoni kuhusu Nadharia ya Mwingilianomatini ambayo mtafiti alishughulikia pia.

Kuloba (2015) alichunguza “mwingilianomatini katika *Cheche za Moto*” (2008) na *Kidagaa Kimemwozea* (2012). Sawia na utafiti wetu, utafiti wake uliongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini ya Kristeva (1966). Tofauti na utafiti wetu unaokusudia kuchunguza fasihi iliyoandikwa na Watanzania na inayopishana sana kiwakati na *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016); Kuloba aliangalia kuathiriana kwa fasihi ya hivi punde na ya Wakenya. Hivyo basi, utafiti huu ulitufaa katika uhakiki wa athari za tamthilia ya *Mashetani* (1971) juu ya tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016).

Utafiti wa Kau (2015) ulitathmini “usimilisho wa riwaya na hadithi fupi kwa wanafunzi wa sekondari nchini Kenya.” Mtafiti alieleza kuwa fani ya usimilisho ni mwendelezo wa mwingilianomatini. Usimilisho ni hali ya kuipa matini inayopatikata katika utanzu fulani wa fasihi sifa za matini nyingine iliyoko katika utanzu tofauti wa fasihi (Kau, 2015). Aidha, matokeo ya utafiti yalibaini kuwa kuna sifa za kinathari kama vile: usimulizi, muundo wa sehemu, mbinu za kimtindo, usawiri wa wahusika na maelezo ya mandhari zinazodhihirika katika tamthilia. Utafiti wake ulitusaidia katika uchanganuzi wa namna tamthilia ya *Mashetani* (1971) inavyoathiri tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) kimtindo na kiwahusika. Vilevile, utafiti huo ulitufaa katika kuelewa zaidi dhana ya mwingilianomatini.

“Mwingilianomatini katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (1979) na *Mstahiki Meya* (2009)’’ulichunguzwa na Bosire (2016). Nadharia ya Mwingilianomatini ilitumika

kuonyesha jinsi vipengele vya ploti, wahusika, mandhari na maudhui vinavyofanana katika tamthilia hizo mbili. Kuongezea, utafiti ulithibitisha kuwa tamthilia hizi mbili zinaingiliana na kuchangiana katika fani na maudhui. Hivyo basi, utafiti huu ulitufaa zaidi kwa kuwa mwandishi alitumia Nadharia ya Mwingilianomatini kuhakiki tamthilia ya *Mashetani* (1971) na tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016).

Isitoshe, Okemwa (2017) alichunguza “mchango wa fasihi simulizi katika fasihi andishi” akijikita na visasili katika *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Aliongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini na akaonyesha mchango wa fasihi simulizi katika kuikuza fasihi andishi. Mtafiti alibainisha umuhimu wa visasili katika utunzi wa riwaya ya Kiswahili. Vilevile, utafiti wake ulirejelea riwaya za Kiswahili kisha za mwandishi mmoja ambaye ni Katama Mkangi. Tofauti na yeye, Utafiti wetu ulihakiki tamthilia ya Kiswahili kisha ya waandishi wawili tofauti ambao ni Ebrahim Hussein na Said Mohamed. Hata hivyo, utafiti wa Okemwa (2017) ulitufaa kuhakiki jinsi tamthilia ya *Mashetani* (1971) imeathiri tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) pamoja na uelewa zaidi wa Nadharia ya Mwingilianomatini.

Massoud (2019) alitathmini “matumizi ya mtindo na dhamira katika tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*: Utafiti linganishi.” Nadharia ya Mwingilianomatini na Nadharia ya Fasihi Linganishi iliyoasisiwa na Zepetnek (1998) zilitumiwa kufanikisha utafiti wake. Mtafiti alichunguza vipengele vya mtindo na dhamira na kuangalia namna tamthilia hizi zinafanana na kutofautiana. Kuongezea, alijikita na uhakiki wa tamathali mbalimbali za semi kama vile nidaa, mdokezo, takriri, majazi na kadhalika. Tofauti na utafiti wake, utafiti huu ulinuia kuhakiki kipengele cha wahusika na uhusika. Pili, mtafiti atatumia Nadharia ya Mwingilianomatini pekee tofauti na Massoud aliyetumia nadharia mseto tulizotaja

awali. Aidha, utafiti wake ulitufaa katika uhakiki wa maudhui katika tamthilia husika kwa sababu mtafiti alitathmini kipengele cha dhamira katika kazi rejelewa.

Okwena (2019) alichunguza “umahuluti wa miundo katika tamthilia za Ebrahim Hussein.” Umahuluti ni mchanganyiko wa mawazo na miundo tofauti katika kazi ya mwandishi. Mtafiti alihakiki tamthilia tano ambazo ni: *Kinjeketile* (1969), *Mashetani* (1971), *Jogoo Kijijini* (1976), *Ngao ya Jadi* (1976) na *Arusi* (1980). Mtafiti alitumia nadharia tatu kufanikisha utafiti wake. Nadharia hizi ni: Nadharia ya Ki-Hegel iliyoa sisiwa na Georg Friedrich Hegel (1822), Nadharia ya Fomula ya Kisimulizi iliyoasisiwa na Vladimir Propp (1939) na Nadharia ya Ki-Brechet ya Bertolt Brechet (1924). Tofauti na Okwena (2019), utafiti wake ulihakiki tamthilia tano za Ebrahim Hussein na ulitumia nadharia tofauti na tunayokusudia kutumia. Mtafiti alitusaidia kuelewa baadhi ya maudhui na wahusika katika tahakiki yake ya *Mashetani* (1971). Hata hivyo, utafiti wake una mwelekeo tofauti kabisa na utafiti huu ambao ulichunguza athari ya tamthilia ya *Mashetani* (1971) juu ya *Mashetani Wamerudi* (2016).

Masatu na Wengineo (2020) walichunguza “mwingilianomatini katika tamthilia ya *Utangamano Wetu Ushindi Wetu* (2017).” Uchunguzi wao ulibaini kuwepo kwa mwingilianomatini unaofungamana na historia ya mtunzi na malezi ya mwandishi kidini, kiutamaduni na kimaadili, kijamii na kitaaluma kwa namna moja ama nyingine. Tofauti na utafiti wao ambao ulihusisha mwingilianomatini na historia ya mtunzi, utafiti huu ulinuia kuchunguza athari ya tamthilia ya *Mashetani* (1971) juu ya *Mashetani Wamerudi* (2016) kidhamira, kimaudhui, kiwahasika na kimtindo.

Ni dhahiri kuwa wapo watafiti wa hapo awali waliohakiki tamthilia ya *Mashetani* (1971) lakini hakuna yeyote aliyehakiki tamthilia hii kwa mwelekeo wetu ambapo

tunachanganua athari ya tamthilia ya *Mashetani* (1971) juu ya tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Vipengele mbalimbali kama vile maudhui, wahusika na mtindo huingiliana na kujengana. Ni kutokana na haya ambapo tulitaka kudhihirisha jinsi matini hizi mbili zinavyoingiliana na kuchangiana.

1.7 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini iliyoasisiwa na Julia Kristeva (1966). Hata hivyo, nadharia hii iliendelezwa na mtaalamu Bakhtin (1984), Fairclough (1992) na wataalamu wengineo. Kulingana na Allen (2000) neno mwingilianomatini lilitumika kwa mara ya kwanza katika lugha ya Kifaransa katika matini iliyoandikwa na Kristeva katika miaka ya sitini. Asili ya nadharia hii inahusishwa na mwanausemezano Bakhtin Mikhail Mikhailovich na Mwanaisimu Ferdinand de Saussure. Mwanafasihi Allen (2000) anaelezea Nadharia ya Mwingilianomatini katika kitabu chake cha *Intertextuality* kwa kutaja na kueleza mirengo mbalimbali ya mwingilianomatini ambayo imefafanuliwa na wanamwingilianomatini tofauti. Kulingana naye, waandishi wa kazi za kifasihi hawachagui maneno pekee kwenye mfumo wa lugha bali pia huchagua ploti, fani, wahusika, ishara, mbinu za utambaji misemo na sentensi kutoka kwenye matini za hapo awali.

Kulingana na mtazamo wa kiisimu wa De Saussure (1974), hakuna ishara iliyo na maana ya kipekee bali kila ishara hupatikana katika mfumo wa lugha na hutoa maana kutokana na mfanano na utofauti kutokana na ishara zingine. Maelezo ya kiisimu ya ishara na mfumo yaliyotolewa na de Saussure yanahusishwa zaidi kama asili ya Nadharia ya Mwingilianomatini. Bakhtin (1981, 1984) ana mtazamo tofauti na de Saussure kuhusu lugha kwani anashughulika na jinsi maneno yanavyobadilishwa

katika sajili mbalimbali. Bakhtin ni mwasisi wa Nadharia ya Usemezano. Kulingana naye dayolojia si mazungumzo kati ya wahusika bali ni ule upekee wa nafsi. Nafsi hii hujumuisha mtazamo wa wahusika kuhusu dunia, hali ya kuhutubu, itikadi na jamii. Anaeleza kuwa hali hizi hujitokeza kupitia maneno yanayotumika na wahusika. Bakhtin (1984) anaeleza zaidi kuhusu maisha ya neno kwa kusema kuwa neno huhamishwa kutoka mdomo mmoja hadi mwingine na kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa hivyo neno haliwezi kujiondoa kwenye sajili iliyotumika.

Kulingana na Bakhtin, fasihi ni njia nyingine ya mawasiliano. Anaeleza kuwa katika matini za kifasihi maneno ni muhimu sana katika dayolojia inayojitokeza kupitia maneno yanayotumika na wahusika mbalimbali. Bakhtin (1981; 1984) anasema kuwa matini ni uwanja ambao una mwingiliano wa kusemezano baina ya sauti mbalimbali za usemi. Mawazo haya ya Bakhtin yanafafanuliwa zaidi na wanamwingilianomatini kama vile; Roland Gerard Barthes, Gerard Genette, G, Bloom na Julia Kristeva.

Kwa mujibu wa Kristeva (1980), waandishi hawatungi matini zao kutokana na ubunifu wao bali wao huandika kutoka kwa matini zilizoandikwa hapo awali. Kristeva anaendeleza mawazo ya Bakhtin ya kidayolojia yanayoelezea dhana ya kuwepo kwa wingi-sauti wa lugha. Kristeva anafafanua kuwa pana mawasiliano kati ya mwandishi na msomaji kwa kuwa matini hujumuisha matini za hapo awali.

Kulingana na Barthes (1977), asili ya matini haitokani na dhamira ya mwandishi bali hutokana na maneno mengine, semi zingine na matini zingine. Anaeleza kuwa maana ya maneno yaliyoandikwa na mwandishi wa matini haitokani na dhamiri ya mwandishi wa matini hiyo bali hutokana na nafasi ya maneno hayo kiisimu na katika mifumo ya kitamaduni. Vilevile, anaeleza kuwa kila neno, sentensi, aya, au matini inayoandikwa na mwandishi inatokana na mfumo wa lugha iliyotungwa kwayo.

Kulingana na Genette (1982), kazi za fasihi si asili bali hutokana na mkusanyiko wa mifumo mbalimbali. Kulingana na Genette mwingilianomatini ni uhusiano uliopo kati ya matini mbili au kati ya matini kadhaa. Anaeleza kuwa mwingilianomatini ni kuunganisha matini iliyoandikwa sasa na matini iliyoandikwa hapo awali. Vilevile, anasisitiza kuwa mwingilianomatini ni hali ya kuandika kile ambacho kishaandikwa tayari.

Bloom (1975) anaeleza kuwa ushairi na fasihi kwa jumla huiga matini za hapo awali. Anafafanua kuwa mwingilianomatini huhusisha sababu za watu kuandika kwa kufuata mfumo wa utamaduni ambapo kila kinachoandikwa huwa tayari kimeandikwa. Harlod anashikilia kuwa katika fasihi huwa kuna matini maalum zinazolingiliana.

Wafula na Njogu (2007) wanamnukuu Bakhtin (1981;1984) na kueleza kuwa kazi ya fasihi ni uwanja ambao una mwingiliano wa matini. Kazi ya fashi ina sauti mbalimbali zinazolingiliana na kupiga mwangwi katika kazi nyinginezo zilizotangulia, zilizopo, au zitakazokuja baadaye. Bakhtin anasisitiza kuwa matini ni uwanja ambao una mwingiliano wa kusemezano baina ya sauti mbalimbali za usemi. Hii ina maana kuwa hakuna matini ambayo ni asilia zaidi.

Kulingana na Kristeva waandishi hutunga matini zao kutokana na matini za awali. Kristeva (1980) na wanamwingilianomatini wengine kama Bloom (1994) na Barthes (2002) wanaamini kuwa msomaji wa pekee ni mwandishi asomaye matini nyingine, hali inayosababisha matini kujisoma na kujiandika yenyewe. Wamitila (2002) anasema sifa za mwingilianomatini zinajitokeza kwa njia kadhaa kama mwangwi wa dhamira au maudhui. Hii ina maana kuwa msomaji anaweza kurejelea matini mojawapo katika kusoma nyingine. Kulingana na Bakhtin kazi ya fasihi ina sauti

mbalimbali zinazolingiliana na kupiga mwangwi katika kazi nyinginezo zilizotangulia, zilizopo au zitakazokuja baadaye. Bakhtin anadai kwamba matini ni uwanja ambao una mwingiliano wa kisemezano baina ya sauti mbalimbali za usemi. Kila matini inarejelea matini nyingi zilizokuwepo, zilizopo na za wakati ujao.

Mawazo ya Bakhtin ya Kisemezano yalifafanuliwa kwa njia mbalimbali ambazo ni Wingi-sauti, Mwingilianomatini, Kronotopu, Kanivali na Kanitovu. Kristeva alichukua dhana ya Usemizano na kuifafanua zaidi. Kulingana na Kristeva hakuna matini yoyote inaweza kuangaliwa kivyake au kujitegemea.

Kaui (2015) anamnukuu D' Angelo (2010) ambaye anasema kuwa kila matini huhusiana na matini nyingine kwa njia ya urejereaji, unukuzi, ukopaji, usimilisho, udokezi, uigizaji wa kubeza, uigizaji, na njia nyinginezo. Aidha Kaui (2015) anamnukuu Dean (2009) ambaye anaeleza kuwa hadithi huibuka katika jamii na kizazi fulani cha jamii hiyo huzibadilisha hadithi za jadi ili ziweze kuafikiana na wakati uliopo, mazingira mapya na mahitaji ya wakati huo pamoja na njia zake za uwasilishaji. Dhana ya mwingilianomatini inasisitiza kuwa matini zote za kisanaa zinaweza kuchukuliwa kama matini moja kuu. Matini zote huhusiana kwa njia moja au nyingine na matini zenyewe hutegemeana ili kuzidisha maana.

Mihimili mikuu ya Nadharia ya Mwingilianomatini ni pamoja na:

- a) Hakuna matini yoyote ile ya kifasihi ambayo inaweza kuangaliwa kivyake. Mihimili huu utatusaidia kuhakiki tamthilia ya *Mashetani* na tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* kidhamira na kimaudhui.
- b) Kazi ya fasihi huundwa kutokana na mifumo ya kanuni za tamaduni zilizowekwa na kazi tangulizi za kifasihi ambazo taswira za maisha ya kawaida na uhusiano wa kimaana huunganishwa na kubadilishwa. Mihimili

huu ulitusaidia katika kuhakiki tamthilia ya *Mashetani* na ile ya *Mashetani Wamerudi* zinavyoingiliana kimtindo.

- c) Kila usomaji wa matini huwa ni kijalizo cha matini tangulizi na hivyo basi huigeuza kwa kiwango. Kwa jinsi kauli hii inayonukuliwa hubadilika na kuelezea kauli asilia kwa kuambatanisha na muktadha mwingine wa kiisimu na kijamii. Mhimili huu utatusaidia kubaini jinsi tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* na tamthilia ya *Mashetani* zinavyoingiliana kimandhari na kiwahasika.

1.8 Mbinu za Utafiti

Kwa mujibu wa Mishra na Alok (2011), mbinu za utafiti ni mchakato wa kisayansi unaoshirikisha ujuzi maalumu katika kufanikisha utafiti. Utafiti huu ulilenga sehemu zifuatazo katika mbinu za utafiti: mahali pa utafiti, muundo wa utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa matokeo pamoja na hitimisho.

1.8.1 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani. Mtafiti alisoma tamthilia ya *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016) ili kutathmini maudhui, dhana ya wahusika na uhusika na mtindo katika tamthilia husika. Vilevile, majarida, makala, usakuraji mtandao na tasnifu nyingine za kifasihi zilisomwa ili kukusanya data iliyohitajika katika kuelewa Nadharia ya Mwingilianomatini pamoja na yaliyoandikwa kuhusu mada hii.

1.8.2 Muundo wa Utafiti

Kwa mujibu wa Poe na Mays (2020), utafiti wa kimaelezo hujikita na matumizi ya maelezo katika mfumo wa sentensi kama data ya kuchanganua matukio mbalimbali. Utafiti huu ni wa kimaelezo unaohusu usomaji na ufafanuzi wa dhana mbalimbali

zinazolinganishwa na kubainishwa kati ya tamthilia ya *Mashetani* (1971) na tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Sentensi zilidondolewa katika matini husika ili kuchanganua data hiyo kwa mujibu wa maswali na malengo ya utafiti.

1.8.3 Uteuzi wa Sampuli

Mtafiti alibainisha athari ya tamthilia ya *Mashetani* (1971) juu ya tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) kimaudhui, kiwahasika na kimtindo. Tamthilia hizi mbili zimeteuliwa kwa mbinu kusudio ili kupata data iliyofanikisha mahitaji ya utafiti huu. Emmel (2013) anaeleza kuwa mbinu kusudio katika uteuzi wa sampuli humhitaji mtafiti kuwa na uhakika kuwa sampuli hiyo inaingiliana na malengo ya utafiti na vilevile itajibu maswali ya utafiti. Isitoshe, mtafiti alijikita katika utanzu wa tamthilia wa fasihi andishi.

1.8.4 Ukusanyaji wa Data

Usofaji wa kina ulifanywa na mtafiti ambapo alisoma tamthilia teule ili kupata data iliyosukuma utafiti huu mbele. Data ya utafiti ilikuwa sentensi teule zilizodondolewa katika tamthilia hizi mbili; *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016). Kwa kila tamthilia teule mtafiti aliitathmini kwa kuzingatia misingi ya Nadharia ya Mwingilianomatini kwa kuchanganua jinsi tamthilia ya *Mashetani* (1971) ilivyoathiri tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) kimaudhui, kiwahasika na kimtindo. Ibainike kuwa matukio ya kimaelezo yaliyodondolewa katika tamthilia teule ndiyo data ya mtafiti.

1.8.5 Uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa kwa kuongoza na malengo ya utafiti ilichanganuliwa kupitia uchanganuzi wa maneno, virai, vishazi na aya katika tamthilia husika. Mtafiti alibainisha athari ya *Mashetani* (1971) juu ya *Mashetani Wamerudi* (2016) kimaudhui, kiwahasika na kimtindo ili shabaha ya utafiti wa tamthilia hizi ubainike.

Majina ya wahusika yalitambuliwa na dhima zao kuonyeshwa. Kwanza, maudhui ya *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016) yaliainishwa na kulinganishwa ili kubaini athari za *Mashetani* kwa *Mashetani Wamerudi*. Pili, mtafiti alionyeshwa iwapo wahusika wa *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016) wameathiriana. Mwisho, mitindo katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) ulilinganishwa.

1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Data iliwasilishwa kwa njia ya kinaelezo. Mtafiti alitoa mifano na maelezo ya maudhui, wahusika pamoja na uhusika wao na mtindo katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) ambayo ilifafanuliwa kwa kuongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini. Kwa namna hii, mtafiti aliyajibu maswali ya utafiti.

SURA YA PILI

ATHARI ZA MAUDHUI YA *MASHETANI* (1971) KWA MAUDHUI YA *MASHETANI WAMERUDI* (2016)

2.0 Utangulizi

Sura hii inaeleza kwa kina uhusiano uliopo baina ya tamthilia zilizotungwa na watunzi Ebrahim Hussein, tamthilia ya *Mashetani* (1971) kwa upande mmoja na Said A. Mohamed, tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) kwa upande mwingine. Hususan, lengo kuu la sura hii ni kulijibu swali la kwanza katika utafiti huu linalonua kudadisi kwa kina jinsi tamthilia ya *Mashetani* (1971) iliyoandikwa na Ebrahim Hussein ilivyoathiri uandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) iliyotungwa na Said A. Mohamed kimaudhui. Hivyo basi, utafiti huu wa kimaudhui unaofuatia katika sura hii umefuata mrengo wa kutaka kutathmini tamthilia hizi zilizoandikwa nyakati tofauti hasa kikanne zinavyofanana au kutofautiana kimaudhui. Katika kufanya hivi, utafiti utaongozwa na nadharia ya mwingilianomatini kama ilivyoelezwa na mwanaisimu wa Kifaransa Julia Kristeva mwisho wa 1960 alipokuwa akirejelea kazi za Bakhtin kuhusu usemezano (Childs & Fowler, 2006; Njambi, 2023).

Mohamed (1995) aeleza kuwa maudhui ni mkusanyiko wa maswala anayokusudia kueleza mtunzi wa kazi ya tamthilia kwa mujibu wa utafiti huu. Bila kuzama katika uchambuzi, ni muhimu kufafanua katika kijisehemu hiki kwamba utafiti katika sura hii unapeana uzito katika jitihada za kuelewa athari za maudhui ya *Mashetani* (1971) kwa maudhui ya tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Lengo hili linatokana na maelezo yanayotolewa katika kazi ya Mose, Obuchi na Mosol (2020) inayodokeza kwamba maudhui katika kazi ya Hussein Mohamed ya *Mashetani* yana mfanano mkubwa na maudhui yanayomulikwa katika kazi ya *Mashetani Wamerudi*

iliyoandikwa takriban miaka arubanne na tano baadaye na Said A. Mohamed. Mfanano huu unabainika kutokana na maelezo ya kinadharia ya mwingilianomatini ulioongoza utafiti huu. Kwa mujibu wa Njambi (2023), matini yoyote ya fasihi hunukuu, huiga au vilevile kurejelea kwa njia moja au nyingine matini ya awali. Hivyo basi kwa mujibu wa nadharia ya mwingilianomatini ambayo iliainishwa na mwanafasihi Julia Kristeva mnano mwisho wa miaka ya 1960, inabainika katika sura hii kwamba kila matini hubuniwa kutokana na matini za awali huku matini za sasa zikiweka msingi hasa wa kuunda matini za siku za usoni (Childs & Fowler, 2006; Njambi, 2023).

Kwingineko, Muusya (2019) aliyefanya udadisi kuhusu Ujumi mweusi unavyojitokeza katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* anakiri kuwa mtunzi Said A. Mohamed ameikuza anwani ya *Mashetani Wamerudi* (2016) hususan kutokana na anwani ya mojawapo ya tamthilia za Ebrahim Hussein inayojulikana kama *Mashetani* (1971). Isitoshe, Mohamed (2016) anakiri katika dibaji ya tamthilia hii ya *Mashetani Wamerudi* (2016) kuwa uamuzi wake kuyaendeleza maudhui ya utandawazi yaliyomulikwa na Ebrahim Hussein katika *Mashetani* (1971) ulitokana na uamuzi wa Ebrahim Hussein kutoandika tamthilia nyingine inayoendeleza kuyafafanua maudhui hayo kwa kina zaidi. Ina maana ya kwamba, utafiti huu ulichochea zaidi na mitazamo tofauti inayoashiria kuwa *Mashetani Wamerudi* (2016) ni uendelezi wa kazi ya tamthilia ya *Mashetani* (1971) iliyotungwa hapo awali na Ebrahim Hussein mwaka wa 1971.

2.1 Watunzi na Mazingira Yao

2.1.1 Ebrahim Hussein: Mwanatamthilia

Udadisi wa maisha ya mtunzi Ebrahim Hussein unaonyesha kwamba mtunzi huyu mahiri wa tamthilia ni mojawapo wa watunzi hodari wa tamthilia na kazi nyinginezo za fasihi andishi. Ebrahim Hussein alizaliwa mwaka wa 1943. Kulingana na Mose (2021), mtunzi Ebrahim Hussein alizaliwa mkoa wa Lindi, nchini Tanzania, kanda ya Afrika Mashariki. Kulingana na unchunguzi uliofanywa na Massoud (2013), eneo hasa la uzaliwa wake lapatikana pwani ya kusini ya nchi ya Tanzania. Eneo alilozaliwa mtunzi Ebrahim Hussein lina ushawishi mkubwa katika uandishi wa wake, hasa uandishi wa tamthilia ya *Mashetani* (1970). Muhimu zaidi katika kuzielewa kazi za kifasihi za mwandishi yeyote ni wakati alimozaliwa mtunzi wa kazi za kifasihi maana wakati huwa na ushawishi kwa kazi za mwandishi yoyote (Mohamed, 1995).

Ina maaana kwamba aghalabu mazingira anamozaliwa mwandishi huwa na ushawishi wa kumpa mwelekeo fulani mwandishi au mtunzi wa kazi ya kifasihi. Hivyo basi, hii ni wazi kwamba Ebrahim Hussein alizaliwa wakati wa ukoloni (1943), tarehe hasa ya kuzaliwa kwake ikiashiria nyakati za utawala wa mabeberu nchini Afrika Mashariki (Massoud, 2013). Akieleza makubaliano na mtazamo huu, Mose (2021) anaeleza kwamba huu ulikuwa wakati ambao utawala wa mkoloni ulikuwa umeshamiri barani Afrika na kushika hatamu za uongozi katika nchi mbalimbali barani humu ikiwemo nchi ya Tanzania inayopatikana kanda ya Afrika Mashariki.

Hatamu za masomo ya mwandishi hujitokeza vilevile katika mazingira yanayochangia utunzi na mada au maudhui anayoyamulika mwandishi wa kazi ya

kifasihi. Kwa sababu hii, ni muhimu kumulika mazingira aliyosomea mtunzi Ebrahim Hussein.

Massoud (2013) anaeleza kwamba mtunzi Ebrahim Hussein aliyatimiza masomo yake ya kifasihi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nchini Tanzania mnamo mwaka wa 1960. Ina maana mazingira haya ya masomo yalichangia utunzi wa tamthilia ya *Mashetani* kwani mada anazozingumzia zaonyesha bayana sababu yake kuitilia mkazo mada na maudhui ya ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo (Shivji, 2002). Hii ni sababu mwaka wa 1960 alipokuwa akiingia chuo kikuu mtunzi Hussein uliashiria wakati ambao utawala wa mkoloni nchini Tanzania ulikuwa ukikaribia kikomo huku nafasi yake ikichukuliwa na utawala wa ukoloni mamboleo. Baada ya masomo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Ebrahim Hussein alienda nchi ya Ujerumani ambako alisomea Shahada ya Uzamifu katika Sanaa za Maonyesho na Historia ya Tamthilia katika Chuo Kikuu cha Humbolt, nchini Ujerumani (Massoud, 2013).

Umuhimu wa mazingira ya nchi ya Ujerumani alimosomea Ebrahim Hussein kwa utunzi wa tamthilia ya *Mashetani* wajitokeza katika uwezo wa mtunzi huyu wa kuutathmini uhusiano uliopo baina ya mkoloni (shetani) na anayenyanyaswa (mwafrika) katika tamthilia husika (Shivji, 2002). Tajriba ya mtunzi Ebrahim Hussein katika tamthilia na kazi za michezo ya kuigiza ni mojawapo ya tajriba tajika mno katika kazi za kifasihi. Mose (2021) anaeleza kwamba mtunzi huyu ameandika takriban sanaa sabini na saba za maigizo na maonyesho hii ikiwa sababu kuu ya umaarufu wa kipekee alohitimu sio tu katika kanda ya Afrika Mashariki bali ulimwengu mzima. Kulingana na Massoud (2013), umahiri wake katika utanzu wa tamthilia unabainika bayana kupitia tamthilia zake kama *Kinjekitile* (1969), *Kwenye*

Ukingo wa Thimu (1988), *Arusi, Jogoo Kijijini* (1976), *Ngao ya Jadi* (1976), na *Wakati Ukuta* (1971) bila kusahau tamthilia husika ya *Mashetani* (1971) inayodadisiwa katika utafiti huu. Pindi tu baada ya kuhitimu masomo nchini Ujerumani, Ebrahim Hussein alirejea nchini Tanzania na kujitosa katika ulingo wa uhadhiri katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam alipofunza kazi za fasihi. Mtafiti wa kazi hii alibaini kwamba safari yake ya masomo nchini Ujerumani na kurejea kwake nchini na kufunza fasihi humu nchini Tanzania zimechangia pakubwa mada na maudhui anayoyapiga msasa katika tamthilia ya *Mashetani* (1971).

Ufundi wa Ebrahim Hussein katika kazi za Kiswahili na Fasihi unajibainisha kupitia tajriba yake ya kufunza lugha na fasihi katika vyuo vikuu kando na zawadi aina aina alizojizolea katika Nyanja za utunzi wa tanzu tofauti za fasihi andishi (Matundura n.w, 2017). Hii ni kama anavyoelezea Mose (2021) kwamba mtunzi Ebrahim Hussein baada ya kurejea nchini Tanzania pindi alipomaliza masomo nchini Ujerumani alijitosa katika shughuli za kufunza sanaa za maonyesho na maigizo kuanzia mwaka wa 1975 na kutamatisha mwaka 1985 ili kuweza kuweka kikomo kwa tajriba hii ya miaka mingi mnamo mwaka 1988. Ina maana kwamba mtunzi Ebrahim Hussein alijihusisha na taaluma ya uhadhiri kwa zaidi ya kipindi cha mwongo mmoja miaka hii ikioana na wakati ambapo ukoloni mamboleo ulikuwa ukichukua hatamu barani Afrika baada ya kufifia na kudorora kwa ukoloni mkongwe uliodhaniwa umekufa zilipopata uhuru nchi za Afrika mashariki miaka ya sitini. Kwa sababu ya maudhui makuu ya wakati huu kuangazia mtazamo mkuu wa wakati wa miaka hii (1970-1988), yaeleweka kwa urahisi sababu ya Ebrahim Hussein kuangazia hasa maudhui ya ukoloni mamboleo na wala si ukoloni mkongwe uliokuwa umeanza kutoweka barani Afrika isipokuwa kwa nchi chache tu barani humu ikiwemo nchi ya Afrika kusini (Gaudioso & Minerba, 2020). Sababu hii inaeleza mojawapo ya mambo

yaliyomsukuma Ebrahim Hussein kutunga tamthilia ya *Mashetani* (1971) na hasa maudhui yake makuu ya ukoloni mamboleo. Weledi wake katika uwanja wa tamthilia unajitokeza katika ushindi alioubuka kama mwandishi bora zaidi wa maigizo ya lugha ya Kiswahili kwa kujinyakulia tuzo ya Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania (UWAVITA) (Mose, 2021).

Isitoshe, ni muhimu kuchunguza kwa kina umbo au mtindo anaoufuata katika utunzi wa tamthilia zake mtunzi Ebrahim Hussein. Mojawapo ya maswala muhimu zaidi anayoyazingatia Mose (2021) anapozidadisi sanaa za maoyesho na tamthilia za Ebrahim Hussein zinazohusu umbo au mtindo wa utunzi wa mwanatamthilia huyu. Kulingana na Mose (2021), ni bayana kuwa tamthilia zote za mtunzi Ebrahim Hussein zinafuata moja kwa moja na kuzingatia umbo na vilevile mtindo wa ki-Aristotle. Kulingana na maelezo yanayotolewa na Clemence (2015) kuhusu nadharia ya Ki-Aristotle inayotambulika vilevile kama nadharia ya Urasmi mkongwe, hii ni aina ya nadharia inayoshabikiwa na kufuatwa kama mwongozo na wasanii wengi mno wa kuigiza barani Ulaya. Chimbuko hasa la nadharia ya ki-Aristotle ni mojawapo ya kazi zake inayojulikana kwa jina, *Poetics* (Clemence, 2015). Aghalabu, Clemence (2015) anaeleza kwamba kanuni na sheria za utunzi wa kazi za tamthilia hutokana na muongozo unaotolewa na nadharia hii ya ki Aristotle. Clemence (2015) alendeleza maelezo kwa kubashiri kuwa mfumo unaofuatwa katika aina hii ya kinadharia huugawa mchezo wa kuigiza katika vijishehemu sita ambavyo ni pamoja na wahusika, maonesho, msuko, dhamira, nyimbo na matumizi ya maneno. Sehemu kuu tatu zinazofuatwa katika utunzi wa tamthilia kulingana na ugavi uliokusudiwa na kubuniwa na Aristotle ni utangulizi au mwanzo ikifuatiwa na kitendo husika kama sehemu ya pili na kumalizikia sehemu ya tatu ambapo Aristotle humhitaji msomaji kuibwa (Clemence, 2015). Kwa wajibu wa mwingiliano wa utunzi na mfumo wa Ki-

Aristotle, mtunzi Ebrahim Hussein alitunga tamthilia yake ya *Mashetani* (1971) pamoja na tamthilia nyingine zake zote kwa kufuata mtindo huu (Gaudioso & Minerba, 2020). Hii ndiyo sababu hasa ya tamthilia zake kama *Mashetani* kuwa na nyimbo, wahusika tofauti, dhamira (lengo), matumizi ya maneno na vilevile msuko zikiambatana na maonyesho.

Kueleza kuwa Ebrahim Hussein aliutegemea na kuufuata mtindo au umbo la ki-Aristotle pekee katika utunzi wake ni kumnyima heko anazozistahili kwa ufundi usio kifani aliouonyesha katika mfumo wa tamthilia zake hasa ya *Mashetani*. Hii ni sababu kando na kuufuata mtindo huo, mtunzi Ebrahim Hussein alizifanyia majaribio sanaa za maonyesho ya kijadi ya kiasia kwa kuoanisha mbinu mbalimbali za sanaa hizo ili kuzindua tamthilia zake kama ile ya *Mashetani* kwa ubunifu wa hali ya juu (Mose, 2021). Baadhi ya mbinu tofauti za sanaa ya kimaonyesho ya jadi alizozifuata na kuzipa matumizi katika tamthilia zake kama ya *Mashetani* ni kama vile kuchanganya miviga ya kijamii na sherehe pamoja na mbinu asili za kuzalisha mali zikiwemo mazingaombwe, na matambiko (Khamis, 2005; Mose, 2021). Ebrahim Hussein hakuachia hapo kwani ubunifu wake ulimshuhudia akichanganya mbinu hizi na shughuli anuwai za maisha ya kikawaida katika jamii kama vile unyago, matanga, arusi, na jando miongoni mwa tanzu nyinginezo anazozihusisha kupitia uwasilishaji unaochukua mbinu tofauti za sanaa za kimaonesho kama vile malumbano ya utani, majigambo, ngoma, nyimbo na masimulizi (Mwaifunge, 2014; Khamis, 2005; Mose, 2021). Mitindo hii inajitokeza kuwa na ushawishi mkubwa katika utunzi wa tamthilia za Ebrahim Hussein hasa ule wa *Mashetani* (1971) amabapo mbinu kama vile nyimbo, masimulizi, malumbano ya utani na mazingaombwe yanajitokeza wazi (Mwaifunge, 2014; Khamis, 2005; Gaudioso & Minerba, 2020). Ni uwezo huu nadra wa kuzichanganya na kuoanisha mbinu hizi tofauti za maonyesho ya sanaa katika

tamthilia ya *Mashetani* unaowafanya wengi kuushangilia weledi wa mtunzi Ebrahim Hussein kuwasilisha maudhui na ujumbe wake kwa hadhira lengwa.

2.1.2 Said A. Mohamed: Mwanatamthilia

Kwa mujibu wa M'Raiji (2021) wasifu huhusu maelezo ya kipekee kuyahusu maisha, tabia, mienendo na matendo ya mwandishi kuanzia wakati wa kuzaliwa kwake. Aghalabu wasifu huandikwa na mtunzi mwingine anayeyatafiti au kuyafahamu maisha ya mtu mwingine hivyo kufafanua maswala ya kimsingi kuhusu mwanzo, kukua, elimu, ujuzi, na kazi ya mtu mashuhuri katika uwanja fulani. Hivyo basi, utafiti wa maisha ya mtunzi Said Mohamed uliofanywa na wadadisi wengine wa kazi za fasihi andishi unatoa maelezo mahususi kuyahusu maisha ya mtunzi huyu, tamthilia yake na mazingira yaliyomchochea kuibuni na kuandika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Kulingana na Mose (2021) akiungwa mkono na Kwambai (2022), mtunzi Said A. Mohamed ni kati ya watunzi tajika katika kazi za kifasihi. Mose (2021) aendelea kueleza kwamba mtunzi Said A. Mohamed alizaliwa sehemu ya Pemba, kisiwani Zanzibar mnamo tarehe 12, Desemba, 1947. Kuongezea kwa haya, Muusya (2019) Pamoja na Florova (2007) wanasema kuwa Said A. Mohamed sio tu mwandishi wa tamthilia bali mtunzi mwenye ufundi wa kiwango cha juu katika fani mabalimbali za kifasihi zikiwemo utunzi wa riwaya, na vilevile diwani za mashairi na hadithi fupi. Osore (2016) vilevile anasitiza kwamba mtunzi Said A. Mohamed sio tu mtunzi wa tamthilia bali pia mtunzi wa kazi nyinginezo za kifasihi.

Kutokana na umuhimu wa mandhari alimokulia mtunzi wa kazi za kifasihi kwa utunzi wake wa kazi za kifasihi, ni lazima kuangazia mandhari ya Said A. Mohamed ili kuzielewa kazi zake kwa njia barabara. Kwa mujibu wa Makena (2018) mandhari ni mojawapo ya vipengele muhimu zaidi vya fasihi inayosaidia kuelewa mazingira

yaliyochochea utunzi wa mwandishi wa kazi za kifasihi. Ina maana kwamba mandhari ya mwandishi hueleza kwa mapana na marefu kuhusu nyakati, mahali na matukio yanayomchochea na kumsukuma mwandishi kutunga kazi fulani za fasihi (Makena, 2018). Hivyo basi mandhari ya shule alimosomea mtunzi Said A. Mohamed yanapewa kipaumbele katika kuelewa maudhui anayoyafafanua katika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi* (2016) maana ni sehemu ya mazingira ya mtunzi wa kazi za fasihi. Said A. Mohamed alosomea katika shule ya wavulana ya Wete huko kisiwani Pemba kisha baadaye kuendeleza masomo yake katika shule ya Kiembe Samaki iliyopo kisiwani Unguja (Mose, 2021). Vilevile, Mose (2021) aeleza kuwa Said A. Mohamed aliendeleza masomo yake katika shule ya Darajani sehemu ya kisiwa cha Unguja alikohitimu na kujiunga na shule ya upili ya Gulioni iloyotambulika kwa jina, “King George the VI” hapo mbeleni. Ni wakati alipokuwa akiendeleza masomo yake katika chuo hiki cha “King George the VI” ndipo mapinduzi yalipotukia Zanzibar. Kulingana na Mose (2021), mapinduzi haya yalimuwahi akiwa kidato cha pili. Baada ya kuhitimu katika masomo ya shule ya upili au sekondari, mtunzi huyu alielekea mji wa Zanzibar mwaka wa 1966 alikojiunga na Chuo cha Taaluma ya Ualimu cha Nkurumah TTC. Ina maana kuwa mandhari ya elimu ya Said Mohamed yalichochea maudhui aliyoangazia katika tamthilia zake ikiwemo ya *Mashetani Wamerudi* ambayo inamulika maudhui kama yale ya ukoloni mkongwe.

Kwingineko ni muhimu kuiangazia tajriba ya mtunzi Said A. Mohamed kwa minajili ya kuelewa mazingira yaliyochochea maudhui anayoyatilia mkazo katika tamthilia zake hasa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) inayofanyiwa utafiti katika kazi hii. Pindi tu baada ya kuhitimu, Said A. Mohamed aliajiriwa kama mwalimu katika Shule ya Msingi ya Kizimbani kwa kipindi kisichozidi wiki mbili na kujiunga na Shule ya Upili ya Utaani mnamo mwaka wa 1969 hadi 1974 alikokua akifunza

masomo ya Bayolojia (Viumbe hai), Hesabu na Sayansi vilevile masomo ya Lugha ya Kiswahili na Kemia (Mose, 2021). Ijapokuwa hangeweza kuendeleza masomo yake moja kwa moja katika kidato cha tano na sita kutokana na marufuku yaliyopigwa na hayati Rais wa Mapinduzi wa Zanzibar wakati huo, Njenga Karume, aliikumbatia nafasi hio pindi tu ilipojitokeza awamu nyingine alipokuwa akiendelea kufanya kazi. Upungufu alokumbana nao ukamsababisha kutopata vifaa vya maabara ya majaribio ya kisayansi katika kidato cha tano na sita hivyo Said A. Mohamed kujipata katika njia ya kujibidiisha kuwa mtaalam wa taaluma ya Sanaa huku akisomea Fasihi na Lugha ya Kiswahili (Kenduiywa, 2022; Mose, 2021). Masomo haya yalimchochea vilivyo mtunzi Said kuzibuni tamthilia zake ikiwemo ya *Mashetani Wamerudi* kwani yalimlazimu kudurusu Sanaa katika fasdihi kwa njia ya kipekee. Baadaye. Mwaka wa 1976 ulimwona Said A. Mohamed akiendeleza masomo ya shahada ya Isimu na Fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hii ikiwa shahada yake ya kwanza ya ualimu. Mose (2021) anasema kwamba shahada alioiafiki katika masomo haya ilimpa upeo uliomwezesha kuajiriwa kuwa mwalimu mkuu wa shule za msingi na zile za upili za Hamamni sehemu ya Unguja. Kwa mujibu wa maelezo yanayotolewa na Mose (2021) Said Mohamed alijiuzulu kutoka ajira ya ualimu kisha akajiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam alikojitahidi kusomea shahada ya uzamili ya Isimu Tekelezi. Baada ya kutambuliwa na mwanahistoria mashuhuri mjerumani kwa jina Sigmund Bruner aliyejulikana kwa weledi wa Historia na Isimu Linganishi, alipata nafasi ya kuendeleza masomo nchini Ujerumani alikosomea shadaha ya uzamifu Chuo Kikuu cha Karl Marx, Leipsig mwaka 1981 na kuhitimu mwaka wa 1985.

Aliporudi nchini Zanzibar, Bw. Idris Abdul alimteua kama mkurugenzi mkuu wa Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni ambayo baadae ilibadilishwa jina na kuwa

Chuo Kikuu cha Zanzibar-Suza (Kenduiywa, 2022; Mose, 2021). Muda mfupi baadae, alihamia nchini Kenya kwa sababu za kisiasa na kufunza kama mwenyekiti wa Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Moi mnamo 1987. Vilevile alifunza Chuo Kikuu cha Nairobi, nchini Kenya mpaka mwaka wa 1990 aliposafiri nchini Japan kwa sababu za kibinafsi nakujiunga na Chuo Kikuu cha Osaka nchini humo ili kuendeleza masiomo katika idara ya lugha za kigeni alikopandishwa cheo na kuwa Profesa chuoni humo (Muusya, 2019). Baadaye, alihamia nchi ya Ujerumani alikojiunga na kufunza katika Chuo Kikuu cha Bayreuth alikoendeleza taaluma yake ya ualimu hadi kufikia mwaka wa 2012 (Aiello, 2018). Masomo alioyaendeleza na vilevile muda aliouchukua kufunza katika vyuo vikuu nchi za ughaibuni, hasa Ujerumani yana uwezo mkubwa wa kuchangia mtazamo wake wa uhusiano baina ya wakoloni na nchi za bara Afrika hususan uhusiano baina ya Tanzania na Ujerumani kama inavyojitokeza katika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi* (2016).

Yapo matukio katika maisha ya mwandishi huyu yaliyochangia pakubwa mwelekeo aliouchukua katika kubuni tamthilia zake. Mojawapo, ya mambo haya ni mashindano ya hadithi fupi yaliyoandaliwa na Idhaa ya BBC, Kiswahili yaliyowahusisha waandishi wa hadithi fupi katika lugha ya Kiswahili (Kenduiywa, 2022). Ushindi wa hadithi yake kwa jina, “Sadiki Ukipenda” ulianika umaarufu wake na kumjengea jina si haba hivyo kumchochea kuzama katika utunzi sio tu wa hadithi fupi pekee bali pia wa tamthilia kama ile ya *Mashetani Wamerudi* (2016) (Mose, 2021). Kando na swala hili, Katutu (2013) anasimulia kwamba mtunzi Said Hussein ni bingwa wa kufunza dini ya Kiislamu weledi huu ukiambatana na uwezo wake wa kipekee wa kuziimba nyimbo za unyago vipawa hivi akiwa amevirithi kutoka kwa mama yake mkubwa aliyekua bingwa na nyakanga wa sehemu hizi za fasihi simulizi.

Malezi aliyoyapitia kutoka kwa ushawishi wa mama yake mkubwa katika kuzitunga na kuziimba sehemu hizi za fasihi ndiyo hasa yaliyomwezesha kuwa bingwa wa nyimbo za unyagani na mahiri wa mafunzo ya dini ya Kiislamu. Mtunzi hodari katika tanzu anuwai za Fasihi Andishi, Said A. Mohamed ana ubunifu wa kiwango cha kipekee unaomuwezesha kujumuisha tanzu tofauti za kifasihi katika kazi zake zikiwemo sanaa za kimaonyesho miongoni mwa tajriba nyinginezo za Fasihi Simulizi (Katutu, 2013; Osore, 2016; Florova, 2007; Mose, 2021). Ubunifu huu wa kiupekee unajitokeza bayana katika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi* inayohusisha tanzu tofauti za fasihi simulizi kama inavyojitokeza katika utafiti huu.

2.2 Muhtasari wa Tamthilia

2.2.1 Tamthilia ya *Mashetani* (1971)

Uchunguzi wa kazi za Hussein unaonyesha kuwa hii ni mojawapo wa kazi muhimu sana za mwanatamthilia huyu. Tamthilia hii iliyochapishwa mnamo mwaka 1971 ni ya nne ya mtunzi Ebrahim Hussein (Philipson, 1989; Ngesa, Matundura na Kobia, 2015). Kulingana na Ngesa, Matundura na Kobia, (2015), ni bayana kuwa Hussein katika tamthilia hii anamulika swala la ukoloni mkongwe na kudhibitiwa kwa hali hiyo kupitia ukoloni mamboleo hata baada ya nchi za Afrika kupata ‘uhuru wa kibendera’. Hivyo basi, tamthilia hii inamulika ukengeushi unaojibainisha miongoni mwa wasomi wa Kiafrika, namna mkoloni anavyoangusha taasisi za kiafrika kwa kuzizika tamaduni za Kiafrika bila kusahau kumulika na kuzidhibiti miundomsingi zilizoachwa na mkoloni (Karata, Muusya & Mavisi, 2021; Ngesa, Matundura na Kobia, 2015). Hussein (1971) aonyesha kwamba baada ya kuwa chini ya ukoloni, uliwadia wakati Waafrika walipozinduka na kujikaza kupigania uhuru wao hivyo kujipatia nafasi ya kuhusika katika maswala muhimu ya kisiasa, kiuchumi na kijamii

barani Afrika (Philipson, 1989; Karata n.w, 2021). Kulingana na ufafanuzi unaotolewa na Abdalla (2018) pamoja na Fiebach (1997), tamthilia hii ilibuniwa sambamba na wakati jamii anuwai barani Afrika Mahariki zilipokuwa zikikabiliana na mabadiliko katika maswala ya kiuchumi, kisiasa na vilevile kijamii.

Ngesa, Matundura na Kobia (2015) pamoja na Minerba (2017) wanatoa maelezo zaidi kwa kunakili kuwa Hussein aliandika tamthilia hii kipindi ambacho jamii za Kiafrika zilijipata zikikabiliana na athari za tamaduni za kimagharibi zilizorutubishwa na mifumo ya dini na elimu za kigeni barani humu. Tamthilia hii inaonyesha mgogoro kati ya Shetani akiwakilishwa na Juma kwa upande mmoja na Binadamu akiwakilishwa na Kitaru kwa upande mwingine (Minerba, 2017; Fides, 2017). Wahusika hawa wawili wanaigiza kijitamthilia nia yake ikiwa ni kupambanua swala linalowakilishwa na gari la Benz linalomilikiwa na babake Kitaru, aliye mojawapo wa wanatabaka la kinaizi. Ngesa, Matundura na Kobia (2015) wanasema kwamba mgogoro huu unatoa mtazamo wa wahusika tofauti na mienendo yao kama vile Mfaume anayeonyeshwa kuamini kuwepo kwa mashetani na bibi yake Juma anayeonyeshwa akitamani maisha ya kibwanyenye sawia na zamali bali katika tamthilia hii. Hivyo basi, Hussein katika tamthilia hii anasitiza kwamba uhuru wa Mwafrika utapatikana tu pindi njia za kuzidhibiti athari za mkoloni zitakapofwatwa bila kusita.

2.2.2 Tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016)

Udadisi unaofuatia uandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) iliyoandikwa na Said Mohamed unadhihirisha bayana kuwa tamthilia hii inafuatizia, kuisitiza, kufafanua na kurejelea maswala yaliyojadiliwa na mtunzi Ebrahim Hussein katika tamthilia ya *Mashetani* (1971). Hii inawiana na maelezo yanayotolewa na

Njambi (2023) kuhusu nadharia ya mwingilianomatini iliyoongoza utafiti huu inayosisitiza kwa mujibu wa Julia Kristeva kwamba matini moja husemezana na hata kujibizana na matini nyingine. Mohamed (2016) katika dibaji ya *Mashetani Wamerudi* aelezea kwa kina kwamba uandishi wa tamthilia hii uliathiriwa pakubwa na kazi ya kitamthilia ya *Mashetani* (1971) iliyoandikwa hapo awali na Ebrahim Hussein. Hivyo basi, mwingilianomatini unabainika kwani matini ya *Mashetani Wamerudi* (2016) inaonekana kujengwa na kuchochewa hasa na matini ya hapo awali ya *Mashetani* (1971). Kutokana na ufahamu huu, ina maana kwamba tamthilia hii ya *Mashetani Wamerudi* aghalabu inamulika na kutilia mkazo mada alizozizungumzia mtunzi Ebrahim Hussein katika tamthilia yake ya *Mashetani* (1971).

Kama vile mtunzi Ebrahim Hussein anavyomulika swala la ukoloni, yakiwemo maswala ya ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo ndivyo jinsi Said Mohamed anavyolipa uzito swala la ukoloni mkongwe na vilevile swala la ukoloni mamboleo. Katika dibaji ya *Mashetani Wamerudi* (2016), Said Mohamed anakiri kwamba uzito aliouwekea swala la ukoloni mamboleo ulitokana pakubwa na athari ya kazi ya Hussein na hasa uamuzi wa mwantamthilia huyu kumulika maswala ya ukoloni na ukoloni mamboleo (Nzilu, 2018; Mwangi, 2021). Kutokana na ufahamu huu, inabainika kwamba matini yoyote ya fasihi hunukuu, hugeza na mara nyingine kuiga au kurejelea matini za hapo awali kwa njia moja au nyingine (Agiso, 2017; Childs & Fowler, 2006; Bulaya, 2016). Kulingana na tamthilia hii, inajibainisha kuwa lengo kuu la Said Mohamed ni kuonyesha kuwa matatizo yanayoikumba bara Afrika yanasababishwa hasa na shinikizo zitokanazo na nchi zenye uwezo mkuu (uwezo wa kishetani) unaobadili mkondo na nyenzo wanazonuia kuzifuata (Mose, Obuchi na Mosol, 2020).

Katika tamthilia hii, Mohamed (2016) anatilia mkazo jambo hili la ukoloni mkongwe analoeleza kuwa limeendelea kujibainisha kupitia viongozi wa kiafrika waliorithi mifumo ya kijamii, elimu, na uchumi kwa vazi jipya lijulikanalo kama ukoloni mamboleo (Nzilu, 2018). Kwa mujibu wa Obondo (2023), hii ina maana kwamba ukoloni mkongwe haukuisha kwani nchi za barani Afrika zilipata uhuru wa kibendera na zimeendelea kushikwa kati ya wavu wa ukoloni mamboleo. Hivyo basi Mose, Obuchi na Mosol (2020) wanaeleza kuwa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) yaliipa kipaumbele swala la ukoloni mamboleo na athari zake kwa nchi za Afrika athari hizo zikijibainisha kwa kubadilisha mifumo ya kiuchumi, kielimu na kisiasa barani Afrika.

2.3 Athari za *Mashetani* (1971) Kwa *Mashetani Wamerudi* (2016) Kimaudhui

2.3.1 Elimu ya Kigeni

Baadhi ya maudhui yanayorejelewa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) kutokana na athari za tamthilia ya *Mashetani* (2016) ni maudhui ya elimu ya kigeni. Kulingana na Mose, Obuchi na Mosol (2020), tamthilia hizi mbili zimeyarejelea maudhui haya ya elimu kwa kuweka bayana namna elimu ya kigeni ilivyotumika kama chombo cha kumgeuza Mwafrika kuwa kikaragosi cha wakoloni. Tamthilia hizi mbili zinaonyesha namna elimu ya kigeni ilivyouharibu ujamaa na utu wa Kiafrika na kuwafanya Waafrika kuingiwa na kasumba za kikoloni (Mose, Obuchi na Mosol, 2020). Ina maana kuwa punde tu kasumba ya kikoloni iliyoenezwa kupitia elimu ya kigeni ilipowaingia Waafrika, iliwafanya wajidunisha na kujichukua kuwa viumbe duni machoni pa mkoloni atokaye ughaibuni.

Dondoo kadhaa wa kadhaa zaonyesha jinsi elimu ya kutoka ughaibuni ilivyowafanya Waafrika kujidunisha mbele ya mkoloni. Kwa mfano, katika ukurasa wa 51 wa

Mashetani (1971), Kitaru aeleza katika dondoo moja kuwa kuna kitu alichonacho mwenziwe (mkoloni) kinachomfanya yeye kuwa kama mdogo kwake (Hussein, 1971). Kitaru aeleza hayo kama ifuatavyo:

KITARU: Lakini kwa nini nikiwa na wewe ninaona kuwa kuna kitu? Kuna kitu Fulani ulichonacho ambacho kinanitenga mimi na kinanifanya mimi kuwa kama mdogo mbele yako? Siyo unanidharau, lakini unanifanya mjinga. (Uk. 51).

Vilevile, katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016), kijana wa 4 anapotoa dukuduku lake anaeleza kwamba elimu wanayojivunia nchini mwao walikuwa wameirithi kutoka kwa mkoloni. Hivyo basi, tamthilia hizi mbili zaonyesha utaratibu wa kuyatilia mkazo maudhui haya ya elimu ya kigeni ikiwa hasa imezungumziwa kwa mara ya kwanza na mtunzi Ebrahim Hussein kabla ya kusisitizwa na Said Mohamed. Kwa kuwa *Mashetani* (1971) iliitangulia *Mashetani Wamerudi* (2016). Bulaya (2016) na Njambi (2023) wanasema kuwa kila matini hubuniwa kutokana na matini za awali kama inavyojitokeza kwa mujibu wa nadharia ya mwingilianomatini iliyoongoza utafiti huu.

2.3.2 Ukoloni Mkongwe

Vilevile, maudhui yanayochukua sehemu kubwa hasa ya tamthilia hizi mbili za *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016) ni yanayohusiana na maswala ya ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Kutokana na nadharia ya mwingilianomatini iliyoongoza utafiti huu, matini zilizotangulia zinasemekana kuwa na ushawishi mkubwa au uchochezi kwa matini za baadaye au hata za siku za usoni (Childs & Fowler, 2006; Bulaya, 2016; Ngesa n.w, 2015). Mose, Obuchi na Mosol (2020) wanaeleza kwamba Said Ahmed Mohamed ametumia kijazanda mchezo wa mashetani ulotangulizwa na Ebrahim Hussein katika *Mashetani* (1971) kufafanua jinsi dhuluma za ukoloni mkongwe zimechangia na kuchochea asili ya hali za

sintofahamu zinazompata Mwafrika awakilishwaye na binadamu. Hii inabainisha mwingilianomatini unaojitokeza kwani matini ya *Mashetani Wamerudi* (2016) inaonekana kunukuu, kuiga na kurejelea maudhui haya yaliyomulikwa katika matini tangulizi ya *Mashetani* (1971). Katika *Mashetani Wamerudi*, wahusika Prof. pamoja na Kijana 1 wanatumika kudhihirisha dhuluma zitokanazo na ukoloni mkongwe na kufafanua namna zinazochangia hali ya taabu inayomkumba mwafrika (binadamu) (Mose, 2021).

Katika tamthilia ya *Mashetani*, hii inabainika kutokana na matendo ya Shetani (mkoloni) ambaye mwanzoni mwa mchezo “anamvunja viungo vya mwili mwanadamu” na kumlazimu mwanadamu kuyasema maneno asoyafahamu katu (Hussein, 1971 uk 4). Dondoo ifuatayo inabainisha haya kati ya Shetani na Binadamu:

SHETANI: Hebu basi nikunong’onoze, maana siri yenyewe ni kwa lugha ya kishetani. Liseme neno linalokufunza.

BINADAMU: Gashalazeritwas.

SHETANI: Sema nikusikie.

BINADAMU: Gashalazeritwas.

SHETANI: Sema kwa dhati yako...Sasa wacha likuumize. (uk 4).

Kutokana na dondoo hii, inabainika kwamba Shetani anamlazimisha Binadamu kutamka matamshi magumu siyoyafahamu na kumsuta Binadamu aseme kwa kumlazimisha.

Hii ni ishara ya mkoloni kumnyanyasa Mwafrika anayewakilishwa na binadamu. La muhimu mno kujua ni kuwa Said Ahmed Mohamed alikuwa akiyaendeleza maudhui haya ya ukoloni mkongwe katika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi* hivyo kuashiria kurejelea maudhui yalojitokeza katika kazi ya Ebrahim Hussein ya *Mashetani Wamerudi* iliyotungwa mbeleni.

2.3.3 Ukoloni Mamboleo

Ukoloni mamboleo umejitokeza katika tamthilia ya Said Ahmed Mohamed ya *Mashetani Wamerudi* (2016) na tamthilia ya *Mashetani* (1971) hii ikibainisha mwongozo wa nadharia ya mwingilianomatini ambapo matini ya awali inaonekana ikiathiri matini ya hivi karibuni (Kalingwa & Kau, 2023). Kwa mujibu wa Ngesa, Matundura na Kobia (2015) pamoja na Ikuathu (2017), ukoloni mamboleo unasimamia namna utawala wa nchi za kimifumo ya kiubepari huathiri hali na shughli za kiuchumi, kijamii na kisiasa katika nchi zisizo nguvu hasa zilizoko barani Afrika.

Kwa mujibu wa Job (2022) akiungwa mkono na Mose (2021), ukoloni mamboleo ni swala zito linalonua kutawala nchi za barani Afrika na nyinginezo katika ulimwengu wa tatu kwa njia za ushetani pasipo nchi hizo kuelewa namna shetani afanyavyo amwingiapo mwanadamu. Katika tamthilia ya *Mashetani*, Kitaru anaeleza kuwa shetani ni kiumbe kimwingiacho mwanadamu kwa njia anuwai na kumvuruga akili athari zake zikiwa na mvuto mkuu katika maisha ya mwanadamu kiuchumi, kielimu na hata kisiasa (Hussein, 1971 uk. 24; M'Ngaruthi n. w, 2015). Maelezo haya anayatoa kama ifuatavyo katika tamthilia ya *Mashetani* (1971):

KITARU: Shetani, hii nafsi yenye ncha nyingi, ni kiumbe kinachomwingia binadamu kwa namna mbalimbali na kumzuga akili. Shetani hufahamu? Hadithi chungu nzima juu ya shetani na binadamu zinazoeleza vipi Shetani anavyomjia binadamu na kumghilibu kwa sura mbalimbali. (Uk. 24-25)

Maelezo hasa ya ukoloni mamboleo katika tamthilia hizi mbili yanaeleza kwamba ni hali inayotokana na nchi za ughaibuni/magharibi kuthibiti nchi za barani Afrika kielimu, kisiasa, kiutamaduni, kiuchumi na kijamii kwa namna inayofananishwa na kupandwa na mashetani au mizuka katika tamthilia za *Mashetani* na hata katika *Mashetani Wamerudi* (Abdalla, 2018; Mose, 2021). Athari za ukoloni mamboleo katika maswala ya kiuchumi na kimiundomsingi ya nchi za barani Afrika zinajitokeza

kupitia hali ya nchi hizi kunyimwa uwezo au uhuru wa kujiamulia maswala yanayoathiri nchi zao pasipo mkono fiche wa mkoloni. Ina maana kwamba kwenda kwa mkoloni kulimpa Mwafrika uhuru wa bendera tu bila kumpa uhuru halisia aliouhitaji hasa (Korir & Mwamzandi, 2019). Said A. Mohammed katika *Mashetani Wamerudi* (2016) aendeleza maudhui haya ya ukoloni mamboleo yaliyomulikwa hapo mbeleni na Ebrahim Hussein katika *Mashetani* kama njia ya kusisitiza kwamba ndio mojawapo ya chanzo kikuu cha taabu na sintofahamu zinazomkabili mwafrika barani humu. Urudiaji wa maudhui haya ya ukoloni mamboleo katika *Mashetani Wamerudi* (2016) unaashiria kwamba matini za awali huwa na uwezo wa kuziathiri matini za baadaye kama inavyojibainisha katika nadharia ya mwingilianomatini iliyoongoza uchambuzi huu (Agiso, 2017; Korir & Mwamzandi, 2019; Njambi, 2023).

Kusisitiza maudhui ya ukoloni mamboleo, ni muhimu kutathmini kwamba swala hili linamulikwa katika tamthilia hizi mbili za waandishi Ebrahim Hussein na Said Ahmed Mohamed ikiwa ni kuonyesha nafasi duni ya Mwafrika katika kuamua hatima yake hasa katika maswala muhimu ulimwengu mzima. Mwandishi Ebrahim Hussein akiwa wa kwanza baina ya wawili hawa kuiwasilisha hoja hii anaeleza kwamba maudhui haya ya ukoloni mamboleo yanahusu mataifa makuu hasa ya nchi za bara Uropa kuyathibiti na kuamua mwenendo na mwelekeo wa mataifa madogo yapatikanayo hasa barani Afrika kupitia njia fiche au vilevile njia zisizo za moja kwa moja (Musimenta, 2018). Nia hasa ya kuyamulika maudhui haya ni kuonyesha kuwa mataifa ya barani humu Afrika yanaamuliwa hatma yake ya kisiasa na kiuchumi kupitia mkono fiche wa mkoloni aliyeondoka barani humu kipindi cha kwanza cha karne ya ishirini ilhali bado ameendelea kushikilia taasisi kuu za nchi hizi hadi waleo (Waithiru, 2022). Hii ndiyo sababu mpaka wa leo, nyenzo mahususi za uzalishaji mali katika mataifa ya bara la Afrika zimeshikiliwa na kuathiriwa kimwelekeo na mataifa

haya ya kiubepari ya nchi zenye nguvu za barani Uropa (wakoloni) (Oketch n.w, 2020; Waithiru, 2022).

Kwingineko, ukoloni mamboleo unajitokeza katika mazungumzo ya babake Kitaru akinena na mamaye Kitaru kama ifuatavyo:

BABA: Mwafrika bwana. Ndio maana tutakuwa nyuma hivi. Wakati huu sio wakukaa nyuma hivi. Wakati huu sio wa kukaa nyuma. Huu wakati wetu sasa. Namna gani! Mwafrika lazma awe mbele ya watu bwana. (Uk. 24)

Kwa mujibu wa dondoo hii, Babake Kitaru aonyesha tamaa ya kushika hatma za uongozi na kurithi raslimali za nchi kutoka katika mikono ya mabeberu (wakoloni) waliokuwa wakiondoka baada ya kuipa Afrika uhuru wa bendera.

2.3.4 Utabaka

Maudhui mengine yanayojitokeza katika tamthilia ya Said Ahmed Mohamed ni yale ya utabaka. Kwa mujibu wa Hussein (2019), matabaka mawili makuu yajitokezeayo katika tamthilia ya *Mashetani* na kurejelewa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ni yale ya ubwanyenye na unaizi mawili haya yakiwakilishwa na Juma na Kitaru, mbasi wawili. Familia ya Juma katika jamii ya *Mashetani* (1971) inawakilisha tabaka la kibwanyenye lililojulikana kwa matajiri wa kiukoo likiwa limemiliki urithi wa mali mengi kutoka kwa wavyele wa jamii zao. Kwingineko, Kitaru na familia yake wanaashiria tabaka la unaizi linalosimamia wanajamii waliopokea elimu ya Kizungu tabaka hili likiwa lile lililoshika hatamu za uongozi serikalini pindi tu baada ya mapinduzi ya 1964 (Mose, 2021). Hapo baadaye, tabaka la unaizi lilikuja kujulikana kama tabaka la wazungu weusi lililochukua urithi wa mienendo ya kimaisha iliyoachwa nyuma na wakoloni, vyeo pamoja na nyumba zilizoachwa na wakoloni waloiondoka bara ya Afrika nyakati hizo (Kimeu, 2016; Mose, Obuchi na Mosol, 2020). Hii inabainika katika dondoo kati ya mazungumzo ya babake Kitaru na mamake kama ifuatavyo:

BABA: Mwafrika bwana. Ndio maana tutakuwa nyuma hivi. Wakati huu sio wakukaa nyuma hivi. Wakati huu sio wa kukaa nyuma. Huu wakati wetu sasa. Namna gani! Mwafrika lazma awe mbele ya watu bwana. (Uk. 24)

Makena (2018) pamoja na Kimeu (2016) wanaeleza kuwa walipofikia ukomo wao wa hatima za kuziongoza nchi za kiafrika, wakoloni walitararisha tabaka lililochukua mwelekeo wao baada ya kurithi miundo ya dini na elimu kutoka kwao jambo hili likifanyika kabla ya nchi za Kiafrika kupata uhuru miaka ya sitini. Kwa mujibu wa Makena (2018), tabaka hili la unaizi ndilo lililotumika kama chambo cha mkoloni cha kushinikiza na kuyaweka hai matakwa na maslahi yao miongoni mwa mataifa huru ya barani Afrika. Baada ya kipindi cha kuanza kusherehekea uhuru bendera, mataifa haya yalijipata katika hali hii ya kutawaliwa kutoka nchi za ughaibuni. Maswala na mwelekeo wa kiuchumi, kibiashara, kielimu, kijamii na kisiasa katika mataifa haya yaliamuliwa kutoka nchi zenye nguvu hasa zile za bara Uropa zilizokuwa mkoloni wao (Kamwara n.w, 2020; Kimeu, 2016). Kurudiwa kwa maudhui ya utabaka katika *Mashetani Wamerudi* (2016) kunatilia mkazo matumizi ya nadharia ya mwingilianomatini katika kazi hii ambapo athari za matini iliyotangulia zinajitokeza na kurejelewa katika matini ya hivi karibuni (Bulaya, 2016; Kalingwa & Kau, 2023; Childs & Fowler, 2006).

Vilevile, utabaka unajibainisha katika mazungumzo baina ya Baba ya Kitaru na Kitaru kama ifuatavyo:

BABA: (Anajaribu kubadilisha mazungumzo) Rafiki yako Juma anatoka wapi? Ninafahamu anatoka Unguja. Lakini wapi? Sehemu gani? Wazee wake walikuwa wanafanya nini huko?

KITARU: Wazee wake walikuwa wana mashamba ya karafuu. Lakini baada ya mapinduzi serikali ikayachukua.

BABA: Kumbe ndio walikuwa mabwanyenye hawa! Loo! (Uk. 26)

2.3.5 Unyanyasaji na Uonevu

Maudhui ya unyanyasaji na uonevu yanajirudia kwa mara nyingine katika *Mashetani Wamerudi* (2016) baada ya kuangaziwa hasa kwa kina katika kazi ya Ebrahim

Hussein ya *Mashetani* (1971). Hii ni njia inayoonyesha wazi kwamba mtunzi Said Mohamed aliyatilia mkazo maudhui haya baada ya mtunzi Ebrahim Hussein kumuathiri kwa namna kuu hivyo kubainisha matumizi ya nadharia ya mwingilianomatini inayosisitiza kwamba matini yoyote huwa ni urejeleaji au ubunifu unaotokana na matini za hapo awali (Bulaya, 2016; Korir & Mwamzandi, 2019). Kwa mujibu wa Ebrahim (2016), Shetani anayemsimamia mkoloni katika tamthilia hii ndiye mnyanyasaji anayemwonea na kumdhalilisha mwanadamu kama inavyojibainisha mwanzoni mwa mchezo huu. Unyanyasaji huu unajibainisha wakati shetani anapomkabili mwanadamu na kuvivunja viungo vya mwili vya mwanadamu mwanzoni mwa mchezo na isitoshe kumlazimisha mwanadamu kuyatamka pasipo hiari yake maneno ambayo mwanadamu hakuyafahamu (ukurasa 4). Dondoo ifuatayo inawasilisha hili:

SHETANI: Sema kwa dhati yako.

BINADAMU: (*anasema kwa dhati*) Gashalazeritwas.

SHETANI: Sasa acha likuumize.

BINADAMU: (*linamuumiza*) Gashalazeritwas.

SHETANI: Likutoe damu.

BINADAMU: (*linamtoa damu*) Gashalazeritwas. (Uk. 4)

Vilevile, maudhui haya yanarudiwa katika onyesho la pili la *Mshetani Wamerudi* (2016) pale kijana 2 anaposema kwamba tatizo lao kuu lilitokana na wao wananchi kufanywa mabwege au vinyago wasiokuwa na mtazamo wowote kimaisha (Mohamed, 2016). Isitoshe, mwanatamthilia Said Mohamed aliyeathiriwa kimaudhui na kazi ya Ebrahim Hussein anaeleza kuwa unyanyasaji katika jamii unajibainisha katika kukiri kwa Kijana 2 kwamba upo ukosefu wa ajira na kazi. Katika maelezo yanayotolewa na Kijana 2 katika kazi ya Mohamed (2016), ajira zilipo ni zile zinazotokana na serikali ambazo hudhibitiwa moja kwa moja na waja wenye umri uliosonga au wazee hivyo kusababisha kuwepo kwa unyanyasaji na kukoseshwa nafasi za ajira kwa vijana. Kwa namna hii, inajibainisha kwamba uonevu na

unyanyasaji ni mojawapo ya maudhui yanayorejelewa katika tamthilia hizi mbili ijapo yanamulikwa kwa njia tofauti katika tamthilia hizi.

2.3.6 Kujittoa Mhanga

Kwingineko, maudhui mengine yanayoashiria kuwepo kwa athari ya uandishi wa mwanatamthilia Ebrahim Hussein kwa utunzi na ubunifu wa mwanatamthilia Said Ahmed Mohamed ni maudhui ya kujitolea mhanga. Kulingana na muktadha wa maudhui husika katika *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016), kujitolea mhanga kuna maana ya mtu kuhatarisha maisha yake kwa minajili ya kupigania haki au masilahi ya jamii yake, nchi yake au masilahi yake hasa kwa njia inayohusisha kujitoa kwa ajili ya wengine (Mahenge, 2022; Faki, 2017; Ponera & Kasiga, 2020). Katika tamthilia ya Hussein (1971) ya *Mashetani*, maudhui haya yanapewa kipaumbele katika mawasiliano baina ya Shetani na binadamu. Vurumai inayowasilisha maudhui haya inamweleza Shetani katika mchezo na binadamu akimvunja binadamu maungo hivyo kumpelekea binadamu kujitoa mhanga na kuamua kukabiliana na adui yake bila uoga wowote. Kulingana na dondoo husika, Binadamu anasikika akimsuta Shetani na kumwambia kwamba kama yeye kweli ni mwanaume kamili basi ajitokeze bila kuogopa kwani Binadamu alikuwa tayari kabisa kujitosa katika makabiliano naye bila kiwewe wala dukuduku lolote (Hussein, 1971).

Mfano ni kama ufuatao:

BINADAMU: Uko wapi? (*Shetani anacheka*)

BINADAMU: Jitokeze. (*Kimya kirefu*). Jitokeze kama wewe mwanamume kweli. Jitokeze. Unaogopa? Ushujaa wako wote unayayuka ukimwona mtu kashika silaha? Tokeza, mwoga mkubwa we. (Uk. 5)

Katika ukurasa wa tano wa tamthilia hii, Hussein (1971) anamuonyesha Binadamu akimkabili Shetani kwa kumueleza kwamba ushujaa wake wote hufifia pindi tu anapomwona binadamu kushika silaha na kumshurutisha ajitokeze kwani alikuwa tayari kukabiliana na mwoga huyo mkubwa (Shetani). Katika *Mashetani Wamerudi*,

Mohamed (2016) anadhihirisha kuathirika na maudhui haya katika tamthilia yake anapoeleza kwa mojawapo ya dondoo ukurasa wa 17 ambapo mhusika Prof anaeleza kuwa amesimama kidete muda wote bila uoga. Asema kwamba haogopi katu kusimama sababu yake kuwa maisha matamu na hivyo basi kulingana naye, kuhofia kifo ni sawa na kuwa mjinga (Mohamed, 2016). Dondoo hii inapomulikwa kwa ukaribu, yadhihirisha bayana kwamba mhusika huyu alikua na ujasiri uliomfanya yeye kujitoa mhanga kwa ajili ya kuitetea jamii yake bila kumwogopa Shetani ambaye ni mkandamizaji wa malengo ya mwanadamu. Kutokana na maudhui haya, inabainika kwamba *Mashetani* (1971) imeiathiri *Mashetani Wamerudi* (2016) kimaudhui hivyo kudhihirisha matumizi ya nadharia ya mwingilianomatini ambapo tamthilia ya awali ya *Mashetani* (1971) inaonekana kuiathiri tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ya hivi karibuni (Njambi, 2023).

2.3.7 Migogoro katika Jamii

Maudhui mengine ambayo hayawezi kusahaulika katika utafiti wa maudhui ya tamthilia hizi mbili za *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016) ni maudhui ya migogoro katika jamii. Katika tamthilia ya *Mashetani*, mgogoro mkuu unaojitokeza unaambatana na kutofautiana kitabaka swala hili likiashiria mgogoro uliokuwepo baina ya mbasi wawili Juma, aliyetoka tabaka la kibwanyenye na Kitaru aliyetoka katika tabaka la unaizi (Hussein, 1971; Massoud, 2013; Massoud, 2018). Wawili hawa walionekana wakiwa katika hali ya kuzozana kuanzia mwanzo wa onyesho la kwanza la tamthilia ya *Mashetani* (1971) (Karata n.w, 2021). Vilevile, ni muhimu kuelewa kwamba mgogoro mkuu ulikuwepo baina ya wahusika Shetani na Binadamu wahusika hawa wakisimamia hali ya sintofahamu au ya kukoseka kwa maelewano baina ya Mwafrika na Mkoloni aliyepeana tu uhuru wa bendera barani Afrika bila kuiachilia Afrika kujiamulia kijamii, kiuchumi na hata kisiasa. Vilevile

katika *Mashetani Wamerudi* (2016) maudhui ya migogoro katika jamii yanajitokeza baina ya Sheta akiwa upande mmoja na kundi la watu likiwa upande mwingine (Nzilu, 2018; Mwangi, 2021; Obondo, 2023). Kutokana na maelezo haya, inajibainisha bayana kwamba Hussein katika *Mashetani* (1971) alikuwa na athari isiyokifani kwa Mohamed hasa katika uandishi wa *Mashetani Wamerudi* (2016).

Maudhui haya ya mgogoro katika jamii yanarejelewa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) kama ifuatavyo:

PROF: Je, unaanza kuukuza mgogoro wetu?

SHETA: Mbona? Nadhani tumeukuza mgogoro wetu tangu zamani.

PROF: Ndiyo, sasa umepanuka mgogoro wetu.

SHETA: Umepanuka vipi mgogoro wetu?

PROF: Ujamii, utamaduni, elimu, uchumi, teknolojia, sayansi, kilimo, vyote hivi vimebanwa. Ndiyo, sisi wenyewe hatuyachangamkii mambo haya. (Uk. 23)

2.3.8 Ulevi na Uasherati

Tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zinaingiliana katika kudhihirisha maudhui ya ulevi na vilevile uasherati katika jamii. Maudhui haya yanayobainika katika tamthilia hizi mbili zilizobuniwa nyakati tofauti yanahusika na maswala ya ulevi na vilevile uasherati katika jamii za *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016). Kaika tamthilia ya *Mashetani* (1971), maudhui ya ulevi yanajitokeza katika sehemu ya tatu ya onyesho la pili katika mkutano baina ya mtu wa pili na wa kwanza pale hotelini (Hussein, 1971; Abdalla, 2018). Wawili hao katika onyesho hilo wanaonyeshwa wakiwa katika shughuli ya ulevi ya “kugubia vinywaji” huku wakiuliza sababu yakutoshughulikiwa barabara licha ya kuwa wahudumu katika hoteli hio walikuwa Waafrika wenzao (Hussein, 1971). Pindi tu baada ya kuingia hotelini humo alimokuwa Juma, wawili hao waliitisha “whisk na beer”, ishara ya kutaka kulewa kama ilivyokuwa desturi katika jamii yao. Ina maana kwamba wawili hao wanasimamia ulevi uliokithiri katika jamii hiyo.

Kwa njia hii, inajibainisha wazi kuwa ubugiaji vileo unaotokana na kukithiri kwa shughuli za ulevi katika jamii ni swala nyeti katika jamii hii kwa kuwa hata Waafrika waliokuwa katika hali ya kukosa uhuru vilevile walipata nafasi ya kujiburudisha kwa vileo katika jamii ya tamthilia hii. Athari ya *Mashetani* (1971) kwa maudhui ya *Mashetani Wamerudi* (2016) inajibainisha baada ya kugundua kwamba Said Ahmed Mohamed anayekubali kuathiriwa na utunzi wa *Mashetani* anayatilia mkazo na kuyarejelea maudhui haya katika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi* aliyoiandika karne ya ishirini na moja. Katika *Mashetani Wamerudi*, maudhui haya yana yanaonekana ukurasa 59 wa onyesho la pili la tamthilia hii ambapo waja wahusika katika shughuli ya kutoa dukuduku zao kuhusu maswala ya jamii yao (Makena, 2018; Nzilu, 2018). Hii ni kama ifuatavyo katika mazungumzo ya Kijana 5:

KIJANA 5: Mimi sina mengi ila kusisitiza upotovu wa maadili nchini mwetu. Si wazee, si hirimu, si vijana si Watoto, sote tumesukumwa na wimbi la utandawazi katika eneo baya la utamaduni...Ulevi na uasherati umekithiri. (Uk. 59)

Kimaususi, Kijana 5 ananukuliwa akieleza kuwa utandawazi wao ulikuwa umekithiri ulevi na vilevile uasherati zikifuatana unyounyo (Mohamed, 2016). Mose n.w, (2021) pamoja na Makena (2018) wanakubaliana na mtazamo huu wanapoeleza kwamba tamthilia hizi za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zilikodolea macho na kulianika wazi swala la ulevi ambalo aghalabu huambatana na uasherati katika jamii kutokana na sehemu hizo za kubugia vileo kuwa vilevile sehemu za starehe na uasherati. Kwa njia hii, inabainika kwamba tamthilia ya *Mashetani* iliathiri kimaudhui uandishi w tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*.

2.4 Nafasi ya Mwanamke katika Jamii

Nafasi ya mwanamke katika jamii vilevile inajitokeza kama mojawapo ya maudhui muhimu mno katika jamii za tamthilia ya *Mashetani* (1971) iliyotangulia utunzi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Mwingiliano baina ya tamthilia ya

Mashetani na *Mashetani Wamerudi* kimaudhui unajitokeza wazi katika nafasi anayojipania mwanamke katika jamii za tamthilia hizi mbili. Mwingiliano katika maudhui haya unaonekana katika shughuli wanazojihusisha mama ya Kitaru katika tamthilia ya *Mashetani* na Msichana katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Wawili hawa wanaangaziwa kuwa shupavu, watetezi, wenye bidii na wenye uwezo sawa au hata zaidi ya wanaume katika maswala ya jamii na familia. Wanawake wanabainika kuwa watu wenye bidii na wenye uwezo wakuzitafutia familia zao sawa na wanaume. Mama ya Kitaru ashona nguo ili kuipa familia yake mapato licha ya mumewe kufanya kazi (Hussein, 1971). Hivyo, anajitokeza kama mwanamke mwenye bidii anayejitolea kikamilifu kuisaidia na kuiani nyumba yake. Msichana aeleza:

MSICHANA: Bora tuendeleo kunyambua mbegu mbovu. Tuendeleo kupambana na maana ya matatizo, ingawa matatizo ya nchi hayana upeo mdogo. (Uk.33).

Mazungumzo baina ya Msichana na Kijana 1 yanazidi kudhihirisha maudhui haya zaidi kama ifuatavyo:

KIJANA 1: Wewe msichana, weledi na ukakamavu huu umeupata wapi? Kisha umesoma shule gani? Chuo kipi? Umepata digrii gani? (Uk. 33)

Kwa mujibu wa dondoo hizi, inabainishwa kwamba Msichana huyu ni mkakamavu anayehusika katika kuitetea jamii yake kutokana na hali mbaya kama vile ya ukoloni iliyokuwa imeigubika jamii yake na hivyo kuhatarisha hatma ya jamii yake. Hivyo basi, mwingiliano unajiwasilisha katika kuimulika nafasi ya mwanamke katika jamii nafasi hio ikisimamiwa na mamaye Kitaru aliyekuwa mkakamavu sana na Msichana katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Ina maana kwamba wanatamthilia Ebrahim Hussein na Said Ahmed Mohamed wanakubaliana kwamba mwanamke anahitaji kujitengenezea nafasi yake katika jamii kama kiumbe mwenye uwezo sawa na wa mwanamume kwani akijikaza hakika ataziafiki ngazi alizozipanda mwanamume.

2.5 Unafiki

Shetani na Sheta ni wahusika wanaotumika kuonyesha mwingiliano kimaudhui baina ya tamthilia ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Unafiki wa Shetani unawalilishwa kupitia kuondoka kwake katika nchi za Afrika na kuwapa waafrika “uhuru” wao kumbe hili lilikuwa wazo la panya kumfunga paka kengele kwani Shetani (mkoloni) hakumpa mwafrika uhuru halisia isipokuwa huo kuwa uhuru wa bendera tu. Huu ni unafiki wa hali ya juu kwa kuwa licha ya kujifanya kumuachia hatma ya uongozi mwafrika na kumpa uhuru, mzungu au mkoloni ameendelea kuzitawala taasisi muhimu nchi za Kiafrika hasa maswala ya kibiashara, elimu, jamii na siasa. Mohamed (2016) anakubaliana na Hussein (1971) kuhusu unafiki huu wa mkoloni ukiwakilishwa na Sheta anayeitisha mshikamano na uwiano baina yake na mwafrika ilhali nia yake ni kumtawala mwafrika na kumnyima uhuru wake. Hii inajibainisha katika dondoo ifuatayo inayoonyesha mazungumzo miongoni mwa Mzee Kitarua na Sheta na Jumai:

SHETA: Ndiyo nyinyi rafiki zangu. (Bado anachekacheka) (Uk. 44)

MZEE KITARUA: Tokea lini shetani kuwa rafiki wa mtu? (Uk. 44)

MZEE JUMAI: Hujawahi kuwa rafiki zamani utakuwa rafiki wetu wa leo? (Uk. 44)

Kulingana na muktadha wa dondoo hii, ina maana kwamba mwafrika akiwakilishwa na Mzee Kitarua na Mzee Jumai waliufahamu unafiki wa Sheta na mbinu zake za kumkandamiza mwafrika uku akijifanya mwenye kujali. Ama kwa yamkini, Sheta ni mbwa mwitu aliyevalia vazi la kondoo. Hii vilevile inajibainisha katika dondoo ifuatayo:

MZEE KITARUA: Bila ya mikataba na sheria zenu za ujanja hamwezi kwenda mbele tena. Kumbuka nyinyi mna maslahi na sisi tuna maslahi yetu pia (Uk. 45).

Kulingana na muktadha wa dondoo hii, ina maana Mwafrika ametambua kwamba Mkoloni ni mnafiki wa kujitakia na kupitia njia za ujanja ilhali alikifanya mwenye kuwajali Waafrika.

2.6 Hitimisho

Sura hii ililenga kubainisha jinsi tamthilia hizo zinafanana au kutofautiana kimaudhui licha ya kuandikwa wakati tofauti.

Tumeweza kudhihirisha umuhimu wa mazingira ya mwandishi katika usawiri wa maudhui katika kazi yake. Tumeonyesha athari ya mazingira katika usawiri wa maudhui. Uchambuzi wa historia za mwandishi Ebrahim Hussein na Said A. Mohamed ulibaini ya kwamba mazingira ulezi, masomo na kazi zao yalichangia pakubwa kujenga maudhui ya tamthilia zao. Kwa mfano, mwandishi Hussein Mohamed wa *Mashetani* alizaliwa katika enzi ya utawala wa wakoloni na vilevile kupata masomo yaliyokuwa na mfumo wa kikoloni. Mazingira haya yalichangia kuwepo kwa maudhui ya ukoloni na vilevile ukoloni mamboleo katika kazi yake.

Matokeo ya utafiti huu yamethibitisha kuwepo kwa athari ya kimaudhui ya tamthilia ya *Mashetani* kwa uandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Hii inabainika kupitia urejeleaji wa maudhui katika tamthilia hizo. Maudhui yanayojitokeza wazi katika tamthilia hizi ni yafuatayo: elimu ya kigeni, ukoloni mkongwe, ukoloni mamboleo, utabaka, unyanyasaji na uonevu, kujitolea mhanga, migogoro ya kijamii, ulevi na uasherati, unafiki, na nafasi ya mwanamke katika jamii. Hivyo basi, matokeo ya utafiti yanatoa ushahidi kuwa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ni uendelezi wa tamthilia ya *Mashetani*.

SURA YA TATU

MFANANO NA TOFAUTI YA USAWIRI WA WAHUSIKA KATIKA TAMTHILIA YA *MASHETANI* (1971) NA *MASHETANI WAMERUDI* (2016)

3.0 Utangulizi wa Utafiti

Sura ya pili ilitilia mkazo swala la athari ya maudhui ya *Mashetani* (1971) kwa maudhui ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Mtafiti katika sura hiyo alijumuisha utangulizi, watunzi na mazingira yao, muhtasari wa tamthilia husika na athari za *Mashetani* (1971) kwa *Mashetani Wamerudi* (2016). Kwingineko, sehemu au sura hii ya tasnifu hii inashughulikia swali la utafiti linalonua kuudadisi usawiri wa wahusika katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) iliyobuniwa na Ebrahim Hussein na kuchunguza iwapo usawiri huo wa wahusika unafanana au kutofautina na wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) iliyoandikwa na mtunzi Said Ahmed Mohamed. Sura hii imenuia kuchunguza usawiri wa kiwahusika katika tamthilia ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*.

Kutokana na athari ya usawiri wa kiwahusika baina ya tamthilia hizi mbili za *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016), nadharia ya mwingilianomatini inajitokeza kama mwongozo halisia wa sura hii ya tasnifu. Kuwepo kwa athari katika usawiri wa wahusika baina ya tamthilia hizi mbili kunabainisha bayana usemi wa Kristeva anayemrejelea Bhaktin kuhusu usemezano anapoeleza kwamba hakuna matini ya kifasihi yoyote inayoweza kuangaliwa kivyake hivyo kuashiria ulazima wa kuchunguza athari za usawiri wa kiwahusika baina ya tamthilia hizi (Childs & Fowler, 2006). Ni sawa na maelezo yanayotolewa na Herman (2011) kwamba kila matini huhusiana na matini nyinginezo zilizoitangulia kwani hakuna matini yoyote inayojisimamia kivyake pasipo athari za matini za apo awali.

Kwa mujibu wa Kanwa (2022), wahusika ni watendaji katika kazi za kifasihi. Hivyo basi, iwapo kuna haja ya kuwaelewa, haina budi kuyamulika matendo yao au mambo wayatendayo pamoja na kuiangazia mitindo tofauti ya lugha iliyotumiwa na watunzi kuwabuni, kuwapa uhai na hata kuwaeleza wahusika wao. Umuhimu wa utafiti wa usawiri wa wahusika katika sehemu hii unafafanuliwa na Muindi (1990) anayeeleza kwamba fikra na mawazo ya waandishi au watunzi kuzihusu jamii hujibainisha bayana kupitia usawiri au nafasi wanaozibunia wahusika tofauti katika jamii zinazojitokeza katika utunzi wao. Mkazo katika sehemu hii unatiliwa uhakiki wa uhusiano baina ya uumbaji na jinsi unavyolingana na uhalisia hasa wa maisha.

Muhimu kabisa ni kwamba sehemu hii inachunguza na kutafiti usawiri uliopo baina ya wahusika wa jamii zilizobuniwa katika *Mashetani* (1971) na Ebrahim Hussein na katika *Mashetani Wamerudi* (2016) na Said Ahmed Mohamed kutokana na mwongozo wa kinadharia wa mwingilianomatini. Kwa ajili hii, usawiri wa wahusika katika tamthilia hizi mbili unachunguzwa kwa njia ya kufananishwa na kutofautishwa nia kuu ikiwa ni kudadisi athari za tamthilia ya *Mashetani* (1971) kwa *Mashetani Wamerudi* (2016) kama inavyoelekezwa na nadharia ya mwingilianomatini. Usawiri wa wahusika unaangaziwa hapa sambamba na ufafanuzi wa Ilomo (2017) kwamba kazi zozote za kifasihi huundwa kupitia kipengele hiki cha wahusika.

3.1 Dhana ya Usawiri

Kwa mujibu wa maelezo yanayotolewa na Awhida (2021), dhana ya usawiri yaangazia mkusanyiko wa tabia aina aina au hali tofauti zibuniwazo na mwandishi wa fasihi. Hali hizo au tabia hizo hulimbikiziwa au kupewa mhusika ili kumpa sifa Fulani au kumfanya aonekane kuwa mtu aliye na tabia mahususi. Vilevile, ni muhimu kung'amua kwamba mtunzi wa kazi ya kifasihi humsawiri mhusika aghalabu kwa ubunifu wa kipekee kama inavyobainika mara kwa mara katika matini ya kazi za

msanii (Awidha, 2021). Kwingineko, Bakizi (2021) anasema kwamba usawiri ni mojawapo wa njia zitumikazo kuzinasa hisia za wasomaji na vilevile wasikilizaji kupitia picha za kimawazo zinazolongwa na wasanii kwa njia ya matumizi tofauti ya lugha.

Ina umuhimu kuchimbua chanzo cha neno ‘sawiri’ ili kuelewa dhana ya usawiri katika kazi za kifasihi. Haji (2018) aeleza kwamba neno ‘sawiri’ yaeleza tendo la kuifanya sura ya kitu kwa njia ya kutumia kalamu au picha au vilevile mashine za kutolea picha. Hivyo basi, Haji (2018) anaeleza kwamba kusawiri maisha kuna maana ya kuibuni kazi ya sanaa iliyo na uwezo wa kusawiri, yaani kazi iliyo na uwezo wa kuiga maisha kupitia njia ya kuizingatia misingi ya kimaisha ya jamii husika. Bakizi (2021) anachangia zaidi kwa kueleza kwamba kusawiri kunaashiria kitendo cha kuchora sura ya jambo, mtu au kitu katika akili. Ali (2015a) akiungwa mkono na Mavisi (2016) wanapeana maelezo zaidi ya tendo la kusawiri au usawiri kwa kueleza kwamba matumizi yake katika fasihi yaashiria kitendo cha kuwalonga, kuwafafanua na kuwaeleza wahusika katika kazi za kifasihi ili kuwawezesha wawezekutenda matendo yao kwa mujibu wa msingi wa maudhui tofauti aliyoyakusudia mtunzi wa kazi ya sanaa au mwandishi wa kazi husika. Mara kwa mara, wahusika hao huenda wakawa wanadamu au viumbe tofauti na binadamu ambavyo huteuliwa na kulimbikiziwa au kubebeshwa majukumu fulani na mwandishi ili kuashiria matendo ya kiubinadamu yaendayo sambamba au sawia na uhalisia wa aushi ya jamii fulani husika (Haji, 2018).

3.2 Dhana ya Wahusika

Wahusika katika tamthilia za *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016) wanapewa kipaumbele katika sehemu hii ya tasnifu hii kwa sababu ya umuhimu wao katika kuzilonga na kuzieleza kazi zote mbili. Ilomo (2017) anaelezea hili katika

msisitizo wake kwamba kipengele hiki cha wahusika hushirikiana na vipengele vinginevyo kuyaendeleza maudhui, hoja na lengo la mwandishi au mtunzi. Ina maana kwamba wahusika ni viumbe vijengwavyo kisanaa na mtunzi au mwandishi wa kazi ya kifasihi umuhimu wao hasa ukiwa kuwasilisha dhamira mbalimbali za kimaisha katika jamii tungwa za kazi ya kifasihi kama vile tamthilia (Awhida, 2021).

Maguo & Alhabib (2021) vilevile wanatoa maelezo ya ziada kuhusu wahusika kwa kueleza kwamba wahusika ni viumbe ambavyo hutumika na mwandishi au mtunzi wa kazi ya kifasihi kupeana ishara fulani. Hii huenda ikawa ishara ya kibinadamu na mara nyingi, wahusika huwa wanadamu. Kwa mujibu wa Ilomo (2017) wahusika hutungwa na mtunzi wa kazi ya kifasihi kupitia mbinu anuwai ziwazowatofautisha hivyo kuziwezesha hadhira zake kuzielewa hulka au sifa za mhusika zinazomtofautisha na wahusika wengineo katika kazi za kifasihi. Kwingineko, Mbatia (2017) anaeleza kwamba wahusika katika kazi za kifasihi ni viumbe anuwai wakiwemo wanadamu ambao mtunzi wa kazi ya kifasihi huwatumia kuwasilisha ujumbe Fulani kwa hadhira yake wakiwemo wasomaji wa kazi zake.

Obondo (2023) anasema kuwa wahusika ni viumbe au vilevile watendaji katika kazi tofauti za fasihi andishi na simulizi. Odhong, Amukowa & Ambayo (2023) waeleza zaidi kwamba wahusika ndio nguzo thabiti zaidi ya maudhui au dhamira ya kuitunga kazi ya kifasihi. Hii ni kutokana na umuhimu wao katika kuzibuni na kuwasilisha dhamira la mwandishi au maudhui fulani anayonuwia kuyafikisha kwa hadhira ya mwandishi (Odhong, Amukowa & Ambayo, 2023). Obondo (2023) anafafanua zaidi dhana ya wahusika kwa kueleza kwamba wahusika aghalabu huwa wanadamu, japo mara nyingine wahusika pia hujitokeza kwa mfano wa vinyago au Wanyama. Iwapo vinyago au Wanyama watumike kama wahusika, ni muhimu kutambua kwamba viumbe hawa mara nyingi huwa na mfanano mkubwa na wanadamu katika

ulimwengu wa kikawaida au ulimwengu hai (Njeru, Kobia & Mugambi, 2022). Kwa mtazamo huu, Njeru, Kobia & Mugambi, (2022) waeleza kwamba wahusika hutumika hasa kuiwakilisha hali halisia ya wanadamu katika jamii. Ni kutokana na sababu hii ndiposa Waithiru, Onyango & Nabea (2020) wanasisitiza kuwa mhakiki wa kazi ya kifasihi anapaswa kuyafahamu majina ya wahusika, maelezo ya mwandishi kuwahusu, mtazamo na maneno ya wahusika wengine kuwahusu, kuchangamana kwao na wahusika wengine na dhima zao ili kuielewa kazi ya kifasihi kwa kina hasa dhamira la mwandishi na maudhui ya kuiandika kazi ya kifasihi.

Ni muhimu kuelewa kwamba kazi yoyote ya fasihi huwa na aina anuwai au tofauti za wahusika. Kwa mujibu wa Njeru, Kobia & Mugambi (2022), kila kazi ya fasihi huwa na mhusika mkuu au wahusika wakuu. Aghalabu, migogoro na matendo yote yenye umuhimu kwa kazi ya fasihi hutokana na wahusika hawa au kuwapata (Njeru, Kobia & Mugambi, 2022). Aghalabu, ndio hutumika na mtunzi wa kazi ya kifasihi kuiwasilisha dhamira kuu ya uandishi kando na kuyafafanua matukio makuu katika kazi ya fasihi. Nyangweso, Nancy & Sangai (2017) wanafafanua kwamba wahusika wakuu ndio mara nyingi hulimbikiziwa changamoto tele na mtunzi wa kazi ya fasihi. Ponera & Kasiga (2020) wafafanua zaidi kwamba mhusika mkuu katika riwaya, hadithi na tamthilia nyingi hupewa sifa ya mhusika wa kimapinduzi anayechangia pakubwa kuongoza hoja ya uanaharakati unaoleta mabadiliko katika jamii yake. Kwa upande mwingine, aina nyingine ya wahusika katika kazi za fasihi ni wahusika wasaidizi. Kwa mujibu wa Njeru, Kobia & Mugambi (2022), aina hii ya wahusika huwasaidia wasomaji kumwelewa zaidi na vilevile kufahamu hulka na mienendo ya mhusika mkuu katika kazi ya fasihi. Vilevile, ipo aina ya mhusika ajulikanaye kama mhusika wa kisaikolojia. Kwa mujibu wa maelezo yanayotolewa na Waithiru, Onyango & Nabea (2020), aghalabu mhusika huyu huwa mhusika mkuu katika kazi

ya fasihi na huumbwa kwa namna ya kumfanya aibue hisia za huruma miongoni mwa hadhira wakiwemo wasomaji. Sampuli nyingine ya wahusika katika kazi za fasihi ni aina ijulikanayo kama wahusika wa kimapinduzi. Kwa mujibu wa Ponera & Kasiga (2020), mhusika wa kimapinduzi ni aina ya mhusika ambaye huwa mwenye ufahamu mkuu wa mazingira ya jamii yake, historia na hali ya kisiasa ya jamii anamokaa. Ni aina ya mhusika ambaye huwa mjasiri sana, mkakamavu sana na asiyeogopa hata kujitoa mhanga kwa niaba ya wanyonge ambao hujitolea kuwatetea (Fuluge, 2023; Ponera & Kasiga, 2020).

Umuhimu wa wahusika katika kuilonga na kuiendeleza simulizi ya kifasihi hauwezitiliwa shaka katika kazi yoyote ya fasihi. Hii ni maana wahusika husimamia sehemu kubwa ya fasihi kwa kuyaendeleza matukio katika simulizi ya fasihi pamoja na kuathiri moja kwa moja simulizi inayosimuliwa (Ilomo, 2017; Mavisi, 2016; Ali, 2015b). Licha ya kuelewa hilo, ni muhimu kusisitiza kwamba wahusika si viumbe hai kwani wao hushabihiana tu na watu kwani wao huishi katika ulimwengu wa utunzi wa kifasihi maana yake ikiwa kwamba wao hulongwa kwa ajili ya watu hivyo kutoa maelezo kuwahusu watu katika jamii (Maguo & Alhabib, 2021). Maelezo haya yanakubaliana na uchambuzi uliofanywa na Mbatia (2017) unaosisitiza kwamba wahusika aghalabu huwa viumbe tungwa, yaani viumbe wasio hai. Kutokana na maelezo yanayotolewa na Ilomo (2017), wahusika si watu halisia bali ni viumbe buniwa vitokanavyo na malengo na mazingira anayotaka kuyawasilisha akilini mwa hadhira yake. Kama asemavyo Muindi (1990), ni baadhi ya matokeo ya ubunifu wa msanii yanayokusudiwa na mtunzi kuwasilisha masuala aliyokusudia msanii. Maelezo anayoyatoa Ilomo (2017) kuhusu wahusika ni kama yafuatayo:

Wahusika ni viumbe wa kubuni wanaotokana na fantasia, mwigo, na kumbukumbu: ni watu bandia wasio na damu na nyama...Mhusika si binadamu lakini anafanana na binadamu. Hana akili, haiba, itikadi wala uwezo wa kutenda bali ana sifa zinazotuwezesha kumtolea maelezo ya kisaikolojia na kiitikadi (Ilomo, 2017, Uk. 39) .

Kwa mujibu wa dondoo inayotangulia hapo juu, ni dhahiri kwamba wahusika si viumbe halisia bali bandia walolongwa kupitia mawazo, malengo na fikra za mtunzi wa kazi ya kifasihi. Kwa sababu wao ni viumbe wa kubuniwa, hivyo basi wanakosa uwezo wa wanadamu au wanyama halisia wanaofananishwa nao kwani uumbaji wao hutokana na dhamira ya mtunzi wa kazi ya kifasihi (Machira, 2015). Mohamed (1995) anaunga mkono ufafanuzi huu kuwahusu wahusika kwa kusisitiza katika dondoo ifuatayo kama ifuatavyo:

Mwandishi awaumbapo wahusika wake, anaumba watu wasioishi katika ulimwengu wetu wa bayana, bali wenye kuishi katika ulimwengu wao wa hadithi au tamthilia ambamo wakitolewa watakuwa hawana maisha (Uk. 72).

Katika ufafanuzi huu anaoutoa Mohamed (1995) katika dondoo hii, ina maana kwamba wahusika si watu wanaoishi katika ulimwengu wa kweli bali huwa picha au taswira inayochorwa na kazi ya kifasihi hivyo kuwa kiini cha vitu vipya katika kazi ya kifasihi vikiwemo mada na dhamira katika fasihi. Hii ina maana kwamba wahusika hushikilia sehemu kuu zaidi katika kuyaendeleza maudhui, lengo au dhamira ya mtunzi wa kazi ya mwandishi zikiwemo maelezo kuhusu mbinu za lugha ambazo aghalabu hujibainisha kupitia usawiri wa wahusika katika kazi ya kifasihi (Ilomo, 2017; Machira, 2015). Kwa minajili ya haya, ni muhimu kusisitiza kwamba wahusika ni kipengele kikuu cha kazi yoyote ya kifasihi.

Katika kazi ya sanaa hasa ya fasihi simulizi na fasihi andishi, wahusika huchukua nafasi kubwa mno. Ali (2015b) anaeleza kwa kina kwamba wahusika hupewa dhana, sifa na sura ya kuelezea mambo ainati ili kuleta dhamira na lengo la mwandishi katika

kazi ya kifasihi. Nafasi ambayo wahusika hupewa katika kazi za fasihi ni ya umuhimu usiokifani na ni sehemu muhimu katika kuangazia maswali kadha wa kadha katika kazi za kifasihi. Kwa mujibu huu, Machira (2015) anaeleza kwamba wahusika ni vigezo muhimu katika kuwasilisha maudhui na mbinu za lugha katika ule utunzi wa mwandishi na humsaidia mwandishi kupitisha ujumbe mahususi na kwa ufundi wa hali ya juu kwa hadhira lengwa.

Katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016), wahusika wametumika vilevile kupitisha ujumbe wa mwandishi kwa kupewa sifa ainati. Ni muhimu kusesitiza kwamba utafiti unahusu kudadisi kama usawiri wa wahusika una mfanano ama utofauti katika uandishi wa tamthilia ya *Mashetani* iliyoandikwa na Ebrahim Hussein na tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* iliyoandikwa baadaye na mtunzi Said Mohamed. Hii ina maana kwamba aidha kuna mfanano katika namna wahusika wamesawiriwa katika *Mashetani* (1971) na katika *Mashetani Wamerudi* (2016) au utofauti katika jinsi waandishi Ebrahim Hussein na Said A. Mohamed wa tamthilia wahusika wamewasawiri wahusika wao kwa mujibu wa mwongozo unaotokana na nadharia ya mwingilianomatini inayoelekeza uchunguzi huu.

3.3 Usawiri wa Wahusika Katika Tamthilia ya Mashetani (1971) Unaofanana na Tamthilia ya Mashetani Wamerudi (2016)

Ni muhimu kufahamu kwa mujibu wa data zilizokusanywa kwa ajili ya utafiti huu kwamba usawiri wa wahusika katika tamthilia teule za *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016) una mfanano mkubwa kuliko tofauti. Hii inaelezewa kutoka katika mtazamo wa mwingilianomatini unaoeleza kwamba matini za nyakati tofauti hutegemeana ili kuweza kuwasilisha maana iliyonuiwa na watunzi wake (Njeru, Kobia na Mogambi, 2022). Herman (2011) akiungwa mkono na Bosibori

(2016) wanafafanua zaidi kwamba mwingilianomatini waeleza jinsi mtunzi wa kazi ya kifasihi anavyoweza athirika kimaudhui, kidhamira au kiwahasika na kazi ya mtunzi wa kazi ya awali. Kwa mujibu wa data zilizokusanywa kuuwezesha utafiti huu, tofauti katika usawiri wa wahusika baina ya tamthilia hizi mbili za *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016) ni za kiwango kidogo mno kwani wahusika aghalabu katika tamthilia hizi teule wanaonekana kusawiriwa kwa mfanano mkubwa zaidi kama inavyofafanuliwa katika sehemu zifuatazo:

3. 3.1 Mfanano Baina ya Usawiri wa Wahusika Shetani na Sheta katika

Tamthilia Teule

Obondo (2023) anaeleza kwamba katika kazi zake tofauti za kifasihi, mtunzi Said Ahmed Mohamed amempa Shetani sifa za kiumbe mharibifu, mwenye kujitakia na asiyewajali wanadamu katika kazi yoyote aliyomtumia kama mhusika. Hii inajibainisha katika usawiri wa mhusika Sheta katika tamthilia ya Said Mohamed ya *Mashetani Wamerudi* inayoonekana kuathiriwa kwa njia kubwa na uandishi wa tamthilia ya *Mashetani* (1971) ya Ebrahim Hussein. Tamthilia ya *Mashetani* (1971) imemsawiri mhusika Shetani kuwa mnyanyasaji, mwenye kiburi kisicho kifani, bepari na mkoloni ambaye raha yake inatokana na kumuona mwafrika akiumia. Massoud (2013) anaonyesha jinsi Hussein amemsawiri Shetani katika *Mashetani* (1971) kwa kuangazia kisa kimoja mwanzoni mwa tamthilia ambapo mhusika huyu anajihusisha katika majibizano na binadamu kina cha malumbano kikiwa ukoloni mkongwe. Massoud (2013) anaendeleza maelezo kwa kusisitiza kusawiriwa kwa mhusika Shetani kama mwenye majigambo asemaye kwamba yeye ni alfa na omega kuashiria ari yake kumnyanyasa binadamu bila kujali. Kwa mfano, Shetani anukuliwa na kusawiriwa na Hussein (1971) kama ifuatavyo:

Mimi ni Shetani
Ninatukuza
Nanabomoa
Mimi ni nguvu
Sijali (Uk 1).

Kwa mujibu wa Massoud (2013) akiungwa mkono na Abdallah (2018), dondoo iliyonukuliwa hapo juu na inayojitokeza katika ukurasa wa kwanza wa tamthilia ya *Mashetani* ya Ebrahim Hussein yaashiria kusawiriwa kwa Shetani kama kiumbe mwenye kujipiga kifua, majivuno, majigambo na asiyemjali binadamu. M'ngaruthi na wenziwe (2015) wanasema kuwa katika tamthilia ya *Mashetani*, mhusika Shetani amesawiriwa kama kiumbe aliyejawa na madaha, mwenye kujionyesha na asiyewajali wengine ama vilevile mbinafsi kupindukia. Ameelezwa kuwa mhusika aliyejawa chuki na mbinafsi kupindukia anayejijali yeye pekee pasipo kuwajali wengine.

Katika tamthilia ilioandikwa na Said Ahmed Mohamed ya *Mashetani Wamerudi* (2016), yabainika kwamba kuna wahusika waliosawiriwa kwa namna moja na mhusika Shetani katika tamthilia ya Ebrahim Hussein ya *Mashetani*. Katika tamthilia ya *Mashetani*, mmojawapo wa wahusika hao aliyetumiwa na mwanatamthilia Ebrahim Hussein kuwasilisha maudhui na sifa fulani ni mhusika aitwaye 'Shetani'. Huyu mhusika (Shetani) katika tamthilia ya *Mashetani*, amesawiriwa kwa namna moja au yenye kufanana na jinsi amesawiriwa katika *Mashetani Wamerudi* (2016) kwa kuvalishwa tabia zinazowiana na za mhusika anayejulikana kama 'Sheta'. Katika *Mashetani* (1971) anatambulika kama Shetani huku katika *Mashetani Wamerudi* (1971), anatambulika kwa jina Sheta, usawiri wao ukijitokeza hasa katika hulka na sifa zao. Katika usawiri huu, mhusika Shetani na Sheta wanatumiwa kueleza ukoloni wa zamani katika tamthilia ya *Mashetani* na ukoloni mamboleo katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Ni muhimu kueleza kwamba wahusika Shetani katika

Mashetani (1971) na vilevile Sheta katika *Mashetani Wamerudi* (2016) wamepewa sifa za ukoloni, ubabe, ukandamizaji, unyanyasaji na uharibifu (Massoud, 2018).

Hii inajibainisha bayana hasa katika tamthilia ya *Mashetani* ya Ebrahim Hussein. Katika tamthilia ya *Mashetani* (1971), mwanatamthilia Ebrahim Hussein (1971) ameonyesha sifa za Shetani waziwazi na kinagaubaga katika onyesho la kwanza iliyoko sehemu ya kwanza kama ifuatavyo:

SHETANI: Unanijua mimi nani?
.....Mimi Shetani
Uwezo wangu hauhifadhiki
Wema wangu hauhisabiki
Ubaya wangu hausemeki
Ninajenga
Ninabomoa
Ninatukuza
Ninadhalilisha nitakavyo (Uk. 1)

Kwa mujibu wa dondoo hii, sifa za mhusika huyu ambaye mienendo na tabia zake zaambatana na hulka ya Sheta katika *Mashetani Wamerudi* (2016) zinambainisha kuwa mharibifu na mwenye uwezo mkubwa wakuleta madhara kwa wale wanaopinga udhalimu na tabia yake ya kuwadhalilisha au kutowaenzi na kuwaheshimu wengine. Ama kwa yamkini, kwa mujibu wa dondoo iliyojitokeza hapa, Shetani anamuwakilisha Mzungu na mfumo wake wa kibepari unaowanyanasa na kuwadhalilisha Waafrika (Massoud, 2018).

Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016), Mwanatamthilia Said Ahmed Mohamed anaendelea kuonyesha sifa za Sheta katika enzi za ukoloni mamboleo kama ifuatavyo katika dondoo ifuatayo:

SHETA: Unajitisha wewe mwenyewe. Kwani kama ulivyosema wewe ni chozi na mimi ni tembo, unadhani mwishowe itakua vipi? (Uk. 20).

Kwa mujibu wa dondoo hii, inajibainisha kwamba jinsi Sheta anavyojieleza kuwa mwenye uwezo usiokifani mfano ukiwa kujilinganisha na tembo ndivyo jinsi Shetani anavyojipiga kifua kwa kueleza uwezo wake kama ilivyonukuliwa katika dondoo iliyojitokeza hapo awali. Mfano ni kujieleza kuwa na uwezo wa kudhalilisha kando na kujipa sifa nzuri za uwezo wa kujenga.

Kutokana na dondoo iliyopo hapo juu ambapo mhusika Sheta yuamdhaliisha binadamu kwa kumwita chozi ilhali yeye mwenyewe yuawajipa sifa za Tembo, inabainika kwamba katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016), mtunzi Said Mohamed amemsawiri Shetani sawa na jinsi Ebrahim Hussein alivyomsawiri mhusika Shetani. Watunzi hawa wawili wanaonekana kummiminia sifa mhusika Shetani katika *Mashetani* (1971) na mhusika Sheta katika *Mashetani Wamerudi* (2016) sifa za kiumbe mwenye madaha, majivuno, majigambo na madharau kwa wengine. Hivyo basi, inabainika kwamba mhusika Shetani katika *Mashetani* (1971) amesawiriwa kwa njia ya mfanano na jinsi mhusika Sheta alivyosawiriwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016).

3.3.2 Mfanano baina ya Wahusika Binadamu, Kijana 1 na Prof katika Tamthilia Teule

Ebrahim Hussein na Said Ahmed Mohamed wamewatumia wahusika Binadamu na Kijana 1 mtawalia kwa tamthilia zao za *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016).

Mazingira walimotumika wahusika hawa yanaweza kutofautiana lakini mwishowe inajibainisha kwamba lengo la waandishi hawa linajitokeza wazi. Katika tamthilia ya

Mashetani (1971), Binadamu amehusika kuliwakilisha eneo la bara Afrika kwa ujumla. Mwandishi Ebrahim Hussein analeta dhana ya Mwafrika kutaka kujitegemea na kupata uhuru wake kutoka kwa minyororo ya wakoloni wanaojulikana kwa sifa ya ubepari na unyanyasaji. Vilevile, Binadamu analeta dhana ya Mwafrika kujielewa na kuamini kwamba mkoloni hayuko kamwe. Inajibainisha katika mazungumzo ya Binadamu na wahusika wengine kwamba Mwafrika anataka kuelewa iwapo mkoloni ametoweka kabisa au iwapo nia yake ni kumchezea shere. Ebrahim Hussein (1971) anatuonyesha hisia ya Binadamu kama inavyojibainisha katika dondoo ifuatayo:

BINADAMU: Amekufa. Nimemuua! Nimemuua! Nimemuua, au alitaka nimuue? (Uk. 8).

Kwa mujibu wa muktadha wa dondoo hii, inabainika kuwa japo Binadamu anafurahia kumuua Shetani (mkoloni), ana dukukudu kwamba huenda hajamuua katu maana yake ikiwa kwamba anaufahamu kuwa uwezo wa Shetani huenda hauwezi kumalizwa ata na kifo.

Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, onyesho la pili, mwanatamthilia Said.A. Mohammed (2016) anamnukuu Kijana 1 akibainisha sifa sawa na za Binadamu kama ifuatavyo:

KIJANA 1: Tufukuzane labda, ingawa hafukuziki... (Uk. 11).

Kijana 1 katika dondoo hii sawa na Binadamu anamzungumzia Sheta anayemsimamia mkoloni. Kwa kusema kwamba angependa kumfukuza mkoloni japo hafukuziki, Kijana 1 sawa na Binadamu anakiri kwamba uwezo wa mkoloni anayewakilishwa na Shetani katika *Mashetani* (1971) au Sheta katika *Mashetani Wamerudi* (2016) haufikiwi na wa mwafrika. Hii ina maana kwamba Kijana 1 na Binadamu wanaosimamia Mwafrika wanakiri bayana kwamba uwezo wa mkoloni umewazidi.

Hali ya kutokuwa na uhakika kwamba ameweza kumuua Shetani inajitokeza katika tamthilia zote teule. Hii inaonyesha kwamba katika tamthilia hizi mbili, Shetani ni kiumbe aliyesawiriwa na kuichukua nafasi ya mkoloni kama inavyowasilishwa katika tamthilia teule. Ina maana kwamba mfanano katika mambo yanayowakereketa wahusika Binadamu na Kijana 1 katika tamthilia za *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016) mtawalia yana mfanano tofauti zikiwa ndogo mno. Kwa mujibu wa Massoud (2018), wahusika hawa wamesawiriwa kwa namna inayonuiwa kuonesha kwamba licha ya kumdhania Shetani anayemwakilisha mkoloni kuwa aliyeliondoka bara la Afrika na kumwacha Mwafrika ajitawale, kweli ni kwamba bado mkoloni (Shetani) yupo na anaendelea kuchochea jinsi maswala yanavyoendeshwa na Waafrika katika nchi za kiafrika licha ya Mwafrika kufikiri alishamfurusha akaenda zake.

Hisia hii inajitokeza katika wahusika Binadamu katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na Kijana 1 katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) vilevile inajitokeza katika mawazo na fikra za mhusika Prof katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Hii inajibainisha kama ifuatavyo: Msicheke ovyo ovyo, mkizani kwamba shetani amemaliza nguvu zake. Yupo hapa hapa. Yumo angani na ardhini. Yuko kule na hapa. Yuko kokote ingawa hayuko kokote. Lakini kwa macho hatumuoni mpaka sasa. Tuko dhaifu na tumeparaganyika (uk. 29).

Kutokana na maelezo haya yanayotolewa na mhusika Prof katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016), uwezo wa Shetani anayemsimamia mkoloni unaonekana kuwa usiowezwa na Waafrika licha ya Waafrika kufikiri walijishindia uhuru na wanajiongoza wenyewe. Massoud (2018) achangia kwa kufafanua dondoo hii kwa kueleza kwamba maelezo yanayotolewa na mhusika Prof yanaashiria ukweli

halisia wa hali anayokubana nayo mwafrika katika karne za baadaye hata baada ya mkoloni kwenda. Dondoo hio yaashiria kujikita kwa ukoloni katika kila kijishemu cha maisha ya Mwafrika. Ingawaje wakoloni wanaoashiriwa na mhusika Shetani hawaonekani wakitawala nchi za barani Afrika moja kwa moja kama ilivyokuwa hapo awali siku za ukoloni, katika karne ya ishirini na moja, wanaonekana kuwa wamebadili mbinu za kulidhibiti bara hili (Massoud, 2018). Kama anavyonakili Muusya (2016), Shetani ambaye anamwashiria mkoloni anazitawala nchi za barani Afrika katika kila uwanja kuanzia katika uwanja wa mawasiliano, madini, kilimo, maswala ya kisiasa na hata katika tamaduni. Dondoo hiyo yaonesha Imani ya mhusika Prof kwamba ingawaje mhusika Sheta au mkoloni ajidai kuwa alishaondoka barani Afrika, bado yupo barani humu tena kwa mpigo sana. Hii inabainika kwa athari za kikoloni zinazoshamiri anga, ardhi na sehemu nyinginezo za nchi za barani Afrika kama inavyoelezwa na mhusika Prof katika dondoo iliyojitokeza hapo juu.

Kutokana na uchambuzi wa dondoo iliyojitokeza hapo juu, inabainika kwamba mhusika Binadamu katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na mhusika Kijana 1 pamoja na mhusika Prof katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) wamesawiriwa kwa namna moja. Wahusika hawa watatu wamesawiriwa kama walio na dukuduku na wasiwasi kuhusu uwezo wa mkoloni kuenda na kuliondokea bara la Afrika kabisa. Mtunzi Said Mohamed katika *Mashetani* anaonesha kwamba hakuna matini inayojisimamia kivyake anapoonesha athari za usawiri wa mhusika Binadamu katika wahusika wakereketwa Kijana 1 na Prof. Athari hii inawiana na maelezo yanayotolewa na Njeru, Kobia na Mogambi (2022) kwamba hakuna matini inayowezasemekana kuwa kazi ya mwandishi mmoja pekee kwani kila matini huwa imeathiriwa na kazi ya mwandishi wa awali. Ni kwa namna hii inabainika katika *Mashetani* (1971) kwamba swala la uhuru bendera linalomkera Binadamu ndilo swala

analogongana na kujaribu kulidhibiti Prof na Kijana 1 katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016).

Dondoo hili ni sehemu inayosimamia majibizano baina ya Kijana 1 na Profesa. Katika kudadisi na kuchanganua mhusika ambaye ni Kijana 1 aliyeko tamthiliani humu, tunapata kuwa anajaribu kuelewa na kuelezwa mambo halisi yalivyo lakini kwa upande mwingine anasumbuka kuelewa bayana maneno anayoambiwa. Mwenendo huu vilevile umeonekana katika hulka za Binadamu. Mbali na hayo, Mohamed (2016) pia anatumia maneno ya Profesa kuonyesha jinsi Kijana 1 anavyodadisiwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* na kuonyesha kiwango chake cha kupambazuka ikilinganishwa na tamthilia ya *Mashetani* (1971). Ni kama ifuatavyo:

PROF: Aaaa, lini vichwa vyetu vitafunguka? Lini tutatoa taka vichwani mwetu? Kwa nini hatutanabahi... (Uk.14)

3.3.3 Kufanana baina ya Juma na Sheta; Profesa na Sheta

Juma ni mhusika katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na ametumika kama mhusika ndani ya mhusika kwani Juma alicheza mhusika wa Shetani katika tamthilia ya *Mashetani* (1971). Lengo la mwandishi ni kuonyesha mwingiliano baina ya wahusika na michezo waliyoicheza kwa mujibu wa nadharia ya mwingilianomatini inayosisitiza kwamba kila matini huathiriwa na kuchochewa kwa njia anuwai na matini zilizoitangulia (Bosibori, 2016; Njeru, Kobia na Mugambi, 2022). Usawiri wa Juma katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) unawiana na usawiri wa mhusika Sheta katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) iliyoandikwa na mwanathamthilia Said Mohammed. Kwa mujibu wa maelezo yanayotolewa na Sarara (1997), wahusika hao wawili wanatumiwa kuonyesha ukoloni mamboleo na ukoloni wa zama au ukoloni mkongwe.

Mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani* (1971) anamlinganisha mhusika Juma na tabaka la washuka ngazi na mabwenyeye wa kitambo waliojikusisha na ukoloni kabla wakati wa mapinduzi kutokeza nchini Tanzania. Kama inavyonukuliwa katika dondoo ifuatayo, Hussein (1971) anaonyesha waziwazi jinsi Juma anavyojitambulisha kama mshuka ngazi na kusisitiza imani yake kwamba watu wa matabaka mbalimabali hawawezi elewana:

JUMA: Mpanda ngazi na mshuka ngazi hawawezi kushikana mikono (Uk. 56).

JUMA: Wewe waishi leo. mimi naishi jana. Tutakuwaje marafiki? Na kila leo yako ni kidato cha kesho yako. Mimi, kila leo yangu ni kidato cha jana zangu... (Uk 56)

Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, mhusika Sheta anaonekana kuathiriwa na imani ya mhusika Juma wa tamthilia ya *Mashetani* (1971). Anaendeleza ile dhana ya kwamba hakuna wakati ambapo mpanda ngazi na mshuka ngazi watasalimiana mikono wala njia zao kukutana kwa njia moja au nyingine. Dhana hii inatilia mkazo uwazi kuwa ukoloni mamboleo bado utaendelea na kuendelea kuchochea kuwepo kwa matabaka ambayo hakuna siku ata moja yatakapoweza onyesha uwiano isipokua kuonezeka tu kwa tofauti za kimapato na njia nyinginezo.

Kwingineko, Mohamed (2016) anatuonyesha kwamba hakuna usawa utakaokua baina ya makundi haya mawili (kundi la unaizi kwa upande mmoja na lile la ubwanyenye upande mwingine) katika kijisehemu cha majibizano baina ya wahusika Profesa na Sheta. Hii inajibainisha wazi kama inavyonukuliwa katika dondoo ifuatayo itokayo katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016): (Uk. 70 na 71)

PROF: Tafadhali kaka. Usinikumbushe ya kale. Hayo tumeyavua na kuyatupa, tunavaa nguo mpya!

SHETA: Kwa nini basi unauleta ukaka? Tokea lini unauleta ukaka? (Uk. 70 & 71)

Vilevile, mwandishi Mohamed (2016) anayatumia majibizano baina ya wawili hawa kuisitiza mgawangiko wa kitabaka na jinsi washuka ngazi hawawezi kuwa na uwiano na wapandangazi. Kutokana na dondoo hio hapo juu, majibizano baina ya Sheta na Prof yanazungumzia tofauti za kitabaka na kukosa Imani kwamba upo uwezo wa matabaka tofauti kuweza kuwiana kwa namna fulani.

Mwingilianomatini unajitokeza wazi kama inavyoonekana katika dondoo hii ambapo athari za Imani ya mhusika Juma katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) inaonekana kuvalishwa mhusika Prof katika *Mashetani Wamerudi* (2016) aneyeendeleza imani ya Juma kwamba hakuna uwezekano wa watu wa matabaka mbalimbali hasa tabaka la walalahoi na lile la walalahai kuelewana, kuwiana na kuungana mkono katika maswala yoyote yale. Herman (2011) anaeleza kwamba kutokana na mtazamo unaoainishwa na nadharia ya mwingilianomatini, matini za awali huathiri uandishi wa matini za hivi majuzi kwa njia tofauti kwani kila matini bila shaka huwa na uhusiano na matini nyinginezo. Kutokana na maelezo haya, mwingiliano baina ya imani na fikra za Juma zinaonekana kujitokeza katika fikra na Mawazo ya Prof anayeonekana vilevile akikerwa na utabaka anaoamini unachochea mgawanyiko usoweza zibika kwa njia yoyote ile.

3.3.4 Watu (Mtu 1, Mtu 2) na Askari kanzu 1 na Askari Kanzu 2

Maudhui ya ukoloni wa kale na wa kisasa yamekita sana katika tamthilia ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Ukoloni huu unahusishwa na bara la Afrika hasa. Waandishi Ebrahim Hussein (1971) na Said Mohamed (2016) wanaonyesha jinsi Waafrika wenyewe kwa wenyewe hawana ule umoja wa kutakiana na kuungana ili wasaidiane katika vita dhidhi ya mashetani (wakoloni). Mwanatamthilia Ebrahim Hussein anatumia mhusika ajulikanaya kama Mtu 2 kuonyesha utepetevu wa waafrika kudhaminiana na kuonyeshana umuhimu baina yao. Vita vya wenyewe kwa wenyewe

havimzui tu mwafrika kujirahisishia kupata uhuru bali vinawapa nguvu wakoloni mamboleo kuendelea kututawala kwa njia zao ainati. Ukilinganisha tamthilia hizi mbili, tamthilia ya *Mashetani* inatuonyesha jinsi mhusika Mtu 1 anaonyesha ghadhabu ya kutothaminiwa na waafrika wenzake katika kupewa huduma hotelini, naye hana budi ila kutoa kufoka kama inavyojidhihirisha katika dondoo ifuatayo:

MTU 1: Hatukusema namna gani. Tumesema hapa mumetuskia bwana. Lakini nyinyi ndio tabia yenu: mnatudharau Waafrika wenzenu. Angekua Mzungu hapa, hata hungethubutu kubishanabishana namna hii (Uk. 41).

Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, mwandishi anatuonyesha kwa kutupa taswira ya ukoloni mambo leo. Anaendelea kutia mkazo kwa kutuonyesha jinsi waafrika walivyo maadui wa wenzao. Mohamed (2016), anatumia wahusika kwa majina ya Askari kanzu 1 na Askari Kanzu 2 kuwahaingaisha wahusika wengine (Profesa, Mzee Jumai na Mzee Kitarua) wanaojaribu kujinyofoa katika tundubai ya ukoloni. Malalamishi anayowawekea waafrika wenzake Mtu 1 yanaoana na kufanana na yale Askari 1 wanayokisiwa kuwafanyia Waafrika wenzao. Wanajaribu kuwaonya dhidhi ya kupanga njama za kutatiza shughuli na mpangilio wa serikali ilhali mbinu hizo za serikali ni mtego wa kutosaidia mwafrika kupata na kuwa na uhuru wake (uk 67).

ASKARI KANZU 1: Nyinyi ni wazee wetu. Hatutaki mtiwe korokoroni. Kwa hivyo leo tumewasamehe. Lakini mara nyingine tukikuta mmekusanyika hapo penye shina la mbuyu, basi mtaona lilichomfanya sangara kuchomwa moto.

MZEE JUMAI: Ndivyo mlivyotumiwa na bosu wenu mje kututishia nyama rero? Katika umri huu sisi hatuna tena la kuogopa. Hasa pale haki zetu zinapokiukwa au zinapovunjwa.

ASKARI KANZU 2: Haya basi tutaona.

Kutokana na dondoo zilizojitokeza hapo awali, yabainika kwamba malalamishi yanayotolewa na Mtu 1 katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) vilevile yanatolewa na Mzee Jumai anapowafokea Askari Kanzu kwa kile anachokisia ni dharau na kuwakosea heshima waafrika wenzio. Wafanyikazi katika hoteli walimoingia Mtu 1

na 2 ndio wanaotumika kuonesha kwamba Waafrika wanachangia hali wanamojipata ndani kwani wao wenyewe wanadharauliana na kumheshimu tu mzungu licha ya changamoto wanazokumbana nazo zinazochochewa na unyanyasaji wa wakoloni. Namna hii imetumika kuashiria kwamba Mwafrika ndiye adui wa maendeleo ya Mwafrika kwani anachangia mno katika kumdhalilisha Mwafrika mwenzake (Massoud, 2018). Vilevile, mwingilianomatini unajitokeza hapa ambapo udhalilishaji wa Waafrika unafanywa katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na Waafrika wengine huku Said Mohamed vilevile akionyesha kwamba Mwafrika bila shaka anadhalilishwa na kuumizwa na Waafrika wenzake katika *Mashetani Wamerudi* (2016).

3.3.5 Binadamu na Vijana (Kijana 1, 2, 3, 4, 5)

Katika hali ya kuonyesha utofauti wa usawiri wa wahusika baina ya tamthilia yake Ebrahim Hussein na Said Mohamed, tunapata kuona athari kiwahusika ya tamthilia ya *Mashetani* kwa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Mwanzoni mwa tamthilia ya *Mashetani* iliyoandikwa na Ebrahim Hussein (1971), mhusika Binadamu anaonyeshwa akicheza sehemu muhimu katika kupitisha ujumbe wa Mwafrika anayetaka kujinyongoa kutokana na minyororo ya wakoloni (mashetani). Mwantamthilia Hussein anamwonyesha Binadamu kuwa kiumbe anayetafuta uhuru wake, kuwa kiumbe mwenye kujisimamia kivyake na kujitafutia ila kuna nyakati ambazo hana uhakika kama amepata kile alichokitaka. Hali hii inajirudia katika wahusika wajulikanao kama Kijana 1, Kijana 2, Kijana 3, Kijana 4 na Kijana 5. Wazo la kukubali kuwa mkoloni ameshakwenda zake halimpi amani na utulivu maanake mawazo yanamsonga na anajipata akijiuliza maswali kama kweli, je ana uhuru wake ama bado hajaupata? Mwandishi Hussein (1971) analeta dhana fulani kupitia mhusika Binadamu kuwa Mwafrika alipopata uhuru, ulikua uhuru bendera ila sio uhuru wa

kujitawala. Anaendelea kueleza kwamba uhuru wa kifikra na kujitegemea kimawazo usiotegemea dhana ya kikoloni ndio jambo alilokosa na halikua linampa amani kamwe (Hussein, 1971). Hussein Mohammed (1971) anatuelekeza na kutuonyesha hali hii ya mwanadamu kama ifuatavyo:

BINADAMU: Lakini...ninasema nini mimi? Haya maneno gani ninayosema! Nikisema namna hii nina itikadi kuwa yule Shetani sikumuua. Ile taabu yote ni bure tu. Kitendo kile kilikuwa stihizai; kilikua kitupu na kisicho na maana. Hilo siwezi kuamini. Haliaminiki. Kuamini hilo ni kuamini kuwa yote aliyosema ni kweli-kuwa mimi...hata kidogo...kivuli, Haiwezekani... (Uk. 10 na, 11).

Dondoo hii inaonyesha kujielewa kwa Mwafrika kunakowasilishwa kupitia mhusika Binadamu anayeoana na ukweli wa mambo yanayomkumba. Ni ishara kwamba mwafrika agundua kuwepo kwa mkoloni katika maswala yake na kuhusika kwa mkoloni kumuamulia hatma yake katika maswala muhimu yanayomkumba aushini. Hali hii ya kupata ufahamu inajitokeza katika *Mashetani Wamerudi* (2016) ambapo wahusika wajulikanao kama Kijana 1, 2, 3, 4 na 5 wanaonekana kufuata mkondo huo wa kimawazo kama inavyonukuliwa katika dondoo zifuatazo.

Vilevile, mwanatamthilia wa *Mashetani Wamerudi* ametumia wahusika tofauti asiawatambulisha kwa majina yao kamili bali kiumri kwa kuwaonesha kuwa wadogo hasa 'Kijana' kama wahusika ili kuleta ufananishi wa usawiri wa wahusika uliojidhihirisha kama ilivyojitokeza apo juu katika tamthilia ya *Mashetani*. Katika nyakati za ukoloni mamboleo, mwandishi Mohamed (2016) anatumia wahusika kuonyesha kujielewa kwao katika safari ya kujitegemea pasi na wazungu. Inaashiria dhahiri shairi kuwa waafrika walikua wameanza kuelimika na kufahamu walipotoka, mahali walipo na maisha ya baadaye wanayotaka kuishi na kuyafurahikia. Hii inajibainisha kama ifuatavyo katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*:

KIJANA 1: Tatizo letu kubwa ni kwamba, sisi wananchi tumefanywa vinyago au mabwege. Hatuna mtazamo wowote sisi. Sisi tuna mtazamo wetu wala si ule wa viongozi wetu wanaopaswa kuendeleza msimamo wetu. Kwa hivyo nchi za Afrika zinasambaratika na kurudi nyuma (Uk. 55-56).

KIJANA 2: Kwanza, nchi yetu haina mwenendo wa kuunda ajira na kazi, na kusema kweli kazi zilizopo ni kazi za serikali ambazo zimedhibitiwa na wazee na watu wenye umri mkubwa. Pili, uchumi wetu umesakama hauendi mbele, ili kurudi nyuma. Tatu, hakuna ubunifu wa kuanzisha viwanda vya kutosha. Tena hakuna mwongozo wala msisitizo wa serikali kuendeleza ajira za watu binafsi. Ikiwa hakuna mipango ya kuendelea ya aina hii au zaidi ya hii, basi ni kama inaelekea usoni mwetu (Uk. 56-57)

Mawazo wanayoyaaisha Kijana 1 na Kijana 2 yanawiana na Mawazo anayoyaaisha mhusika Binadamu kama ilivyonukuliwa katika dondoo iliyotangulia. Jinsi mhusika Binadamu katika tamthilia ya Mashetani (1971) anavyoonekana kuanza kuukubali ukweli wa hali anayokumbana nayo mojawapo ikiwa kushamiri kwa mkoloni katika kila maswala yake kama ilivyoashiriwa katika dondoo iliyotangulia ndivyo jinsi wahusika wenye umri mdogo katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* wanaukumbatia ukweli wa hali zao na kuanza kuuona jinsi ulivyo. Hii imejibainisha katika mfanano wa mazungumzo ya Kijana 1 na Kijana 2 katika dondoo iliyotangulia hapo juu.

Kwa mfano, Kijana 1 kama inavyodhihirika katika dondoo iliyotangulia hapo juu aonekana akijutia ufahamu kwamba wao wananchi katika nchi za barani Afrika wanakumbwa na swala la viongozi wasiopigania haki na masawala ya dhati kwa wananchi isipokuwa kujinua wenyewe na kuyafanya wasiyopaswa hasa kuyafanya. Hio ndio maana yake anapokiri kwamba tatizo lao wananchi ni kwamba wamefanywa vinyago na mabwege na viongozi wao (Mohamed 2016). Mtazamo huu wa Kijana 1 ni bayana kwamba unajitokeza kihalisia katika mtazamo wa Binadamu katika *Mashetani Wamerudi* (1971) kama ilivyonukuliwa katika dondoo iliyotangulia amabapo mhusika huyo alionekana kupata ufahamu na kuukubali ukweli kuhusu

kumilikiwa na kutawaliwa na wakoloni apende asipende. Mtiririko wa athari hii unaonekana kutoka katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na kujibainisha katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) hivyo kuonesha kwamba hakika kila matini huathiriwa na matini tangulizi kama inavyoelezwa katika maelezo ya nadharia ya mwingilianomatini (Bosibori, 2016; Herman, 2011).

Athari hii ya mfanano katika fikra za Binadamu katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na fikra za Kijana 1 katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) vilevile zinajidhihirisha katika dondoo inayotokana na fikra za Kijana 2. Sawa na Kijana 1, Kijana 2 vilevile anaonekana kulalamikia changamoto wanazokumbana nazo zinazotokana kadamnasi na uongozi na utawala mbaya usowapa vijana uwezo sawa na wazee. Kwa mfano, Kijana 2 yualalamikia hali ya ubinafsi serikalini ambapo sera ni za kuwanufaisha wachache walio uongozini bila ya kuwajali walalahoi wasiosauti. Kwa mujibu wa Muusya (2016), hii yaashiria kwamba kabla kuondoka, wakoloni walijitengenezea tabaka linalofanana na wao ili likaweze kuendeleza sera na mifumo yao ya kiuchume pindi tu watakapoliondoka bara la Afrika. Changamoto anazozizungumzia Kijana 2 na Kijana 1 zaashiria hali hizi anazokumbana nazo Mwafrika.

Ni kwa sababu hii inabainika kwamba mwanatamthilia Said Mohamed aliathiriwa kiwahusika na mwanatamthilia Ebrahim Hussein ambaye kazi yake ya kifasihi ya *Mashetani* (1971) ilitangulia. Njia mahususi ya kuelewa athari hii ya kiwahusika ni kwa kuzingatia nadharia iliyoongoza utafiti huu. Hii ni nadharia ya mwingilianomatini iliyopewa upeo na mwandishi Julia Kristeva. Yaeleza ya kwamba matini yoyote ya kifasihi lazma ioneshe uhusiano wa kipekee na matini nyinginezo maana yake ikiwa kwamba kila matini bila shaka huitegemea matini nyingine ili kuzaa maana faafu (Ngesa, Kobia na Matundura, 2015; Njeru, Kobia na Mugambi,

2022). Hii yaeleza sababu ya wahusika katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) kama Kijana 1 na Kijana 2 kuonekana kuiga mitazamo ya hali zao ya kweli kutoka kwa mhusika Binadamu katika *Mashetani* (1971) anayeonekana kuikubali hali yake ya kukosa mamlaka ya kweli yaliyo mikononi mwa mkoloni.

Kutokana na maswala yaliyowasilishwa katika dondoo hizi, inabainika kwamba kila kijana (Kijana 1 na Kijana 2) anasimamia sehemu au swala fulani analotaka lijadiliwe na litiliwe mkazo ili iwe rahisi kujinasua kutokana na aina anuwai za vifungo vinavyosimamia vizuizi anavyokumbana navyo mwafrika. Maswala haya yanaashiria mikwamo na mambo ambayo Mwafrika anapitia yanayotokana na athari za upepo wa ukoloni mamboleo.

Katika sehemu ya tatu onyesho la pili, mwandishi anaeleza mbinu, itikadi na mambo ya ukoloni mamboleo yanayowaathiri waafrika kwa kujua na kutojua na yanayowakosesha wao kujinasua kutokana na minyororo tofauti. Hii inajidhihirisha katika dondoo kadhaa katika *Mashetani Wamerudi* (2016) kama ifuatavyo:

KIJANA 3:...Suala la Kwenda mbele ni suala la kukataa kutegemea mapato kutoka nje kwa njia ya sadaka na ufadhili. Afrika haitakwenda mbele kwa kutegemea sadaka na ufadhili. Tunahitaji kufunga mikanda na kuvumilia ili kujenga maendeleo kwa misingi ya mapato ya hapahapa. Pia tuwe tayari kukataa kuuza rasilimali zetu kwa waambangoma wanaovutia ngozi upande wao. Tusiwe na dhana ya kuwa sisi ndio wahitaji, wenzetu si wahitaji. Ukweli ni kwamba wao ndio wahitaji wakubwa na rasilimali na pia wahitaji wa kuuza bidhaa zao zinazotoka kwenye viwanda. Sasa wakati umewadia wakujitegemea na kuendeleza kuuziana vifaa sisi kwa sisi (Uk. 57-58).

Kwa mujibu wa dondoo hii, inabainika kwamba Kijana 3 ana imani kwamba ni wakati wa Mwafrika kujitegemea na kuzitegemea rasilimali zake kujiendeleza bila kumsujudia mkoloni na kumpigia magoti ili kupewa misaada naye.

KIJANA 4: Mimi nataka kutoa dukuduku lililo moyoni. Kwanza ni elimu tuliyonayo nchini mwetu. Elimu hii tuliirithi kutoka kwa wakoloni. Bila shaka, wakoloni hawakuwa na nia ya kutuelimisha sisi kwa ajili ya kupiga hatua ya kuenda mbele katika nchi na maisha yetu. Elimu tuliyonayo sasa ni elimu inayotandazwa kwa wingi wa nadharia kuliko vitendo vinavyotumiwa kujenga na kutengeneza vifaa na mashine. Ingawa vyyo vikuu vyetu vinafundisha somo la uhandisi bado hatujaunganisha vitendo vinavyoweza kutupa mapato kwa kutumia mashine na vifaa mbalimbali (Uk. 58-59).

Nukuu katika dondoo hii yaonyesha jinsi Kijana 4 ambaye fikra zake zamsimamia mwafrika anavyowaza kuhusu elimu ya kigeni ambayo Waafrika waliirithi kutoka kwa wakoloni. Aeleza kuhusu ukweli alokuja kuuelewa kuhusu elimu hii ya kigeni na ukosefu wa uwezo wa elimu hiyo kumpa mwafrika uwezo wa kuyatenda hasa aliyoyasoma kinadharia.

KIJANA 5: Si wazee, si hirimu, si vijana, si watoto, sote tumesukumwa na wimbi la utandawazi katika eneo baya la utamaduni. Ni kweli kwamba utamaduni wetu una mabaya lakini una mazuri pia. Kusema kweli hakuna utamaduni ambao hauna dosari. Sisi tumeyakumba maovu ya utamaduni za wenzetu. Na yote haya tunayokutana nayo, ndani ya utandawazi ni mambo ambayo yameharibu dunia kwa sababu za pesa. Ulevi na uasherati umekithiri. Dhuluma ndio mchezo wetu. Wizi, ufisadi na unyang'anyi umesambaa. Watu hawamwabudu na hawamwogopi Mungu. Sheria za nchi hazifuatwi wala hazitekelezwi (Uk. 59-60).

Vilevile, mwandishi katika dondoo hii aonyesha jinsi amekuja kuelewa ukweli mtupu kuhusu athari za utamaduni wa wakoloni kuingia katika nchi za kiafrika. Ni kweli anaogundua na kuufafanua kwa kina kupitia maelezo yanayofichua imani yake kwamba utamaduni wa wakoloni uliojikita katika utandawazi umekua na athari mbalimbali kama kusababisha kuwepo kwa unyang'anyi katika nchi za Kiafrika.

3.4 Usawiri wa Wahusika Katika Tamthilia ya *Mashetani* (1971)

Unavyotofautiana na Tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016)

3.4.1 Juma, Kitaru na Mzee Jumai na Kitarui

Juma na Kitaru ni wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mashetani* iliyotungwa na mwandishi Ebrahim Hussein. Mzee Jumai na Kitarui ni wahusika katika tamthilia ya

Mashetani Wamerudi ya mwanatamthilia Said Ahmed Mohamed. Mwandishi Hussein (1971) amewasawiri wahusika Juma na Kitaru kama viumbe ambavyo ni tofauti ili kuleta dhana ya ukoloni na mwafrika mtawalia. Zaidi ya hayo, aliweza kuongeza natija katika kuyaelezea matabaka mbalimbali walimokua wakitokea na pia vilevile kuonyesha historia za mahali walipokuzwa wahusika hawa wakuu. Inajibainisha wazi kuwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, Said Ahmed Mohamed anabuni wahusika wake wakuu kutokana na wahusika wakuu katika *Mashetani*.

Katika tamthilia ya *Mashetani* (1971), wahusika wakuu ni Juma na Kitaru. Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016), majina yanabadilika kwa njia isiyo kubwa huku jina Juma katika *Mashetani* liliongezwa maneno ‘ai’ na kufanywa Jumai katika *Mashetani Wamerudi* (2016) ilhali jina Kitaru katika *Mashetani* likibadilishwa na kufanywa Kitarui. Hii yaonesha wazi kwamba wahusika katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* wanatokana na wahusika waliolongwa na kubuniwa na mwandishi Ebrahim Hussein katika tamthilia yake ya *Mashetani* (1971).

Chanzo cha athari hii kinatokana hasa na dhana ya kinadharia ya mwingilianomatini ulioongoza utafiti huu. Kwa mujibu wa Ngesa, Matundura na Kobia (2015), dhana ya mwingilianomatini yaeleza kuwa hakuna matini yoyote iliyona uwezo wa kujisimamia kivyake kisanii kwani matini yoyote huhusiana na matini nyengine zilizoitangulia. Bosibori (2016) anasema kwamba matini yoyote ile huwa mabadiliko ya mpangilio wa matini zilizotangulia. Hii inatusaidia kuelewa namna mtunzi Said Mohamed anavyowatunga wahusika wake. Ina maana ameathirika na nadharia ya mwingilianomatini ambapo anaonekana kuwafanyia wahusika wa tamthilia iliyotangulia ya *Mashetani* (1971) mabadiliko fulani katika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi*. Kwa namna nyingine, yanabainika kwamba mtunzi Said Mohamed huenda amewatoa wahusika wake kutoka katika matini ya Ebrahim

Hussein ya *Mashetani* (1971) iliyoitangulia hivyo ikiwasilisha ujumbe unaowasilishwa na Herman (2011) kwamba matini zote huwa na uhusiano fulani unaojidhihirisha kwa njia moja au nyingine. Ni kutokana na maelezo haya ya athari za matini moja kwa matini nyinginezo ndiposa inawezaeleweka chaguo la mtunzi Said Mohamed kuwatunga wahusika wake wakuu kama Jumai na Kitarui kutokana na wahusika wa tamthilia ya awali ya *Mashetani* (1971) ya Ebrahim Hussein.

Isitoshe, mwandishi Ebrahim Hussein anatilia mkazo kwamba Juma alikuwa mwanatabaka la mabwanyenye na Kitaru mwanatabaka la unaizi. Inabainika kwamba mwanatamthilia wa karne ya ishirini na moja Said Mohamed (2016), aliathiriwa na uswahiri wa wahusika hao hivyo kuamua kuwaendeleza katika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi* ila akaongeza vigezo tofauti na hivyo basi kubuni wahusika Mzee Jumai na Mzee Kitarui, sura nyingine katika utunzi wake. Kwa njia ya ufundi, Said Ahmed awabuni wahusika hawa wawili, Jumai na Kitarua kutoka kwa wahusika aliowalongo Ebrahim Hussein, Juma na Kitaru waliosimamia sehemu kubwa yakuendeleza maudhui aina aina kama vile ya ukoloni mamboleo, elimu ya kigeni na utabaka. Mwandishi alileta dhana ya kuerevuka na kuelewa masuala yanayowakabili ila kupambauka huku kumekuja baada ya muda fulani. Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016), Said atatudokolea maongezi yao katika dondoo ifuatayo:

MZEE JUMAI: Kusahau itikadi zetu. Kuifuta Mashariki na Magharibi au kupuuza Kaskazini na Kusini. Tushughulike na uwepo wetu ili kukuza chetu badala ya kukuza vya watu wanaozikandamiza nchi zetu na watu wetu.

MZEE KITARUA: Mmmm...Kweli.

MZEE JUMAI: Naam, kweli (Uk. 42).

3.4.2 Mama Kitaru na Msichana

Mama kitaru ni mhusika katika tamthilia ya *Mashetani* ilhali Msichana ni mhusika katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Lengo na madhumuni ya wahusika hawa

katika tamthilia walizochezeshwa ni kuonyesha maudhui ya nafasi ya mwanamke katika jamii. Wahusika hawa wawili wanashabiana ila kwa utofauti wa kimsingi wa kimazingira, kimalengo wanayopaswa kutimiza na vilevile kwa minajili ya tofauti katika nyakati.

Mhusika Mama Kitaru anavyoelezewa na mwanatamthilia Ebrahim Hussein (1971) anaonyesha kuwa mwanamke anaweza fanya kazi za kuleta mapato mbali na kulea watoto na kuwa mke katika familia. Kwa njia hii, mwandishi anamtumia Mamaye Kitaru kuonyesha uhuru wa mwanamke kutomtegemea ama kumwacha mume wake awe ndiye kitega uchumi pekee. Katikia tamthilia hii tunadukuliwa shughuli ambayo Mama Kitaru anendeleza akiwa nyumbani kwa dondoo ifuatayo:

MAMA: Hata angekua ananilaumu, ungesema? Lakini hapana, kusema kweli nimeshikwa na kazi mpaka kopeni mwangu. Nguo za watu chungu nzima, na mkono wenyewe huu huu mmoja. Sijui nimshonee nani nimwache nani. Basi akiniuliza mama yako, ninakutuma hivyo. Usisahau. Akaniuliza mwambie kuwa ‘na kazi. lakini nikipata nafasi tu nitakuja watazama (Uk. 14).

Vilevile, naye Mohammed (2016) alitumia mhusika wa kike ili kuleta maudhui ya nafasi ya mwanamke katika jamii. Utofauti ni kwamba mhusika huyu yumo katika mazingira mengine na anaunda nadharia tofauti kabisa na ya mhusika Mama Kitaru katika *Mashetani* (1971).

Katika harakati za Mwafrika kuanza kujitambua na kujielewa katika enzi za ukoloni mamboleo, mhusika kwa jina la Msichana anajitosa na kuungana na rika lake katika ulingo wa kujikomboa kutokana na mfumo wa sasa wa kikoloni unaohusisha elimu, sayansi, tamaduni, uchumi na utandawazi. Mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* anampa msichana sifa za ukakamavu, weledi, ujasiri na uelevu wa mambo yanayohitaji suluhisho la pamoja (Mohamed, 2016). Mwandishi anaonyesha kuwa mwanamke vilevile ana uwezo kama wa mwanaume wa kuleta nguvu na ushikamano

ili kusuluhisha jambo fulani. Mwandishi pia analeta dhana ya kwamba mtu yoyote hapaswi kuachwa nyuma na kutobaguliwa kwa misingi ya jinsia, kwa maana umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

MSICHANA: Aaaa, tunapaswa tusome katika shule au chuo cha mateso yetu ya dunia. Lakini tuyaache hayo ya kwamba tumesoma shule au chuo gani. Bora tuendeleo kunyambua mbegu mbovu. Tuendeleo kupambana na maana ya matatizo, ingawa matatizo ya nchi hii hayana upeo mdogo.

3.5 Hitimisho

Sura hii ilianguzia usawiri wa wahusika katika tamthilia teule za *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016). Nia hasa ikiwa ni kubaini iwapo wahusika katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) wamesawiriwa kwa namna sawa na jinsi wahusika wamesawiriwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Sura hii imeanguzia iwapo wahusika wamesawiriwa kwa njia tofauti katika tamthilia za *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016) au iwapo wamesawiriwa kwa njia ya kufanana.

Mtafiti ameonyesha kwamba mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) ameathiriwa pakubwa sana na mwandishi wa tamthilia tangulizi ya *Mashetani* (1971) ambaye ni Ebrahim Hussein. Nadharia ya mwingilianomatini imetumika katika sura hii kumulika sababu za mwanatamthilia Said Mohamed kuonesha kuathiriwa kiwahusika na kazi ya mwanatamthilia Ebrahim Hussein aliyeandika tamthilia ya *Mashetani* (1971). Imeonesha hasa kwamba katika kuwaumba na kuwahaisa wahusika wake katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016), mwanatamthilia Said Mohamed ameathirika has ana kazi ya Hussein ya *Mashetani* (1971) iliyompa msingi wa kuwabuni wahusika wake. Hii yaonesha makubaliano kwamba hakuna matini iliyona uwezo wa kujisimamia kipekee kwani kila matini huchangiwa na matini za awali.

Katika kufananisha na kutofautisha jinsi wahusika tofauti walivyosawiriwa na waandishi wa tamthilia teule, mtafiti ameonyesha kwamba wahusika katika tamthilia hizi wamesawiriwa kwa mfanano mkubwa tofauti zikiwa haba mno. Hii ni Pamoja na kupata kwamba wahusika Shetani na Sheta, Binadamu na Kijana 1 na vilevile Prof katika tamthilia hizi teule wamesawiriwa kwa njia ya mfanano. Vilevile, wahusika Juma na Sheta, Profesa na Sheta waonekana kusawiriwa kwa njia ya mfanano. Tofauti katika usawiri wa wahusika zipo japo kwa njia ndogo mno. Hii yabainisha kwamba matini huathiriana huku tamthilia ya Mashetani (1971) ikionekana kuathiri tamthilia ya Mashetani Wamerudi (2016) kiwahasika.

SURA YA NNE

ATHARI ZA TAMTHILIA YA *MASHETANI* (1971) KWA *MASHETANI*

WAMERUDI (2016) KIMTINDO

4.0 Utangulizi wa Utafiti

Sura ya tatu ya utafiti huu ilichunguza athari ya usawiri wa wahusika katika tamthilia ya *Mashetani* (1972) na *Mashetani Wamerudi* (2016). Ilitilia mkazo hasa maswala mbalimbali kama vile kuchanganua dhana ya usawiri, dhana ya wahusika na usawiri wa wahusika kama unavyofanana na kutofautiana katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016) kwa mujibu wa nadharia ya mwingiliano matini uloinishwa na kufasiriwa na Kristeva (1968). Kwa upande mwingine, ni muhimu kuwa na ufahamu kwamba sehemu hii ya tasnifu inatilia mkazo swali la utafiti la tatu linalochunguza iwapo huenda mtindo katika tamthilia ya Ebrahim Hussein ya *Mashetani* (1971) una athari katika mtindo anaoutumia mtunzi Said A. Mohammed katika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Ina maana ya kwamba sehemu hii ya utafiti inachunguza athari za kimtindo katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016). Hivyo basi, utafiti huu unaangazia maswala ya kimtindo kama vile matumizi ya jazanda yanavyojitokeza katika kazi hizi mbili za *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016).

Kabla ya kuzama katika kuainisha athari ya mtindo katika kazi hizi, ni muhimu kujibu swali, nini maana ya dhana ya mtindo katika kazi za kifasihi? Akieleza kwamba mtindo katika kazi ya kitamthilia hueleza mbinu za lugha anazoitumia mwandishi katika kuwasilisha hoja zake, Okwena (2018) anasema kuwa mtindo ni hulka katika utungaji inayotumika kumpambanua mtunzi mmoja na mwingine. Hii ina maana kwamba mtindo katika tamthilia moja unawezaathiri aidha kupitia kuigizwa au

kuhusishwa kwa njia ya ubunifu zaidi katika kazi ya kitamthilia ya mtunzi mwingine. Sehemu hii ya utafiti imebeba vijishehemu anuwai kama uchambuzi wa dhana ya wahusika, na uchambuzi wa kina wa mbinu tofauti za lugha zinazojitokeza katika tamthilia hizi mbili za *Mashetani* (1972) na *Mashetani Wamerudi* (2016). Ama kwa yamkini, jambo hususan katika sehemu hii ni jinsi mwandishi Ebrahim Hussein wa *Mashetani* (1972) anavyoathiri uandhishi wa *Mashetani Wamerudi* (2016) uliofanywa na mtunzi Said Ahmed Mohamed.

Kama zinavyofuata sehemu ya pili na ya tatu ya kazi hii, ni muhimu kusesitiza kwamba utafiti katika sehemu hii ya nne utafuata nyayo ya utafiti katika sehemu za awali kwa kufuata vilevile nadharia ya mwingiliano matini kama ilivyoasisiwa na Julia Kristeva (1969) kutokana na nadharia ya Mikhail Bakhtin (1968). Agiso (2017) akimnukuu Bhaktin (1968) aeleza kwamba kazi yoyote ya kisanaa haipaswi kuchukuliwa kuwa kazi mahususi au kazi kamili ya mtunzi wake bali yapaswa kueleweka kuwa aina ya usemezano uendeleo baina ya msanii na wasanii wengine waliomtangulia. Ni kwa kufuatia huu mtazamo Kristeva (1969) anaeleza kwamba matini yoyote ni kazi inayobuniwa kutokana na matini zilizopo. Hii ina maana kwamba matini haibuniwi kutokana na fikra au mawazo ya watunzi wake pekee bali kutokana na mkusanyiko wa matini anuwai za kitamaduni (Kilingo, 2019; Agiso, 2017). Kilingo (2019) anamnukuu Kristeva (1969) na kusema kuwa matini yoyote ile ya Kiswahili haiwezi kujisimamia kivyake pasipo uhusiano na matini nyinginezo kwani kila matini au usanii ni upangaji mpya wa mawazo ya hapo awali ya watunzi wengine. Nadharia ya mwingiliano matini yaongoza utafiti katika sehemu hii ya tatu ya kazi hii ili kuwezesha uchanganuzi wa athari za kimtindo katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016).

4.1 Dhana ya Mtindo

Kwa kuwa uzito wa sura hii unalipiga darubini swala la athari za kimtindo katika tamthilia ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*, ina maana kuchanganua dhana hii ya mtindo kiundani ili kuwasaidia wasomaji waweze kuelewa kiundani maana hasa ya mtindo kama inavyotumika katika kazi hii ya kifasihi. Uchanganuzi wa athari za *Mashetani* kwa *Mashetani Wamerudi* katika sehemu hii unaambatana na matakwa ya nadharia ya mwingiliano matini unaosisitiza kwamba matini yoyote bila shaka haiwezi kujisimamia kivyake bali lazma itokane na athari za matini zilizotangulia (Kristeva, 1969; Agiso, 2017; Kilingo, 2019).

Ni muhimu kuisitiza kwamba mtindo ni sehemu ya fasihi inayotumika sio tu katika tamthilia bali hata katika kazi nyinginezo za kifasihi kama vile katika riwaya. Wamitila (2008) akiungwa mkono na usemi wa Silavwe (2016) anasema kwamba mtindo ni mojawapo ya elementi muhimu zaidi katika kazi yoyote ile ya kifasihi. Kwingineko, Silavwe (2016) aendelea kunakili kwamba mchanganuzi yeyote wa kazi ya kifasihi au matini ya Kiswahili alazimika kudadisi maswala tofauti katika kazi husika ili kuweza kubainisha na kueleza sifa za kimtindo za kazi husika. Kwa mujibu wa maelezo yanayotolewa na Nyutu (2016) akiungwa mkono na Silavwe (2016) anasema kuwa mambo ama maswala hayo tofauti ni kama vile mipangilio na miundo ya sentensi, uteuzi wa misamiati ambayo mtunzi anayoamua kuyatumia katika kazi yake ya kifasihi, uteuzi na matumizi ya tamathali kama vile jazanda na usemi, motifu pamoja na dhamira zikaririwazo katika kazi tofauti za waandishi wa fasihi, mbinu za usimulizi, sifa za uakifishaji hasa zikiukazo uakifishaji wa kikawaida na usimulizi, na usawiri wa wahusika ambao umedadisiwa katika sehemu ya pili ya kazi hii ya kifasihi. Wamitila (2008) anaeleza ya kwamba mtindo katika fasihi uhusu mambo anuwai bila kuainisha yote isipokuwa ya kimsingi kabisa, japo wachunguzi wengine

kama vile Nyutu (2016) na Silavwe (2016) wanaendeleza mada hio kwa kutoa maelezo zaidi kuhusu baadhi ya mambo hayo. Maguo na Alhabib (2021) wazidi kueleza maana ya mtindo na sifa zake kwa kueleza kwamba sifa nyinginezo za mtindo katika kazi ya kifasihi zinajibainisha kutokana na namna mtunzi anavyoteua visa na matukio tofauti katika kazi yake ya kifasihi, mwingiliano baina ya tanzu na matumizi ya michoro na picha pamoja na mwingiliano matini ambazo hutumika katika kufafanua maelezo anayoyotoa mwandishi katika tamthilia, riwaya au kazi yoyote ile ya kifasihi.

Kwingineko, kwa mujibu wa maelezo yanayotolewa na Okwena (2018), mtindo katika fasihi ni mojawapo ya dhana ambayo hutumika kurejelea jinsi ya kujieleza katika kazi za kifasihi. Ni namna anayoitumia mtunzi wa kazi ya kifasihi kujieleza katika utunzi wake. Katika ufafanuzi wake wa dhana hii ya mtindo, Okwena (2018) anasema kwamba mtindo hususan unajitokeza kama tabia katika utunzi itumikayo hasa kumpambanua mtunzi mmoja na mwingine. Kutokana na maelezo yanayotolewa na Massoud (2018) akiungwa mkono na Okwena (2018), mtindo humsimamia mtu mwenyewe maana yake ikiwa kwamba unahusisha namna mtu anayotumia kujieleza kupitia matumizi ya lugha, yaani maana yake ikiwa namna au jinsi ya mtu ya kuwasilisha ujumbe anaokisia kuuwasilisha kwa hadhira husika au wasomaji wa kazi yake ya kifasihi. Hii ina maana kwamba mtindo ni namna mtunzi anavyowasilisha ujumbe wake kwa hadhira husika. Umuhimu wa mtindo katika kazi yoyote ya kifasihi unafafanuliwa na Okwena (2018) anayesisitiza kwamba nadharia ya kimtindo katika kazi za kifasihi huzingatia kufafanua kwamba kazi yoyote ya kifasihi haiwezi kuwasilisha maelezo kadamnasi pasipo matumizi ya lugha. Hii yamaanisha kwamba namna mtunzi anavyotumia lugha katika kazi ya kifasihi ndiyo humpa uwezo

kuwasilisha ujumbe anaonua kuuwasilisha kwa wasomaji ambao ni miongoni mwa hadhira zake lengwa.

Kwingineko, akichangia katika kueleza maana ya mtindo, Fadhili (2014) anatoa maelezo yanayochanganua swala hili kwa mapana na marefu au kwa undani zaidi. Kwa mfano, anaeleza kwamba ili mchanganuzi wa kazi ya kifasihi au matini kuweza kubainisha sifa za kimtindo katika kazi za kifasihi, ni lazma aweze kutathmini maswala anuwai katika kazi husika zikiwemo uteuzi wa jazanda na matumizi ya tamathali za semi, uteuzi wa misamiati ya mtunzi, usawiri wa wahusika, dhamira na motifu zikaririwazo katika kazi za kiutunzi na sifa za kuakifisha zielekeazo kukiuka njia za kikawaida za uakifishaji (Fadhili, 2014). Kupitia maelezo haya, Fadhili (2014) aoana na kukubaliana na mtazamo wa Maguo na Alhabib (2021) kwamba mtindo vilevile uhusiana na matumizi ya michoro na picha pamoja na mwingiliano matini ambazo hutumika katika kufafanua maelezo anayoyotoa mwandishi katika tamthilia, riwaya au kazi yoyote ile ya kifasihi.

Kwingineko, ni muhimu kuelewa kwamba kila mtunzi huwa na mtindo wake kwa mara nyingine mtindo wa mtunzi mmoja ukitofautiana na mtindo wa mtunzi au watunzi wengine (Okwena, 2018). Utofauti hujitokeza hasa katika uteuzi na matumizi ya vipengele tofauti vya lugha au kimtindo (Fadhili, 2014). Fadhili (2018) anaendelea kutoa maelezo kwamba hata katika harakati ambazo waandishi wawili waliokulia sehemu moja au mazingira sawa yenye miktadha sawa, jambo ambalo hupelekea kujitokeza kwa utofauti katika kazi zao ni namna waandishi husika wanavyotofautiana katika matumizi ya vipengele tofauti vya mtindo au lugha. Fadhili (2014) anasema kuwa ni muhimu kuelewa kwamba si rahisi kushughulikia au kupeana uzito kwa vipengele vyote vya mtindo mwongozo huu ukiashiria uamuzi wa

mchanganuzi kushirikisha vipengele kadhaa vya mtindo katika tamthilia za *Mashetani* (1972) na *Mashetani Wamerudi* (2016).

Ni bayana kutokana na udadisi uliofanywa hapo awali na wachanganuzi wengine wa kazi za kifasihi kuhusu mtindo katika *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* kwamba kazi hizi mbili zinafanana kwa njia kubwa katika namna zinavyotumia vipengele tofauti vya kimtindo hasa vinavyohusiana na matumizi ya lugha. Massoud (2018) anayelinganisha matumizi ya mtindo katika *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2006) aleleza kwamba kazi hizi mbili zinashirikiana katika matumizi ya vipengele vya kimtindo hasa vya kimatumizi ya lugha kama vile katika uteuzi wa misamiati, matumizi ya tamathali za semi, mandhari ya fasihi simulizi, masimulizi, majigambo, mtindo wa nyimbo, mtindo wa tamthilia za majaribio, matumizi ya nafsi zote na dayalojia. Massoud (2018) anaeleza kwamba kazi hizi mbili za kifasihi zashabihiana katika matumizi ya mtindo wa nyimbo, mashairi, na mtindo wa matumizi ya ndoto. Isitoshe, tamthilia ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zinaingiliana katika matumizi ya mtindo wa lugha kama vile taswira, misemo, methali, ishara, nahau, jazanda na tamathali za semi utofauti katika kimtindo ukijitokeza kwa umbali hii ikiwa tu katika matumizi ya mtindo wa mchezo ndani ya mchezo unaotumika katika *Mashetani* (1971) pekee bila kutumika katika *Mashetani Wamerudi* (2016). Kwingineko, tofauti katika mtindo pia zajitokeza hasa katika namna ya jinsi kazi hizi zinavyotumia mtindo wa taswira huku uchunguzi ukionyesha bayana kwamba taswira ya punda, simba, kuku, jogoo na batamzinga yajitokeza tu katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) bila kubainika katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) (Nzilu, 2018; Massoud, 2018). Vipengele hivi vya kimtindo katika tamthilia hizi mbili vinadadisiwa kama ifuatavyo katika sehemu ifuatayo.

4.2 Vipengele Vya Mtindo Katika Mashetani (1971)

4.2.1 Matumizi ya Jazanda katika *Mashetani* (1971)

Kwa mujibu wa Massoud (2018) na Ngesa na wenzake (2015), jazanda ina maana ya utumizi wa maneno ya kimapumbo ambapo neno hutumika kuwasilisha maana ya jambo jingine. Kwa mujibu wa Ngesa na wenzake (2015), data zilizokusanywa kutoka tamthilia ya *Mashetani* (1971) zinaonyesha kwamba mtindo wa kijazanda umetumika mara kadha wa kadha katika tamthilia hiyo ya Ebrahim Hussein. Ufafanuzi ufuatao wadhihirisha bayana matumizi ya mtindo wa kijazanda katika tamthilia ya *Mashetani*.

4.2.1.1 Jazanda ya Neno ‘Ukweli’

Kwa mujibu wa Massoud (2018) akiungwa mkono na Ngesa, Matundura na Kobia (2015), inabainika kwamba neno ‘ukweli’ limetumika kijazanda katika tamthilia hii kudhihirisha kwamba ukweli ni silaha ya kipekee iliyo na uwezo wa kuimaliza migogoro tofauti katika jamii huku jazanda hii ikitumika kama ifuatavyo katika dondoo ifuatayo:

Ukweli?

Ukweli ndio upi?

Ukweli ni huu.... Kuna lile lipaswalo kufanywa, na yule apasayekulifanya.

Mimi-mimi au yeye-mimi anayetaka kulitekeleza azimio hili?

Kamasiujuwi ukweli wa swali hili basi siujui ukweli wa kitendo changu, maisha yangu wala azimi langu (Uk 12).

4.2.1.2 Jazanda ya Kisu

Vilevile, neno hili ‘kisu’ limetumika kijazanda kuashiria jitihada walizodhihirisha Waafrika katika vita vyao vya kuutafuta uhuru wao kutoka katika mikono ya wakoloni walokuwa wamezitibithi nchi zao. Kwa mujibu wa Massoud (2018), neno

‘kisu’ linatumika kuonyesha ishara kadamnasi ya uwezo uliowapa Waafrika nguvu za kuwadhibiti na kuwabandua wakoloni kutoka katika uongozi wa bara Afrika. Hii inajibainisha kama ifuatavyo katika dondoo ifuatayo:

SHETANI: Wakati wangu wa kufa umefika. (Shetani na Binadamu watazamana. Wote watabasamu. Shetani anampa binadamu kisu. Wanashikana...) (Uk. 8)

4.2.1.3 Jazanda ya Neno “Chewa”

Ni muhimu kubaini kwamba neno chewa vilevile limetumika kijazanda kuwasilisha dhana ya uwezo wa wakoloni katika kujipenda na kuhakikisha wameyakidhi maslahi yao pasipo uwezo wa Waafrika wanyonge kujisimamia na kujitetea. Hii ni sababu Chewa kama alivyotumika katika tamthilia hii asimamia kiumbe mkuu aishiye baharini na aliye na uwezo wa kuwameza viumbe wengineo wote baharini uwezo wake ukiwepo na nguvu za kubaini hata mwendo wa meli majini kwa kuuvuta mkondo wa maji na kukilazimu chombo hicho kuelekea asiko taka wala kutarajia nahodha wake (Massoud, 2018). Katika tamthilia hii ya *Mashetani*, mwandishi Hussein anatumia ndoto aliokuwa nayo Kitaru kuisimulia hadithi ya Chewa kama ifuatavyo:

KITARU: Hadithi ya chewa. Mbali sana ukivuka bahari saba, kuna chewa mkubwa. Chewa huyu akivuta pumzi maji yote yanakupwa, maji yote yanaingia kinywani mwake. Anaweza kutoka huko aliko, kuivuta na kuimeza mashua yoyote anayoitaka. Mashua inavutwa tu na mkondo wa maji, ikitaka isitake. Na huyu chewa siyo chewa bali Shetani” (uk. 28).

Kutokana na dondoo hii, inabainika kwamba neno Chewa limetumiwa kimajazi na Ebrahim Hussein kuwasilisha dhana ya ulafi uliomjaa mkoloni hususan katika ari yake kuuendeleza ukoloni mamboleo. Kwa mujibu wa ufafanuzi unaotolewa na Massoud (2018), Chewa azisimamia nchi za kikoloni zilizo na uwezo wa kuziamulia nchi changa hasa zilizoko barani Afrika kuhusu njia wanazostahili kufuata ili

kuimarika kiuchumi huku nchi hizo changa zikikosa nguvu za kujiamulia njia zinazopaswa kufuata kwa hiari yazo. Uwezo mkuu wa kiumbe Chewa unakinzana na kukosa uwezo kwa mashua ambayo yaashiria bara Afrika lililojawa nchi zenye wanyonge ambao mambo yao yote huamuliwa na nchi komavu na zenye uwezo mkuu za ughaibuni hasa zilizoko Uropa.

4.2.1.4 Jazanda ya Maneno “waltz” na “Gashalazeritwas”

Katika tamthilia ya *Mashetani*, maneno haya mawili ‘waltz’ na ‘Gashalazeritwas’ yametumika kijazanda ili kuashiria aina ya uhusiano uliopo baina ya nchi za bara Afrika na wakoloni walizozitawala nchi hizi hapo awali kabla nchi za barani humu kujitafutia na kuupigania uhuru wao. Inabainika kuwa ‘waltz’ ni aina ya ngoma yenye asili ya nchi za ukoloni (Hussein, 1971). Kwingineko, akipiga msasa na kuangazia maana ya kijazanda ya matumizi ya neno ‘waltz’, Massoud (2018) anasema kuwa uchezaji wa ngoma kama hii ya ‘waltz’ unaashiria kwamba uhuru uliopatikana na nchi anuwai za bara Afrika ni wa kibendera tu kwani nchi hizi hazijaupata uhuru halisia wa kujisimamia pasipo ukoloni mamboleo. Neno ‘waltz’ linaashiria kijazanda kwamba bara Afrika halijapata uhuru halisia kwani lilipokea na kukubali kutekeleza mifumo totauti ya utawala wa wakoloni pasipo bidii ya kuihakiki mifumo hio ya waliokuwa watawala wazo enzi za ukoloni. Kuchezwa kwa ngoma hii ya ‘waltz’ inayotambulisha kuwepo kwa utamaduni wa Shetani barani Afrika hasa katika shughuli za kusherehekea uhuru linaashiria kwamba nchi za bara Afrika hazikuupata uhuru halisia isipokuwa kuusherehekea tu uhuru wa kibendera (Massoud, 2018).

Kwingineko, neno “Gashalazeritwas” vilevile limetumika kijazanda kuashiria athari za nchi hizo za kigeni katika mifumo ya kielimu barani humu Afrika. Linaashiria jinsi matumizi ya lugha barani humu na hasa katika mifumo ya elimu barani humu yalivyoathiriwa na lugha za kikoloni kama vile ya Kijerumani. Katika uchambuzi wa

asilia ya neno hili, Massoud (2018) anasema kwamba neno “Gashalazeritwas” linajibaini hasa katika nchi zilizotawaliwa na Wajerumani hapo awali kama Tanzania asilia yake hasa ikiwa lugha ya Kijerumani. Hivyo Basi, yabainika kwamba uteuzi wa maneno haya kijazanda na mwandishi Hussein (1971) katika tamthilia hii ulikusudiwa kuashiria kwamba jamii za nchi za barani Afrika zinaamini kuwa zilijishindia uhuru ilhali huo si ukweli kwani licha ya wakoloni kwenda, bado jamii barani humu zinaendeleza sera, mipango na matakwa ya nchi za kikoloni na kuelekezwa hasa na nchi hizo za kibeberu katika mifumo ya kiuchumi, kielimu na maswala yoyote yanayohusisha maendeleo. Hii imethibitishwa katika tamthilia ya *Mashetani* kama inavyowasilishwa katika dondoo ifuatayo:

SHETANI: Hebu basi nikunong’oneze maana siri yenyewe ni kwa lugha ya kishetani. Liseme neno nililokufunza Binaadamu: Gashalazeritwas

SHETANI: Sema nikusikie

BINAADAMU: Gashalazeritwas

SHETANI: Sema kwa dhati yako

BINAADAMU: (Anasema kwa dhati) Gashalazeritwas

SHETANI: Sasa acha likuumize

BINAADAMU:(Linamuumiza) Gashalazeritwas

SHETANI: Sema likutoe damu

BINAADAMU: Linamtoa damu Gashalazeritwas (uk 3 na 4)

Kwa mjibu wa dondoo hii, inabainika wazi kwamba maisha ya kila siku ya jamii zilizoko katika nchi barani Afrika zinaendelea kuathirika na dhana ya ukoloni mamboleo licha ya nchi hizo kufikiria zilipata ukoloni katika sehemu ya pili ya karne ya ishirini.

4.2.1.5 Jazanda ya Neno “Mheshimiwa”

Katika tamthilia hii, neno ‘Bwana’ vilevile limetumika kijazanda kaushiria maana fulani mahususi. Salem (2013) anasema kwamba matumizi ya neno hili kijazanda yalijitokeza hasa wakati wa ukoloni nia hasa ikiwa ni kuashiria ‘ubwana’ wa mzungu dhidi ya mtu mweusi aliyechukuliwa kutokuwa hadhi sawa na mzungu hasa

kufahamika kuwa ‘mtwana.’Kwingineko, Sarara (1997) aeleza kwamba pindi tu baada ya nchi za barani Afrika kupata uhuru kutoka kwa wakoloni, matumizi ya neno ‘mheshimiwa’ yalichukua mkondo tofauti nia hasa ikiwa kubainisha matumaini yaliyokadiriwa baada ya kufukuzwa kwa mkoloni kutoka nchi za barani humu. Massoud (2018) anaongezea uchanganuzi wa msamiati huu kwa kueleza kwamba baada ya mkoloni kuondoka bara Afrika, neno ‘mheshimiwa’lilipata maana ya kutumika na kada tofauti kuwatofautisha kwa njia ya kuwatambulisha watu wenye upeo wa juu katika jamii hasa waliokuwa katika tabaka lililotawala.

Salem (2013) anaendelea kuchanganua maana ya msamiati huu ‘mheshimiwa’ kwa kueleza kwamba neno hili lilibeba kasumba hasa miongoni mwa viongozi wa barani humu waliojiona kuwa wa maana kuwaliko wanajamii wengine na hivyo kutaka ikawe desturi kwao kutambulishwa kama waheshimiwa. Sababu hasa ya viongozi wa barani Afrika kutaka kutambulishwa kama ‘waheshimiwa’ ni maana wao walijiona kuwa chanzo cha uhuru wan chi zao. Ama kwa Yakini, waliamini ndio waliousababisha na kuupigania uhuru wa nchi zao hivyo kustahili kutambulishwa kama ‘waheshimiwa (Salem, 2013; Sarara, 1997).

Kasumba hii inajitokeza hasa wakati wahusika Juma na Kitaru wanapolitumia neno hili likiambatanishwa na neno la kimombo ‘chief’kuashiria utukufu wa daraja la juu katika jamii dhidi ya daraja la chini la walalahoi. Dondoo ifuatayo inaleta usawiri hu kama ifuatavyo:

KITARU: Ah, Mheshimiwa.

JUMA: Unasemaje chief? Nasikia unalala tu. Holiday inakupa time kidogo. (uk. 14).

Kutokana na dondoo hii, inabainika bayana kwamba dhana ya kutambulishana kwa msamiati ‘mheshimiwa’ limepata rotuba nafasi na matumizi yasiyo kifani katika jamii

za nchi zilizoko barani humu Afrika. Ni wazi kuwa katika jamii barani humu, watawala hufahamika kama ‘waheshimiwa’ neno hili likiwapendeza wengi wao wanaolienzi kwani linawainua Zaidi na kuwaonyesha kuwa wa daraja muhimu na la juu Zaidi kuliko wengine au watawaliwa. Kwingineko, Massoud (2018) aonya kwamba yapaswa neno hili lisiendelee kutumika katika namna hiyo inayochochea na kupelekea kukita mizizi kwa utabaka ambao ni adui mkubwa wa usawa na undugu katika jamii. Salem (2013) vilevile anaonya kuwa maana hiyo huenda ikachochea ugumu unaojibainisha katika kuunganika kwa utafu.

Katika tamthilia hii, mwandishi amemulika matumizi ya neno ‘bwana’ kijazanda kama ifuatavyo:

JUMA: Je, ‘bwana’ yupo?”

MAMA: Hata. Utamweza siku hizi. Anafanya kazi usiku na machana! Hana kituo. Yeye na baba yako hajulikani anayempita mweziwe. Afadhali baba yako, kazi yake iko nyumbani. Je ulikuwa na shida naye!

JUMA: Hapana. Nilitaka kumwamkia tu. (Uk.14)

Dondoo hii inajitokeza wakati Juma alipofika kwa kina Kitaru na kumuuliza mamake Kitaru iwapo Kitaru alikuwepo, huku Juma akimtabulisha kama ‘Bwana’. Akitoa uchanganuzi wa dondoo hizi, Salem (2013) aeleza ya kwamba wahusika Juma Pamoja na mwenziwe Kitaru waashiria uzao wa tukio hili lililo na msingi wa kihistoria hasa sababu yao kutambuana kama ‘mheshimiwa.’ Vilevile, Salem (2013) anaeleza kuwa Azimio la Arusha lilifahamu athari ya matumizi ya neno hili katika kueneza utabaka na hivyo kuhimiza na kuwataka watu kuchochea usawa nchini kote hivyo kuwataka watu wote kutambulishana kama ‘ndugu’ na wala si ‘mheshimiwa’. Hii ina maana kwamba waasisi wa Azimio la Arusha walikuwa macho wazi na hivyo kuiona athari iliyosababishwa na matumizi ya neno ‘mheshimiwa’.

4.2.2 Taswira

Taswira ni mbinu moja wapo ya lugha iliyotumika na mwandishi Ebrahim Hussein katika tamthilia ya *Mashetani*. Taswira ni lugha ya picha ya kitu au mahali kwa kutumia ishara (Massoud, 2018). Kwa mujibu wa Massoud (2018), kuna aina tofauti za taswira zikiwemo taswira zionekana, taswira za hisi na za kimawazo. Vile vile, kuna taswira ya kimaono na ya kiishara huku taswira ya kiishara ikitumika na wanatamthilia kuonyesha kwamba kitu fulani kinawakilisha kingine (Ikuathu, 2017). Mfano wa matumizi ya tamthilia ya kiishara katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ni matumizi ya jina Sheta (Shetani) anayewakilisha wakoloni mamboleo wanaofyonza rasilimali za bara la Kiafrika na kulidhibiti bara hili kwa hiari na kutaka kwao (Nzilu, 2018). Mwanatamthilia Ebrahim Hussein (1971) ametumia mtindo wa mbinu ya kitaswira katika kueleza maudhui ya kazi yake ya sanaa. Baadhi ya taswira zinazojitokeza katika kazi hizi ni Shetani, Binadamu na Mbuyu zinazotumika katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na kuendelezwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) kuashiria mambo fulani mahususi. Katika kutumia mbinu hii ya taswira, mwandishi anatumia maneno ya kisitiari na ishara katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na kisha msomaji anapaswa kuelewa maana za kiishara zilizobebwa na maneno hayo. Inajibainisha kuwa msanii ametumia mhusika Shetani kuashiria au kuiweka wazi picha ya ukoloni mamboleo. Katika tamthilia ya *Mashetani* (1971), mtunzi Ebrahim Hussein anajaribu kuuchora ukoloni mamboleo kwa kutumia sitiari ya mhusika Shetani kama inavyobainika katika dondoo ifuatayo:

SHETANI: Unanijua mimi nani?

Ninajenga.

Ninabomoa.

Ninatukuza.

Ninadhaliisha nitakavyo... (Uk1)

Katika muktadha wa tamthilia hii ya *Mashetani*, mtunzi Hussein ametumia sitiari ya binadamu kutuchorea taswira kama watawaliwa ambao wanaishi na Shetani ambaye anawanyonya, kuwadhalilisha na vile vile kuwatumia vibaya katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii. Hata hivyo, mwanathamthilia Ebrahim (1971) ametumia wahusika shetani na binadamu kujaribu kuashiria na kuwasilisha maudhui ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa hasa baada ya nchi za kiasia kupata uhuru. Kwa sababu hii, mbinu hii ya taswira inamsaidia msomaji kupata ujumbe wa ndani na wa nje unaowasilishwa na mtunzi. Hii inajitokeza kama ifuatavyo katika Mashetani (1971):

SHETANI: Unanicha?

BINADAMU: Ndiyo.

SHETANI: Unaninyenyekea?

BINADAMU: Ndiyo.

SHETANI: Mbona siuoni unyenyekevu wala uoga katika uso wako?

BINADAMU: Kipitacho moyoni si lazma kionekane usoni. (uk 2)

S.A Mohamed katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) anaonekana kuathiriwa kimtindo na Ebrahim Hussein katika kazi ya Hussein ya *Mashetani* (1971). Said Ahmed Mohammed anatumia aina mbalimbali za taswira kama mtindo wa lugha na kwa kila aina alikuwa na lengo fulani za kuibua athari tofauti kwa wasomaji wa kazi zake.

4.2.2.1 Taswira ya Shetani

Mhusika Shetani anajulikana na kuchora taswira kama kiumbe wa sifa ya matendo mabaya katika tamthilia hii ya *Mashetani* (1971) na hasa katika *Mashetani Wamerudi* (2016) inayorejelea taswira hii ya mhusika Shetani. Shetani kulingana na muktadha wa *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016) analeta taswira ya viongozi wadhalimu ambao wanawadhulumu wanyonge katika jamii na kuwasababishia maafa (Massoud, 2018). Kwa mujibu wa maelezo yanayotolewa na Nzilu (2018) kuhusu

taswira ya Shetani, mhusika huyu anaonekana kubeba taswira ya kiumbe malaika mwasi aliyelaaniwa na Mungu kutokana na uasi wake. Hivyo, mhusika Shetani analeta taswira ya viongozi walaghai na wenye dhuluma wanaowakandamiza walalahoi katika jamii kupitia nguvu zisizo kifani wanazomiliki (Nzilu, 2018). Vile vile, Muusya (2019) akubaliana na Nzili (2018) kwamba taswira ya Shetani yaashiria viongozi wa kikoloni wanaoendelea kulidhibiti bara Afrika kwa kuliamrisha kufanya kama wanavyotaka pasipo pingamizi au mapendekezo ama kuhusishwa kwa viongozi wa bara hili la walalahoi. Hivyo basi, muonekano huu wa mhusika Shetani unaashiria viongozi wa kikoloni katika tamthilia hizi mbili za *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016). Muusya (2019) atoa mfano wa taswira ya Shetani kama inayoashiria viongozi wa kikoloni kupitia kitendo cha Shetani kumtupia kijana mzinga na vile vile kumkojolea kuwa ishara ya dhuluma na ukandamizaji anazoziendeleza mkoloni dhidi ya wanyonge wanaoashiria bara la Afrika (Mashetani Wamerudi uk.11-12). Kutokana na taswira hii, inabainika kwamba matumizi ya kiumbe Shetani yanabainisha kuwa taswira nzima ya Shetani inampevua msomaji kuhusu mbinu zinazotumiwa na viongozi wa kiubepari kuwadhulumu wanajamii wanaowatawala. Isitoshe, sintofahamu kati ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa linaangaziwa kupitia taswira ya Shetani katika tamthilia hizi mbili.

Tunafahamishwa kuwa mashetani huwa na nia mbaya kila wakati kwa watawaliwa. Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016), mhusika shetani na profesa katika maongezi yao wanaonyesha bayana lengo la mashetani.

SHETA: Sisi unajua kwamba tuna mazingaombwe. Tena ni wepesi kwetu kuwapa watu ugonjwa wa kizunguzungu. Ndio maana mmetupa jina la kizunguzungu? (Uk.20)

Nzilu (2018) vile vile anapiga msasa matumizi haya ya taswira katika dondoo hii kwa kueleza kwamba Shetani alikuwa akimueleza maneno hayo mhusika Profesa ambaye

anatoka katika tabaka la chini la walalahoi linaloahiria Waafrika. Kwa mujibu wa Nzilu (2018), maelezo yanayojitokeza katika dondoo hii yanamuonyesha Shetani kuwa kiumbe mwenye uwezo mkubwa wa kuamrisha mambo katika ulimwengu anaoutawala. Yaani, maana yeake ni kwamba Shetani ana uwezo usio kifani wa kufanya lolote atakalo na kumthibiti takriban kila kitu ulimwengu mzima hivyo kuchora taswira ya uwezo wa kupita kifani alio nao mzungu dhidi ya Waafrika anaowanyanyasa na kuwakandamiza kupitia dhana ya ukombozi mamboleo. Maelezo haya yanatujaza kiumbe ambaye ana uwezo mkubwa wa kuamrisha katika utawala wake kwa kufanya atakavyo na kudhibiti takribani kila kitu. Taswira ya shetani inayotumiwa na S.A Mohamed (2016) inalenga kumzindua msomaji dhidi ya unyanyasaji unaoendelezwa na viongozi kwa sababu ya tamaa ya uongozi na kumpevua kimawazo kwa kumwonyesha mwanga wa hali halisia ya unyanyasaji na udikteta wanaoupitia mikononi mwa viongozi wao.

Ili kuonyesha uwezo wa Sheta kama unavyojitokeza katika dondoo iloanagaziwa kwa kina hapo awali, Nzilu (2018) aeleza kuhusu matumizi ya kiishara ya chombo cha ‘remote control’ anachotumia Sheta kulidhibiti bara la Afrika Pamoja na kudhibiti raslimali zake kupitia ukoloni mamboleo kama ifuatavyo katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*:

SHETA: Hapana nguvu yoyote ya kutudhibiti, maana sisi tuko nchini mwetu tunabonyeza remote control. Kwani mmesahau kwamba utandawazi ndio remote control Zaidi kuliko ukoloni mamboleo? (UK.61)

Kutokana na msasa anaoupiga dondoo hii, Nzilu (2018) akiungwa mkono na Muusya (2019) waeleza kwamba dondoo hii yaonyesha jinsi taswira ya Shetani (wakoloni mamboleo) inavyomwashiria kama kiumbe mwenye kuwadhibiti na kuwaumiza walalahoi katika jamii hasa ya barani Afrika kwa kutumia utandawazi. Hii ndio maana hasa ya ishara inayobebwa na ‘remote control’ (Muusya, 2019).

4.2.2.2 Taswira ya Mwanamke

Katika kazi nyingi za sanaa mwanamke hupewa sifa za kiumbe dhaifu mwenye nafasi ya chini na kama chombo cha kumfurahisha mwanamume (George, 2014). Katika tamthilia hii ya *Mashetani Wamerudi*, mwandishi amechora mwanamke kama shujaa, mwanamapinduzi na mwanaharakati wala si kiumbe duni tena. Mwanamke anaonekana yumo mstari wa mbele kupigania haki na mabadiliko katika jamii. Isitoshe, mbinu hii ya taswira inatumika kama chombo cha mwandishi kupitisha ujumbe wa maudhui ya nafasi ya mwanamke katika jamii. Kwa hivyo, mwanamke kwa jina la mhusika aitwaye Msichana katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) anapigania mageuzi bila woga na amejitolea kuwapa vijana wasia ili wasikubali kutumiwa na viongozi kwa ajili ya manufaa yao. Hali hii inaonyesha weledi na ukakamavu wa mwanamke kuchangia katika masuala nyeti ya jamii na kumpevu mwafrika kuwa mwanamke ana uwezo wa kusaidia jamii kuenda mbele kwa nafasi yoyote ile atakayotegemewa kutekeleza. Katika *Mashetani Wamerudi* (2016), hii inajibainisha kama ifuatavyo katika dondoo hii:

MSICHANA: ...nimefika kwenye maskani ya utetezi. Wapi pengine pakushtakia kama si hapa? Ukweli uko wapi? Tunauona uongo unaoning'inizwa hewani? Hakuna haja ya kukata kauli. Tuseme tu. Hakuna haja ya kukimya. Hakuna sababu ya kufa wakati tuko hai. Kwa nini haturudi kwenye mwanzo uliowafukuza mashetani. Nguvu za umma kila siku zinafaulu. (Uk.32)

4.2.3 Utohozi

Waandishi wa sanaa ya kazi za fasihi simulizi na fasihi andishi hutumia mtindo wa lugha wa utohozi ili kuswahilisha maneno ya lugha nyingine ili yatoe matamshi ya Kiswahili yakitamkika. Bila shaka, mbinu hii imetumika katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) ili kuleta dhamira ya mwandishi kwa msomaji au hadhira yake.

Katika onyesho la pili iliyoko sehemu ya pili ya tamthilia ya *Mashetani* (1971), mwandishi anamtumia mhusika ambaye ni babaye Kitaru ili kuonyesha tamaduni ya mkoloni iliyokumbatiwa pindi alipoondoka bara la Afrika. Mwafrika anaonekana kuacha utamaduni wa kutumia miti shamba iliyoaminiwa kuwa na nguvu za kuponya. Mbinu hii inaonyesha na kutueleza ya kwamba mkoloni anaeza kua hayupo tena lakini athari alizoacha bado zinatawala katika bara la Afrika. Dondoo ifuatayo inathibitisha hili:

MAMA: Anasema kichwa tu kinamuuma.

BABA: Mpe **asprini**. (Uk 26)

Wachunguzi Ngesa, Matundura na Kobia (2015) vilevile wameangazia jinsi mtindo wa utohozi ulivyojitokeza katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) ya Ebrahim Hussein. Uchunguzi wao wabainisha kwamba mtindo huu wa utohozi umetumika na mwanatamthilia huyu kuyaendeleza maudhui ya ukoloni mamboleo na athari yake kwa Waafrika ambao wanashirikiana na Wazungu wenye nguvu. Hivyo basi, yabainika kwamba swala la ukoloni mamboleo vilevile limeainishwa na kukaririwa katika tamthilia ya Ebrahim Hussein ya *Mashetani* kupitia njia ya kimtindo ya utohozi ambayo yajitokeza katika dondoo ifuatayo:

JUMA: Twende senema basi. Itakusaidia.

KITARU: Hakuna senema nzuri.

JUMA: Iko cowboy moja. Tikiti juu yangu.

KITARU: Senema yenyewe ninajua hata kabla sijaiona. Cowboy atawaua Red Indians wote. (*Mashetani*: 18)

Kwa mujibu wa Ngesa, Matundura na Kobia (2015), mtunzi Ebrahim Hussein ametumia utohozi kuonyesha jinsi ukoloni mamboleo unavyomfinyilia na kumuumiza Mwafrika anayebainishwa kupitia utohozi wa neno la kimombo 'Red Indians' huku neno 'cowboy' linalomwashiria mzungu mwenye kuendeleza ukoloni mamboleo likitoholewa vile vile kutoka lugha ya Kimombo.

Kwingineko, mwanatamthilia Ebrahim anatudokezea katika uandishi wake wa *Mashetani* jinsi matabaka yalivyotokea pindi mkoloni alipo salimu amri na kurejea makwao. Mwandishi Ebrahim Hussein (1971), anamtumia mhusika Bibi kuonyesha tabaka la tajiri na maskini miongoni mwa waafrika. Haya yanabainika katika maongezi ya Bibiye Juma anapoongelea familia ya kina Kitaru kwa mukhtasari. Kulingana na umri wake mkongwe, mhusika Bibiye Juma anasema kuwa katika enzi za ukoloni walikua na mali bali wakaporwa baada ya wakoloni hao kuondoka. Maudhui ya Matabaka yandhihirishwa katika mbinu ya utohozi na tamthilia hii ya *Mashetani* (1971) kwa ujumla kama ifuatavyo katika dondoo hii:

BIBI: Yeye akiwa na ‘mabenzi’ na wewe Mungu atakupa zaidi ya hayo. Kwani hilo si geni kwako. Ulikua na mangapi, licha ya benzi. Ulikua na mashamba maddal basari. Ulikua na watu chini yako. Haya yaliyopita si basi tu, mwenyewe Mungu ndivyo alivyopenda-mali yetu kuchukuliwa na kugaiwa watu. Watu tu hivi hivi. Watu wasiojua hata maana ya milki ni nini. (uk38)

Vile vile, inabainika bayana kwamba mbinu hii ya utohozi imetumika na kuendelezwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) na mwanathamthilia Said. A. Mohammed ambaye huenda aliathiriwa na Ebrahim Hussein kimtindo katika kazi hii ya fasihi (Massoud, 2018). Mbinu hii inaonekana bayana katika mazungumzo ya Profesa na Sheta na kuleta maudhui ya ukoloni mamboleo. Mwandishi anatuonyesha jinsi ukoloni mamboleo umekita mizizi hata baada ya mabeberu kuondoka. Kwa mujibu wa Massoud (2018), utanadwazi ndio njia inayotumika katika ukoloni maomboleo ambapo mwafrika anatumia mbinu ya kisasa katika mawasiliano. Said (2016), anatuonyesha hali hii inaweza mpelekea mtu kuasi utamaduni wake halisi na kufuata ule wa mkoloni hivyo basi kuingia bado kwa mtego wake wa kutawaliwa naye.

SHETA: Umepanuka vipi mgogoro wetu?

PROF: Ujamii, utamaduni, elimu, uchumi, teknolojia, sayansi, kilimo, vyote hivi vimebanwa. Ndiyo, sisi wenyewe hatuyachangamkii mambo haya. (Uk 23)

Kwa mijibu wa dondoo hii, inabainika kwamba mwandishi Said Mohamed ameathirika kimtindo katika matumizi ya utohozi kama inavyoainishwa katika dondoo hii. Kwingineko, katika enzi ya ukoloni mamboleo, mzungu bado anamtawala mwafrika kwa kumwekea miundo misingi ambapo Mwafrika bado atamtegemea. Mkoloni hayuko katika maeneo ya mwafrika lakini mbinu za kisasa za kuishi zimetengenezwa na mzungu hivyo basi mwafrika hulazimika kuomba msaada kutoka kwake ili kujimudu kimaisha (Ngesa, Kobia & Matundura, 2015). Hali hii inamfanya Mwafrika kuwa kikaragosi cha mbeberu na hivyo basi yeye kukatisha kutawaliwa kwake na mkoloni ni ngumu. Mbinu hii ya lugha pia inatia natja maudhui ya ukoloni mamboleo kwa kupitia mhusika Sheta. Katika Mashetani Wamerudi (2016), hii inabainika katika dondoo ifuatayo:

SHETA: Sikiliza kijana. Sisi ndio watoa chakula na maji mnapokuwa na njaa na kiu. Tunawakopeshe ni mnapofilisika. Tunawapa ‘cheki za mamilioni’ kwa mamilioni mnapokuwa na haja au dhiki. Sisi ndio tunaolea mifumo ya elimu mnaioyendeleza. Sisi ndio tunaosambaza tamaduni za uungwana... (uk50)

Kwa mijibu wa dondoo anuwai zilizoainishwa hapo juu, inabainika kwamba athari za tamthilia ya *Mashetani* (1971) kimtindo zimekolea katika tamthilia ya Said Ahmed Mohamed ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Hii yatokana na matokeo ya utafiti yanayodhihirisha urejeleaji wa matumizi ya mbinu ya lugha ya utohozi inayoonyesha jinsi watunzi Ebrahim Hussein na Said Mohamed walivyoyaomba maneno ya Kiingereza na kuyatohoa katika kuwasilisha maudhui tofauti kama vile yale ya ukoloni mamboleo katika tamthilia zao husika zinazomulikwa katika utafiti huu.

4.2.4 Lakabu

Lakabu ni mbinu ya mhusika kubandikwa jina na mhusika/wahusika wengine ama pia yeye mwenyewe kujipatia jina linoloambatana na sifa ama vilevile tabia zake. Katika tamthilia ya *Mashetani* kuna mchezo ndani ya mchezo ambapo mhusika Juma na Kitaru wanapeana majina ya Shetani na Binadamu kwa kufuatana. Majina Shetani na Binadamu ni lakabu maana pia majina hayo yanaoana na sifa zao kwa mpigo. Shetani anapewa sifa za mkoloni ambaye ni mnyanyasaji, mkandamizaji, muuaji na mwaribifu. Kwingineko, Binadamu anapewa tabia kuashiria umbo la Mwafrika na bara la Afrika kwa ujumla. Katika mchezo huo Shetani anamkandamiza na kumfanya Binadamu kuonekana kama kiumbe mdhaifu asiye uwezo. Vilevile, mbinu ya lakabu pia inatumiwa na mwandishi kupitisha maudhui ya ukoloni, utabaka na ukandamizaji kama ifuatavyo katika dondoo hii:

SHETANI: Huinioni. Huwezi kuniona. Nimejigeuza upepo. Hunioni lakini unanihisi. Huna la kunifanya eh? Wewe huogopi kugombana na mtu usiyemwona na ambaye anakuona?

BINADAMU: Acha kunitisha. Sitishiki hivyo. Kama mwanamume kweli, jitokeze. (Uk 5)

Mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani* anatuchorea picha kamili na kutuonyesha jinsi wahusika wawili wanapania kuucheza mchezo mwingine. Mbinu ya lakabu inadhihirika pale ambapo Kitaru anataka awe Shetani na Juma awe Binadamu. Mpango huo unakosa kutimia pale ambapo Juma anakataa kukubali mapendekezo ya Kitaru (Nzilu, 2018). Mwandishi anatuonyesha kwamba matabaka mawili yenye uwezo tofauti hayawezi kuwa kitu kimoja. Vilevile imebainika kwamba mkoloni hana maneno mazuri ya kutakia bara la Afrika kwa ujumla ila anataka yeye awe juu na aendelee kumkandamiza na kumtawala mwafrika.

JUMA: Wananchi kwa mara nyingine chini ya mbuyu huu mimi Juma, na rafiki yangu Kitaru, tutakuonesheni mchezo wa ‘Shetani’ na ‘Binadamu’. Mimi nitakuwa Shetani, na Kitaru, atakuwa Binadamu. (uk1)

KITARU: Safari hii mimi ninataka kujaribu kuwa Shetani.

JUMA: Tucheze kama zamani.

KITARU: Hapana, sasa mimi nataka kuwa Shetani.

JUMA: Hapana. Mimi nitakuwa Shetani.

KITARU: Sikiliza kwanza. Wewe ulishakuwa Shetani mara moja. Sasa zamu yangu. (Uk 54)

Mwandishi wa tamthilia *Mashetani Wamerudi*, Said Mohamed anaendeleza mbinu ya lakabu iliyotumiwa katika tamthilia ya *Mashetani*. Katika tamthilia hii, mhusika Mzee Kitaru anatumika kuonyesha majina aliyopewa katika enzi za zama na tabia zinazoambatana na majina hayo (Massoud, 2018). Majina aliyopewa yanajenga picha za unyakuzi, utajiri, ufidadi na uporaji hivyo basi kuonyesha dhana ya mwafrika kumdhaliisha Mwafrika mwenzake pindi tu mabeberu walipoondoka bara la Afrika (Massoud, 2018; Nzilu, 2018). Hii inajionyesha katika dondoo ifuatayo:

MZEE KITARU: ... Aaa, mnajua kwamba mimi nilikuwa na kiburi kisicho na maana. Kwa hali hiyo hata marafiki zangu waliniita majina mengi...mapozi, mpandangazi, limbukeni, kupe, bwanyenye, mla-mali-ya-umma...Aaa orodha ndefu isiyokuwa na mwisho! (Uk 41)

4.2.5 Tashihisi

Kwa mujibu wa maelezo yanayotolewa na Maguo na Alhabib (2021), tashihisi ni mojawapo wa mtindo wa lugha unaotumiwa na wasanii ili kukipatia kitu kisicho uhai sifa za uhai ama za mwanadamu. Tunapoendelea kuangazia athari za mbinu ya lugha ya tamthilia ya *Mashetani* (1971) kwa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) tashihisi imeweza pia kungaziwa ili kupitisha ujumbe wa mwandishi. Mwanatamthilia Ebrahim Hussein anatumia mbinu hii katika kazi yake kupitisha ujumbe wa ukoloni na kuleta dhana ya jinsi tabaka lililonyakua mali pindi wakoloni walipoondoka wanavyoishi maisha ya kibinafsi na ya kujitakia pasipo kuwajali wananchi wa tabaka la chini. Msomaji na hadhira anaona jambo hili kutoka kwa mazungumzo na

maonyeshi baina ya Mama na Baba Kitaru. Gari jipya la Baba Kitaru kwa jina la ‘Benz’ limepewa sifa za ndege.

BABA KITARU: Shhh.... Njoo, njooni nikuonesheni kitu.

MAMA KITARU: Nini?

BABA KITARU: Ndege wangu.

JUMA NA KITARU: Ndege!

MAMA KITARU: Ndege?

BABA KITARU: Njooni hapa dirishani. Unaiona nini?

MAMA KITARU: Gari mpya! Benz!

BABA KITARU: ...Tazama ilivyotulia. Basi pale itoneshe tu-waah, linaruka kama ndege. (Uk 22)

Mwanatamthilia Ebrahim ameizindua mbinu hii mwishoni mwa tamthilia yake ya *Mashetani* (1971). Mwandishi anamtumia mhusika Kitaru kupitisha habari kuwa mwafrika hafai kukubali kuendelea kukumbatia kasumba ya mabeberu kwa namna jinsi walikua wanawapotosha katika enzi za zama. Hadhira ama msomaji anaraiwa kuendelea kujikwamua kifikra ili awe na mwanzo mpya ambapo katu kamwe hautamrudisha kwa maisha ya kale ya minyororo.

KITARU: Huwezi kusema umeshindwa kabla hujajaribu. Hutaki hata kujaribu. Juma, kesho nitakupitia. Umeskia? Umeskia? Hatuwezi kuacha hadithi za jana zitawale roho zetu. (Uk 57)

Athari ya mbinu hii ya lugha kama ilivyotumika na mwandishi Ebrahim Mohammed inaibainisha au kudokeza athari zake katika uandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) vilevile amejumuisha mbinu hii ya lugha katika uandishi wake. Kazi yake iliyo na mchanganyiko wa fasihi simulizi na andishi bado ina jukumu la kupitisha ujumbe wa mwandishi, kuonyesha usawiri wa wahusika na hatimaye kueleza maudhui yaliyotumika ili isawazishe kazi ya sanaa. Katika kazi hii, mwandishi anauhaiisha mduara na kuleta ile dhana ya umoja, ushirikiano na upendo unaofaa kuwa miongoni mwa waafrika ili kurahisisha vita dhidi ya ukoloni mamboleo (Massoud, 2018).

Kwingineko, Senkoro (2011) aleleza kwamba mwanatamthilia Said Mohammed anamtumia mhusika Prof kupitisha ujumbe huu mwafaka.

PROF: Dunia ni dunia Kijana. **Duara linafinya.**
Linafumba. Lina taabu kupangua.
Linashirikisha. Linalinda. Linafanya
tutazamane. Kisha tushirikiane. (Uk 30)

Katika harakati za kuitetea jamii, mwanatamthilia wa *Mashetani Wamerudi*, Mohamed (2016) anamtumia mhusika Msichana kama mwanaharakati wa kuleta mabadiliko katika jamii husika. Mwandishi anaonyesha mbinu ya lugha ya tashihisi na maudhui ya nafasi ya mwanamke katika jamii ili kupitisha mapendekezo kwa msomaji. Mhusika Msichana anonekana kama nguzo muhimu katika kuonyesha harakati za mwafrika kujikomboa. Katika wakati huu wa ukoloni mamboleo, mwandishi anampevua msomaji kuwa mwanamke akipewa nafasi, nguvu na uwezo, anaweza kuwa nguzo muhimu sio tu katika harakati za kutafuta ukombozi pekee bali pia katika kusaidia jamii yake kuinuka kwa viwango vya juu kama inavyosisitizwa katika dondoo ifuatayo:

MSICHANA: Nimefika duarani. Nimefika kwenye maskani ya utetezi. Wapi pengine pa kushtakia kama si hapa? Ukweli uko wapi? **Tunauona uongo unaoning'inizwa hewani?**

4.2.6 Kuchanganya Ndimi

Kuchanganya ndimi ni mbinu ya lugha itumiwayo katika kazi za fasihi ili kuingiza maneno yasiyo ya Kiswahili katika sentensi ya Kiswahili. Ebrahim Hussein (1971) ametumia mtindo huu vilevile katika kazi yake ya *Mashetani*. Mfumo huu wa lugha umeenea pakubwa katika kuwasilisha ujumbe katika tamthilia ya *Mashetani*. Hussein anatuonyesha katika mbinu hii ya kuchanganya ndimi jinsi maudhui ya malumbano na vita vya ubabe ulivyokithiri mno. Wahusika wakuu katika tamthilia hii Juma na Kitaru wanatuonyesha vile mwambangoma anvyovutia upande wake.

KITARU: Siyo bwana. Mi *cowboy films* sipendi.

JUMA: Alaa,

KITARU: Senema yenyewe ninaijua hata kabla sijaiona. *Cowboy* atawaua *Red Indians wote* peke yake, Mimi, mchezo ukaonyesha ugomvi au mgongano baina ya mwenye nguvu na asiye nguvu, sipendi (uk 18).

Mwanatamthilia anatomia mbinu ya kuchanganya ndimi kuonyesha jinsi waafrika wameathirika na kasumba ya kikoloni katika kujistarehesha. Ebrahim (1971) anatuonyesha jinsi waafrika wanavurugana wenyewe kwa wenyewe.

MTU 1: Ah, nishaelewa bwana. Basi mimi sijui *double* na *single* bwana? Tunakunywa *whisky* siku zote hizi chifu; namna gani?

MTUMISHI 1: Wazee, hamjanijibu bado.

MTU 1: Tunajibu nini tena? Tumeshakwambia utuletee nini. Sasa bado nini tena? (Uk41)

MTUMISHI 1: *Double whisky*, wapi? Hapa? *Double whisky*, a hapa...beer. (Uk 41)

Tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* pia inaangazia mbinu ya uchanganyaji ndimi. Mbinu ya lugha hii kwa mukhtasari hunuia kupitisha lengo, maudhui na mafundisho ya mwandishi kwa hadhira yake (Massoud, 2018). Mwanatamthilia Said. A. Mohammed (2016), amekusudia kutumia mbinu hii kama ilivyotumika na mwanathamthilia Ebrahim Hussein katika tamthilia ya *Mashetani* (1971). Nzilu (2018) aeleza kwamba lugha isiyo ya Kiswahili huleta uzito wa uhalisia wa jambo linalozungumzwa hasa ya kimombo ambapo inajulikana kama ni ndio lugha rasmi inayotambulika ya wakoloni.

Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016), lugha ya kimombo inatumiwa kuashiria utamaduni na ushawishi wa kikoloni hasa kwa wakati uliopo (Sarara, 1997).

Wakoloni wanajaribu kutuziba macho kwa kuonyesha kuwa utamaduni na utandawazi wao ni bora kuliko ule wa waafrika kama inavyonukuliwa katika dondoo ifuatayo:

PROF: Aaaa, togwa tamu hii. Tamu tokea kinywani mpaka damuni. *Coca Cola* itawezaje kutia fora mbele ya togwa? Basi tu – abrogation, yaani vidonge vya dawa ndani ya sharia ya kufuata na kukanusha katika kutuziba vichwa vyetu na kutuchezesha noma kwenye *TV*, ili kibaya kiwe chetu daima na

kizuri kiwe chao daima. Kibaya chao kiwe kizuri chetu! **Coca Cola** si kwa siha wala si kwa ladha yoyote ikilinganishwa na togwa (uk 7,8).

Mwandishi anaonyesha jinsi mabeberu wanapenda kutumia mabavu ili kutawala.

Matendo haya yanatia natija maudhui ya ukoloni mamboleo, mhusika Kijana 1 anasisitiza kuwa ‘ubosi’ huja kwa matendo ya heshima.

KIJANA 1: Mimi sitakubali kulazimishiwa ubosi, kwani ubosi huja kwa matendo ya kuheshimiana. Unakumbuka *Kunta Kinte* wa filamu iitwayo ‘Roots’? (Uk 49)

UMMA: Sisi ni wananchi...Hii ni nchi yetu...Hatutaki kutawaliwa kwa *remote control*... (Uk74)

4.2.7 Maswali ya Balagha

Kwa mujibu wa Okwena (2018), maswali ya balagha humpa uhuru mhusika ama msimulizi kuuliza maswali ambayo hayahitaji majibu. Mbinu hii ya lugha imetumika kwa ujumla katika sehemu tofauti katika tamthilia ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Mwanatamthilia Hussein (1971), alijumuisha mbinu hii katika kazi yake ya fasihi andishi ili kuka bayana lengo alilokuwa akiliwasilisha katika tamthilia ya *Mashetani*. Katika sehemu ya pili onyesho la kwanza mhusika Kitaru anauliza swali la balagha katika maongezi yake na mhusika Juma. Mtindo huu pia unaonyesha maudhui ya utabaki, kulikua na tabaka la mabwenyenye na tabaka la unaizi. Hii inabainika katika dondoo ifuatayo:

KITARU: Sasa mimi nasmea ukweli, wewe unafanya mzaha. Sasa nyinyi mkitwambia hivyo, sisi tuseme nini? Na nyinyi ndio wanahistoria wenyewe (Uk 16).

Mwanatamthilia Ebrahim Hussein bado anaendelea kuonyesha mtindo huu katika mazungumzo ya wahusika Juma na Kitaru. Mbinu hii inaendelea kuweka mkazo nguvu na amri aliyo nayo mkoloni (Shetani). Mtindo huu pia unavumbua macho kuona kuwa mkoloni (Shetani) bado ana ushawishi katika bara la Afrika.

KITARU: Unaogopa mashetani bado? Lo! Hata sikudhania.

JUMA: Tuachilie maneno haya.

KITARU: Unaogopa atakupenda nini? (Uk 17)

Mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani* anafafanua maudhui ya ukoloni katika miktadha mbalimbali. Mbinu hii inatumika kuonyesha umairi na nguvu za mabeberu. Katika maongezi ya Juma na Kitaru, mbinu hii inaonyesha utepetevu na unyonge wa mwafrika katika kujikwamua kutoka kwa minyororo ya mkoloni.

KITARU: Lakini nitamlaani vipi? Nitamuondoa vipi naye kanizunguka?

JUMA: Tia azma, utaweza.

KITARU: Azma itakujaje ikiwa mtu ana shaka... (uk 52)

Mwanatamthilia wa *Mashetani Wamerudi* anaendeleza mbinu hii ya lugha katika uandishi wa tamthilia yake, Said (2016), anatumia wahusika Kijana 1 na Profesa kuleta umbo la mtindo huu. Katika maudhui ya ukoloni mambo leo, maswali ya balagha yanatumiwa kusesitiza na kutia mkazo harakati za waafrika wachache kuendelea kupigania ukombozi wao kwa miaka na mikaka. Walakini, wito unatolewa kwa waafrika wengine kuvumbuka na kuungana mikono ili ima faima wapate uhuru kutokana na ukoloni chipukizi.

KIJANA 1: Lakini sasa tunanyamaza. Hatuna midomo ya kusema?

PROFESA: Miaka au karne. Tunanyamaza huku midomo tunayo. Lakini si sote tunaonyamaza...Tatizo si kusema tu. Tatizo ni nani ananiskia? Nani? Nani? Nani anajali? ... (uk 4)

Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, mwandishi Said anaendelea kuzingatia maudhui ya ukoloni mamboleo kupitia swala la balagha. Anaendelea kuonyesha unyanyapaa na unyanyasaji wa mkoloni katika ardhi la mwafrika. Mkoloni anaomwogofya mwafrika (Profesa) kuwa tayari yeye haezi dhibitika.

SHETA: Mimi nakuona. Wewe hunioni. Huoni kwamba kuna hatari upande wako? kibanda hiki na kibanda kile hatuonani kwa nini? (Uk20)

4.2.8 Inkisari

Inkisari ni mojawapo wa mbinu za lugha zinazotumiwa katika kazi za tamthilia. Inkisari kwa lugha ya kifasihi ni mtindo wa kupunguza au kuyafupisha maneno kwa silabi fulani kwa minajili ya kutosheleza vina au mizani ya mshororo (Maguo & Alhabib, 2021). Katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016) mtindo huu wa lugha umetumika katika njia tofauti. Mwanatamthilia wa *Mashetani* Ebrahim ametumia mtindo huu wakati ambapo wahusika Juma na Kitaru wanalongana wakiwa kwa kina Kitaru (Uk 20):

KITARU: Wewe unataka kwenda senema; mara unanicheza shere. Hata sijui, Mara tunagombana.

JUMA: *Okay*, **sendi** tena senema; nitakusikiliza.

Mwanatamthilia Said Mohammed katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* aliathiriwa kimtindo na pia yeye kutumia mbinu ya inkisari katika kazi yake. Mhusika Prof katika wimbo wake anatumia mbinu hii ya kupunguza silabi ili kutosheleza mizani katika mishororo yake (uk 13). Vilevile mhusika Prof ametumiwa na mwandishi ili kupitisha ujumbe na lengo la kumwamsha mwafrika kutokana na lepe la usingizi la ukoloni mambo leo. Hii inajibainisha ifuatavyo katika *Mashetani Wamerudi* (2016):

PROF: Kwa sababu Waswahili wameimba (Profesa anaimba kwa usanii)

Msegeju ana ng'ombe,

Nami nina ng'ombe wangu,

Kanambia nichanganye,

Sebu nakwenda zangu.

4.2.9 Misemo/Nahau

Misemo ni mbinu ya lugha ambayo hurahisisha kueleza ujumbe wa mwandishi kwa kutumia maneno ambayo hayamaanishi katika hali halisia. Matumizi ya mbinu hii ya

lugha hutumika katika kazi za fasihi ili kufanya lugha ipendeze ama pia hupunguza makali na machukizo ya maneno katika kuwasilisha ujumbe fulani.

Katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) mwandishi Ebrahim Hussein ametumia misemo kama mojawapo ya mtindo wa lugha. Misemo imetumika katika sehemu tofauti tofauti katika kitabu hiki cha Ebrahim Hussein (1971). Vilevile, mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* ametumia misemo anuwai kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira lengwa. Dondoo ifuatayo yabainisha matumizi haya ya misemo:

BABA: Naona *umepigwa na bumbuazi* (uk 24).

Baba Kitaru anamanisha kuwa Kitaru anakaa mwenye mafikirio mengi.

BABA: Ehe bibi, ehe. Ukitakakumwita mganga, we mwite; usije *kunitoa roho* bure. (uk31)

Haya ni mazungumzo katika ya wazazi wa Kitaru. Babake Kitaru anampa mamake rufusa ya kumtafutia matibabu mbadala kutokana na shinikizo alilokua nalo la kutatua shida ya kitaru baada ya yeye kuona kwamba suluhu la awali liligonga mwamba.

4.3 Utofauti wa Mtindo Katika Tamthilia Teule

Licha ya kuchunguza mfanano katika matumizi ya kimtindo katika tamthilia teule, utafiti huu vilevile uliangazia tofauti zinajojitokeza katika matumizi ya kimtindo katika tamthilia teule. Kwa mujibu wa data zilizokusanywa na kuchunguzwa katika utafiti huu, unaonesha kwamba tofauti zilizopo kimtindo baina ya tamthilia teule zipo ilhali kwa kiwango kidogo mno. Huu mtazamo unakubaliana na ule wa Massoud (2018) anayekiri kwamba tofauti za kimtindo baina ya tamthilia ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* ipo japokuwa kwa kiwango kidogo mno.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa, tofauti za kimtindo zinajitokeza kama ifuatavyo; Mitindo ya ngano na mchezo ndani ya mchezo imetumika katika *Mashetani* (1971)

ilhali haijatumika katika *Mashetani Wamerudi* (2016). Kwingineko, mitindo ya lugha ya karaha na lahaja imetumika katika *Mashetani Wamerudi* (2016) bila kutumika katika *Mashetani* (1971).

4.3.1 Matumizi ya Lahaja katika Mashetani Wamerudi

Lahaja ni mtindo mahususi wa lugha wa kieneo au kijamii ujibainishao kupitia seti maalum za kimaneno au vilevile za kimuundo wa kisarufi (Zahra, 2016). Kwingineko, Hans (2017), lahaja yasimamia kitarafu cha kilugha kijibainishacho kijiografia au kijamii na kinachojidhihirisha kupitia vipengele tofauti vya kimuundo na kisauti. Ni kwa sababu hii Zahra (2016) anaeleza kwamba lugha anuwai aghalabu hugawika kutokana na msukumo wa maswala tofauti ya kijamii kama vile umri, dini, matabaka ya kiuchumi, jinsia Pamoja na hadhi ya kitaalamu. Hivyo basi lahaja tofauti husimamia tofauti katika matumizi ya lugha katika viwango vya msamiati, sarufi na matamshi yanayojikita hasa katika fundi Fulani la kijamii (Hans, 2017).

Japo mwandishi wa *Mashetani* anaonekana kutotumia lahaja kama mbinu ya kimtindo, mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* ameitumia mbinu hii mara kadha wa kadha katika kazi yake. Kwa mujibu wa data zilizokusanywa katika utafiti huu, mwandishi anaonekana akitumia hasa lahaja ya Kipemba katika kazi yake. Matumizi ya lahaja yamejitokeza kama ifuatavyo katika *Mashetani Wamerudi*:

“Kiduchu kiduchu (Uk 24)”

“Nitaselelea papa hapa petu” (uk 78)

Maelezo hayo juu yanaonesha jinsi Mohamed (2016) anavyotumia neno ‘kiduchu kiduchu’ ambalo kwa mujibu wa ufafanuzi unaotolewa na Massoud (2018), lina maana ya kidogo huku neno ‘papa hapa’ likimaanisha hapa hapa. Massoud (2018) aeleza kwamba matumizi ya lahaja ya kipemba katika *Mashetani Wamerudi*

yanatokana na historia ya mtunzi Mohamed ambaye ni mzaliwa wa kisiwa cha Pemba hivyo kumaanisha Kipemba ndio lugha yake ya kwanza.

4.3.2 Matumizi ya Karaha

Motanya, Kisurulia na Sawe (2021) wanasema kwamba matumizi ya karaha kimtindo yaashiria matumizi ya maneno yasiyokubalika kutumika kiuwazi katika wanajamii kutokana na aibu yanayofikiriwa kusababisha. Ngunyi (2017) aeleza kuwa karaha ni maneno ya kimatusi kutokana na aibu yanayohusishwa nayo miongoni mwa wanajamii. Ni maneno yasokubalika kuzungumziwa kihadharani katika jamii (Motanya, Kisurulia na Sawe, 2021).

Matumizi ya mtindo wa karaha yanajitokeza katika *Mashetani Wamerudi* bila kutumika katika *Mashetani*. Mohamed (2016) anautumia mtindo wa karaha kama ifuatavyo katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*:

‘Alikojoa’ (uk. 14).

Neno hili ‘alikojoa’ linaonyesha matumizi ya karaha katika *Mashetani Wamerudi* kwani Uswahilini, neno hili huleta utata miongoni mwa wasikilizaji hivyo kupelekea kutumiwa kwa neno ‘kuenda haja ndogo au kujisaidia’ linaloonekana kuwa lenye kukubalika na heshima katika jamii. Vilevile, mifano mingine ya matumizi ya karaha katika *Mashetani Wamerudi* inabainika katika maneno yafuatayo:

- (i) “Si mizinga, si mashuzi Profesa” (uk. 12)
- (ii) “Jamaa zako wanaanza kujikojolea mikojo na kujipaka kinyesi” (uk. 27)
- (iii) “Kinachotisha ni mashuzi” (uk. 19)

Mifano ilioainishwa hapo juu yaonesha jinsi mtindo wa karaha ulivyotumika katika *Mashetani Wamerudi* maneno hayo yakiwa yasiyowezakutamkwa kwa uwazi katika

jamii kwa kuaminiwa kuashiria matusi. Kwa upande mwingine, karaha haijatumika katika *Mashetani*.

4.4 Hitimisho

Sura hii imechambua na kuwasilisha uchanganuzi wa data zilizokusanywa na mtafiti nia hasa ikiwa kulijibu swala la tatu la utafiti huu. Hili ni swala linaloangazia iwapo tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* imeathiriwa kimtindo na tamthilia ya *Mashetani* iliyoitangulia. Katika uchambuzi wa athari za kimtindo baina ya tamthilia teule, mtafiti aling'amua kutokana na data zilizokusanywa kwamba kuna mfanano mkubwa sana baina ya mtindo kama ulivyotumika katika *Mashetani* na katika *Mashetani Wamerudi*. Hii yaonesha kwamba nadharia ya mwingilianomatini ina nafasi kuu ya kueleza athari za kimtindo baina ya tamthilia teule. Kwa mfano, nadharia ya mwingilianomatini iliyoongoza utafiti huu inabainisha mwingiliano unaojitokeza katika matumizi ya maneno kama vile 'waltz' katika tamthilia hizi mbili. Hii inaonesha kwamba mtunzi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ameathiriwa kimtindo na mtunzi wa *Mashetani*. Kwa ujumla, mtafiti ameonyesha katika sura hii kwamba waandishi wa tamthilia teule wametofautiana padogo mno katika mitindo yao tofauti za kimtindo zikijibainisha katika matumizi ya lahaja, ngano, mchezo ndani ya mchezo na matumizi ya lugha ya karaha.

SURA YA TANO

HITIMISHO

5.1 Utangulizi

Sura zilizotangulia zimeshughulikia athari ya tamthilia ya *Mashetani* (1971) juu ya tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Kila sura imeshughulikia dhana moja muhimu kwa kuongozwa na maswali ya utafiti. Sura hii ya tano ndiyo ya mwisho katika utafiti huu. Katika sura hii, mtafiti ametamatisha kwa kutoa muhtasari wa utafiti, mapendekezo ya utafiti na pia changamoto za utafiti.

5.2 Muhtasari wa Utafiti

Lengo la utafiti lilikuwa kuchunguza athari ya tamthilia ya *Mashetani* (1971) juu ya tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Sura ya kwanza ni kitangulizi cha kazi nzima na pia ni muhtasari wa utafiti mzima. Sura ya kwanza ilishughulikia mambo yafuatayo: Usuli wa mada, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na hatimaye mbinu za utafiti. Sura ya pili ilishughulikia athari ya maudhui ya *Mashetani* (1971) kwa maudhui ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Mtafiti alishughulikia maudhui mbalimbali katika tamthilia ya *Mashetani* yalivyoathiri maudhui katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*.

Maudhui haya yalielezwa kwa kuongozwa na nadharia ya Mwingilianomatini. Baadhi ya maudhui yaliyojitokeza katika tamthilia hizi ni yafuatayo: elimu ya kigeni, ukoloni mkongwe, ukoloni mamboleo, utabaka, unyanyasaji na uonevu, kujitolea mhanga, migogoro ya kijamii, ulevi na usherati, unafiki na nafasi ya mwanamke katika jamii. Sura hii ilimalizia kwa kuweka wazi kuwa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ni

uendelezi wa tamthilia ya *Mashetani*. Sura ya tatu ilishughulikia mfanano na tofauti ya usawiri wahusika katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016). Mtafiti ameonyesha kwamba mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) ameathiriwa na mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani* (1971) katika kusawiri wahusika. Mtafiti ameonyesha kuwa wahusika katika tamthilia hizi wamesawiriwa kwa mfanano mkubwa, tofauti zikiwa chache mno. Ilibainika kwamba wahusika Shetani na Sheta, Binadamu na Kijana I na vilvile Prof katika tamthilia hizi teule wamesawiriwa kwa njia ya mfanano. Hii ilibainisha kuwa matini huathiriana kiwahusika.

Sura ya nne ilishughulikia athari za kimtindo katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) kwa *Mashetani Wamerudi* (2016). Mtafiti alionyesha kuwa kuna mfanano wa kimtindo katika tamthilia teule. Baadhi ya mitindo iliojitokeza katika tamthilia ya *Mashetani* na tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ni: Jazanda, taswira, lakabu, tashihisi, kuchanganya ndimi, maswali ya balagha, inkisari na misemo. Kwa hivyo ni wazi kuwa mwandishi Ebrahim Hussein (1971) alimwathiri mwandishi Said Ahmed Mohamed (2016) katika mtindo. Data iliyotumika katika Utafiti huu ilikusanywa kwa kusoma vitabu, makala na tasnifu zilizoshughulikia mada. Data iliyochanganuliwa iliwasilishwa kimaelezo huku Mtafiti akiongozwa na nadharia ya Mwingilianomatini.

5.3 Matokeo

Utafiti huu umethibitisha kwamba tamthilia ya *Mashetani* (1971) imeathiri tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) kwa njia kubwa. Hii ilijibainisha kutokana na maudhui yanayojirejelea katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) yaliokuwa yamemulikwa hapo awali katika tamthilia ya *Mashetani* (1971). Kwa mfano, maudhui ya elimu yanajitokeza katika tamthilia zote mbili husika. Vilevile ilibainika kwamba

katika tamthilia zote mbili, elimu hii ilitokana na misingi ya kiukoloni kwani imerithiwa kutoka kwa wakoloni iwapokuwa elimu katika tamthilia zote husika imesawiriwa kama chombo cha kuwadhalilisha Waafrika.

Kwingineko, maudhui ya ukoloni mkongwe yaliosawiriwa katika *Mashetani* (1971) yanajitokeza tena katika *Mashetani Wamerudi* (2016) ambapo yameelezwa kwa namna ya dhulma wanazopitia Waafrika kutokana na misingi ya ukoloni huo mwkongwe. Vilevile, maudhui haya yanafuatwa na maudhui ya ukoloni mamboleo ambapo utawala wa nchi za kimfumo wa kiubepari unasemekana kuwa na uwezo wa kuathiri hali na shughuli za kiuchumi, kijamii na kisiasa katika nchi zisizo nguvu za barani Afrika. Maudhui mengine yanayojitokeza katika tamthilia zote mbili ni kama ya utabaka ambapo matabaka makuu ni ya unaizi na ya ubwanyenye na maudhui ya ulevi na uasherati. Isitoshe, kuna maudhui mengine kama ya nafasi ya mwanamke katika jamii, maudhui ya unafiki na yale ya uonevu na unyanyasaji yanayomhusisha mkoloni katika tamthilia ya *Mashetani* na tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Mpaka hatua hii, inajibainisha kwamba tamthilia ya *Mashetani* imeathiri tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* kimaudhui kwa njia kubwa.

Lengo la pili lilikuwa kuchunguza usawiri wa wahusika katika tamthilia husika. Ilibainika kuwa kuna utofauti na mfanano unaojitokeza katika usawiri wa wahusika katika tamthilia teule. Utafiti umethibitisha kwamba kuna uwiano katika usawiri wa wahusika katika tamthilia hizi hasa katika hulka na mienendo ya wahusika fulani.

Kwa mfano, inadhihirika kwamba wahusika kama Juma na Sheta wanalingana kwa kuonyesha ukoloni na ukoloni mamboleo. Kwa njia hiyo ya ulinganishi, inabainika ya kwamba Mtu 1 na Mtu 2 katika *Mashetani* (1971) wamesawiriwa sawa na Askari Kanza 1 na Askari Kanza 2 katika *Mashetani Wamerudi* (2016). Wahusika hawa

wanaonyesha jinsi Waafrika hawana umoja na walivyo maadui wa wenzao. Vilevile, Binadamu katika *Mashetani* (1971) ana mfanano na Kijana 1, Kijana 2, Kijana 3, Kijana 4 na Kijana 5 katika *Mashetani Wamerudi* (2016). Ijapokuwa mazingira yao yanatofautiana, wahusika hawa wanamwashiria Mwafrika aliye chini ya uongozi wa mkoloni. Ilhali Ebrahim Hussein anaeleza Binadamu kuwa katika harakati za kupigania uhuru wake, Kijana 5 anazungumzia jinsi alivyohitaji kujinasua kutokana na wimbi la utandawazi lifunikalo tamaduni za Kiafrika, hivyo kuleta hali ya mfanano. Kutokana na wahusika hawa kupambana ili kujinasua kutokana na hali mbalimbali zilizowasonga, ilibainika kwamba usawiri wa wahusika katika *Mashetani* (1971) unafanana na usawiri wa wahusika katika *Mashetani Wamerudi* (2016).

Kwingineko, inabainika kwamba usawiri wa wahusika katika *Mashetani* (1971) vilevile unatofautiana na usawiri wa wahusika katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Utafiti umethibitisha kwamba ijapokuwa Mama Kitaru katika *Mashetani* (1971) na Msichana katika *Mashetani Wamerudi* (2016) wamebuniwa na kutumika kuonyesha nafasi ya mwanamke katika jamii, waandishi Ebrahim Hussein na Said A. Mohamed wametofautiana katika kuujenga upeo wa mazingira ya wahusika hawa. Ni kwa sababu hii, Msichana anapigania uhuru dhidi ya dhulma na mateso yanayosababishwa na ukoloni ilhali Mama Kitaru anajipata katika mazingira tofauti ya manzilini anapojihusisha na juhudi za kuitafutia jamii yake mapato, kando na mwanamume ambaye ni babake Kitaru.

Vilevile, utofauti unajitokeza kupitia wahusika Juma na Kitaru wa *Mashetani* (1971) na Mzee Jumai na Mzee Kitaru wa *Mashetani Wamerudi* (2016). Wahusika Juma na Kitaru katika tamthilia ya *Mashetani* wametumika kuleta dhana ya Mkoloni na Mwafrika mtawaliwa. Inabainika kwamba mwaandishi wa *Mashetani Wamerudi* aliathiriwa na usawiri huo ingawa alitumia vigezo tofauti kuwabuni wahusika Mzee

Jumai na Mzee Kitarui kwa kuwapatia usawiri wa kuerevuka na kuelewa masuala yanayowakabidhi kama watawaliwa.

Lengo la tatu lilikuwa kubaini jinsi tamthilia ya *Mashetani* inavyoathiri tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* kimtindo. Utafiti huu ulithibitisha kuwepo kwa mwingiliano wa mitindo katika tamthilia teule. Hii inajitokeza katika urudiaji wa mbinu za lugha katika tamthilia ya *Mashetani* na tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* tofauti zikiwa chache mno.

Kwa mfano, jinsi mbinu ya utohozi ilivyotumika kubainisha athari za ukoloni kwa mwafrika katika *Mashetani* (1971) ndivyo ilivyotumika kueleza athari za ukoloni kwa Mwafrika katika jamii ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Kwingineko, taswira ya mwanamke imetumika kueneza picha ya mwanamke kuwa shujaa katika *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016). Mitindo ya lakabu, tashihisi, maswali balagha, inkisari, nahau (misemo) na kuchanganya ndimi vilevile inarudiwa katika tamthilia husika.

Aidha, ni muhimu kuweka wazi kwamba licha ya kuwa na uwiano mkubwa wa mitindo ya lugha, tamthilia ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zinatofautiana kimtindo kwa kiasi kidogo. Hii inabainika katika matumizi wa lahaja, ngano, mchezo ndani ya mchezo na lugha ya karaha. Tamthilia ya *Mashetani* (1971) imetumia mbinu ya mtindo ya ngano na mchezo ndani ya mchezo ambazo hazijitokezi katika *Mashetani Wamerudi* (2016). Kwa upande wa pili, tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* nayo imetumia mbinu ya lahaja na lugha ya karaha ambazo hazipatikani katika tamthilia ya *Mashetani*.

5.4 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu umedhihirisha athari ya tamthilia ya *Mashetani* (1971) juu ya tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Utafiti huu utasaidia watunzi wa tamthilia kuelewa jinsi waandishi wa tamthilia za hapo awali wanaweza kuathiri watunzi wa tamthilia za baadaye. Kutokana na hili wanaweza kutunga tamthilia zingine kwa kurejelea tamthilia zilizotungwa hapo awali.

Utafiti huu utawafaidi watunzi wa tanzu zingine za fasihi. Hawa ni kama vile watunzi wa riwaya na hadithi fupi. Wataweza kutunga kazi upya kwa kuendeleza maudhui, wahusika na mtindo katika utunzi wao kwa kurejelea kazi zilizotungwa hapo awali.

Utafiti huu utawanufaisha wanafunzi wa lugha ya Kiswahili. Wataweza kutambua Mwilingianomatini katika tamthilia. Vilevile wataweza kuelewa kuwa licha ya tamthilia kuathiriana kimaudhui, kiwahusika na kimtindo zinaweza kuwa na utofauti katika kusawiri vipengele hivi.

5.5 Mapendekezo

Utafiti huu ulichunguza athari ya tamthilia ya *Mashetani* (1971) juu ya tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Hivyo basi, utafiti mwingine unaweza kufanywa kuchunguza jinsi tamthilia za watunzi tofauti zinavyoathiriana. Waaidha, utafiti mwingine unaweza kufanywa ukiongozwa na nadharia tofauti.

5.6 Changamoto

Utafiti huu umekuwa wa manufaa mengi kwa watafiti waliohusika. Hata hivyo watafiti walikumbana na na matatizo mbalimbali. Kulikuwepo na tatizo la fedha za kufanyia utafiti. Usafiri wa kwenda maktabani uligharimu mtafiti kias i kikubwa cha pesa. Baadhi ya vitabu vilivyohitajika havikuwa maktabani. Mtafiti alipakuwa makala

muhimu kutoka mtandaoni. Pesa nyingi zilitumika katika shughuli hii ya kupakuwa makala kutoka kwenye mtandao.

5.7 Hitimisho

Sura hii imeangazia muhtasari wa matokeo na umuhimu wa utafiti. Mtafiti pia ametaja baadhi ya changamoto alizokumbana nazo wakati wa utafiti.

MAREJELEO

- Abdallah, S. (2018). Kutathmini Ufasihi Simulizi katika Uandishi wa Ebrahim Hussein: Mfano wa *Mashetani, Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).
- AGISO, Y. O. (2017). Mwingiliano matini wa maumbo ya fasihi simulizi ya Kiafrika na matini teule za Biblia (Doctoral dissertation, Maseno University).
- Aiello, F. (2018). Shani Omari and Method Samuel. Fasihi, Lugha na Utamaduni wa Kiswahili na Kiafrika. Kwa Heshima ya Prof. MM Mulokozi. 2018. *Kervan. International Journal of African and Asian Studies*, 22.
- Ali, A. R. (2015). Kuchunguza Dhana Zilizobebwa na Wahusika na Zinavyolandana na Majina yao: Uchunguzi katika Riwaya ya *Kiu na Kiu ya Haki* (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).
- Ali, H. A. (2015). Kutathmini Usawiri wa Mhusika Mwanamke katika Hadithi Simulizi za Wapemba (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).
- Allen, G. (2000). *Intertextuality*. London: Routledge.
- Awhida, H. (2021). Usawiri Wa Mwanamke Katika Utenzi wa Vitimbi vya Wanawake. (2) 20:101-105.
- Bakhtin, M. (1990). *Arts & Answerability*. Austin: University of Texas Press.
- Bakize, L. H. (2021). Usawiri Chanya wa Watoto Katika Fasihi ya Watoto kama Njia Faafu ya Kujenga Jamii Bora ya Leo na Kesho: Mifano Kutoka Vitabu Teule Vya Watoto Vya Kiswahili. *JARIDA LA MNYAMPALA*, 2(1), 83-94.
- Bertoncini, E.Z. (1959). *Outline of Swahili Literature: Prose, Fiction and Drama* Leiden: E.J. Brill.
- Bosibori, B. T. (2016). Mwingilianomatini Kati ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Mstahiki Meya* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).
- Bulaya, J. (2016). Mandhari na usawiri wa ukimwi katika riwaya ya kiswahili 2000-2010 (Doctoral dissertation, University of Dar es Salaam).
- Childs, P., & Fowler, R. (Eds.). (2006). *The Routledge dictionary of literary terms*. Routledge.
- Clemence, S. M. (2015). Kuchunguza Mbinu za Kitanzia za Ki-Aristotle Katika Tamthilia za *Fumo Liongo na Sundiata*.
- Emmel, N. (2013). *Sampling and choosing cases in qualitative research: A realist approach*. Sage. *Kutathmini Mabadiliko ya Usawiri*.

- Fadhili, F. E. (2014). Kuchunguza Dhima ya Mtindo katika Tamthiliya za Kihistoria: Utafiti Linganishi wa Tamthilia za *Morani* na *Kinjeketile* (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).
- Fakih, S. J. (2017). Usawiri wa Mwanamke Katika Riwaya ya *Utengano na Kamwe si Mbali tena: Utafiti Linganishi* (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).
- Fides, C. (2017). Kutathmini Matumizi ya Lugha na Dhamira Katika Tamthilia za *Kinjeketile* na *Nyerere na Safari ya Kanaani: Utafiti Linganishi* (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).
- Fiebach, J. (1997). Ebrahim Hussein's dramaturgy: A Swahili multiculturalist's journey in drama and theater. *Research in African Literatures*, 28(4), 19-37.
- Frolova, N. S. (2007). The renovated poetry of Theobald Mvungi and Said Ahmed Mohamed: on mechanisms of transformation of traditional Swahili verse.
- Fuluge, A. (2023). Matukio ya Mchakato wa Kujiua katika Riwaya ya Rosa Mistika. *Mulika Journal*, 41(2).
- Gaudioso, R., & Minerba, E. (2020). Materialism and Secularism in Swahili Literature: The Case of Topan's Aliyeonja Pepo. *Afrikanistik-Aegyptologie-Online*, 1-23.
- George, G. (2014). Usawiri wa mwanamke katika tamthilia teule za Penina Muhando (Doctoral dissertation, Chuo Kikuu cha Dodoma).
- Haji, A. V. (2018). Kutathimini Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo na Asali Chungu: Utafiti Linganishi* (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).
- Hans, M. M. (2017). Usanifishaji wa Kiswahili Afrika Mashariki: Changamoto na namna ya kukabiliana nazo.
- Herman, L. (2011). Dhima ya Mwingilianomatini kwenye Hadithi za Watoto katika Kiswahili. *Kioo cha Lugha*, 9(1), 73-83.
- Holquist, M. (1990). *Dialogism: Bakhtin and his world*. London: Routledge.
- Hussein, E. (1971). *Mashetani*. Nairobi: Oxford University Press.
- Hussein, E. (1983). Hatua Mbalimbali za Kubuni na Kutunga Tamthilia Kufuatana na Misingi ya Ki-Aristotle. *Makala za Semina Ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III. Fasihi*, 197-205.
- Ikuathu, S. T. (2017). Maudhui ya Ukoloni Mamboleo Katika Tamthilia Teule za Kiswahili (Doctoral dissertation, University of Nairobi).
- Ilomo, L. F. (2017). Mbinu za Ujenzi wa Wahusika na Usawiri wa Sifa Zao: Uhakiki wa Riwaya ya Dunia Uwanja Wa Fujo ya E. Kezilahabi. *Mulika Journal*, 34(1).

- Job, J. N. (2022). Matumizi ya jazanda katika uwasilishaji wa mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Kithaka wa Mberia. *Research Journal in African Languages*, 3(3).
- Kalingwa, F. M., & Kau, T. M. (2023). Mwachiriano kati ya Watunzi wa Riwaya ya Kiswahili: Mwangwi wa Maudhui ya *Mafuta* (2008) na katika *Cheche za Moto* (2008). *Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili*, 6(1), 394-402.
- Kamwara, K., wa Mutiso, K., & Swaleh, A. (2020). Ujenzi wa Ujitambuzinafsi Hasi katika Bunilizi za Omar Babu. *Mwanga wa Lugha*, 5(1), 57-74.
- Kanwa, O. (2022). Usawiri wa wahusika wa Kiume Katika Riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na Wanawake. Chuo Kikuu Cha Kenyatta.
- Karata, R., Muusya, J., & Mavisi, R. (2021). Vipengele vya ontolojia katika tamthilia za Kiswahili: *Mashetani* (1971) na *Kivuli Kinaishi* (1990). *Editon Consortium Journal of Kiswahili*, 3(1), 293-306. katika *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Katutu, R. M. (2013). Mtindo katika diwani ya *Mfuko mtupu na hadithi nyingine* (Doctoral dissertation, University of Nairobi,).
- Kau, T. M. (2015). Tathmini ya Usimilisho wa Riwaya na Hadithi Fupi kwa Wanafunzi wa Sekondari Nchini Kenya (Doctoral dissertation, Kenyatta University).
- Kenduiywa, A. C. (2022). *Uwasilishaji wa wahusika na uhusika wa kimazingaombwe katika riwaya za Watu wa Gehenna (Tom Olali) na Babu alipofufuka (Said Ahmed Mohamed)* (Doctoral dissertation, university of kabianga).
- Khamis, S. A. (2005). Book Review: Alain, R., Ebrahim Hussein: Swahili Theatre and Individualism. *Nordic Journal of African Studies*, 14(3), 10-10. Kimemwozea. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)
- Kimeu, A. N. (2016). *Maudhui Ya Ukombozi Katika Wimbo Mpya na Msururu wa Usaliti* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).
- Kombo, D. K., & Tromp, D. L. (2006). Proposal and thesis writing: An introduction. *Nairobi: Paulines Publications Africa*, 5(1), 814-30.
- Korir, E. J., & Mwamzandi, I. (2019). Vipengele vya Mwingilianomatini katika Ujenzi wa Maudhui ya Umaskini: Mfano Katika Musaleo! na Bina-Adamu! *Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili*, 1(3), 110-117.
- Kristeva, Julia. *Desire in language: A semiotic approach to literature and art*. Columbia University Press, 1980.
- Kuloba, P. Wafula (2015). Mwingilianomatini katika *Cheche za Moto* na *Kidagaa Kimemwozea* (Haijachapishwa)

- Kwambai, M. (2022). Matumizi ya jazanda katika tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga* ya Said A. Mohamed. *Editon Consortium Journal of Kiswahili*, 4(1), 399-403.
- Lewis, A. (1962). *The Contemporary Theatre*. New York: Crown Publisher.
- Longhorn Publishers (2011). *Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja*. Nairobi.
- M’Ngaruthi, T. K., Kobia, J. M., Mukuthuria, M., Ngesa, A. K., Matundura, E., & Kobia, J. (2015). Mwingilianomatini katika Tamthilia za Kiswahili: *Mashetani na Kijiba cha Moyo*.
- Machira, S. (2015). *Uchambuzi wa mikakati ya upole kama inavyotumiwa na wahusika wakuu katika Tamthilia ya Mbaya Wetu* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).
- Maguo, O. M., & Alhabib, E. A. (2021). Mtindo na Wahusika katika Diwani za Dhifa na Wasakatonge. *Mulika Journal*, 39.
- Mahenge, E. (2022). Matumizi ya Mbinu ya Usimulizi katika Kuibua Dhamira ya Ukombozi wa Kisiasa Kusini mwa Afrika: Uchunguzi wa Nyimbo Teule za Muziki wa Dansi nchini Tanzania 1940-1990. *Mulika Journal*, 40(2).
- Makena, M. E. (2018). *Uwasilishaji Wa Maudhui Katika Hadithi Fupi Teule Za Said A. Mohamed* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).
- Masatu, F., Hyera, V., Ndunguru, O., & Ponera, A. (2020). Mwingilianomatini katika Tamthilia ya Utangamano Wetu Ushindi Wetu (2017) ya Anitha E. Mgimba. *East African Journal of Swahili Studies*, 2(2), 128-143.
- Massoud, S. M. A. (2013). *Maudhui na Fani Katika Tamthilia za Kiswahili: Utafiti Linganishi wa Tamthilia za Mashetani na Kivuli Kinaishi* (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).
- Massoud, S. S. (2018). *Kutathmini Matumizi ya Mtindo na Dhamira katika Tamthilia za Mashetani na Mashetani Wamerudi: Utafiti Linganishi* (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).
- Matundura, E., Arege, T. M., & Kobia, J. (2017). Mgogoro wa Ushairi wa Kiswahili Miaka Hamsini Baadaye. *Mwanga wa Lugha*, 1(2), 95-106.
- Mavisi, R. (2016). Usawiri wa Wahusika wa Kike katika Riwaya Teule za Zainabu Burhani. *Kioo cha Lugha*, 16(1).
- Mbatiah, M. (2017). Wahusika wa Kitashtiti katika Gamba la Nyoka. *Mulika Journal*, 34(1).
- Minerba, E. (2017, January). A Frightening Play: The Element of Horror in Hussein's Mashetani. In *Swahili Forum* (Vol. 24).
- Mlama, P. (1983). *Utunzi wa Tamthilia Katika Mazingira ya Tanzania. Fasihi. Dar.*

- Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za nathari ya Kiswahili: tamthilia, riwaya, na hadithi fupi* (Vol. 8). East African Publishers.
- Mohamed, S.A. (2016). *Mashetani Wamerudi*. Nairobi. Spotlight Publishers.
- Mose, E. N. (2021). Motifu ya sanaa za maonyesho ya jadi katika tamthilia ya Kiswahili: mfano wa *Mashetani, Pungwa, Ngoma ya ng'wanamalundi na Mashetani Wamerudi* (Doctoral dissertation, Moi University).
- Mose, E. N., Obuchi, S. M., & Mosol, M. K. (2020). Taswira ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi katika tamthilia ya Kiswahili: Mfano wa Mashetani, Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi na Mashetani Wamerudi. Nairobi Journal of Humanities and Social Sciences, 4(2), 31-59.
- Motanya, M. M., Kisurulia, E., & Sawe, S. (2021). Ukiushi kama elementi ya kimtindo katika baadhi ya riwaya za Ken Walibora. *International Academic Journal of Social Sciences and Education*, 2(2), 340-353.
- M'Raiji, J. (2021). The role of autobiographies and biographies in the promotion of Kiswahili prose. *Research Journal in Modern Languages and Literatures*, 2(2), 20-35.
- Murithi, Jesse. (2002). Usemezano katika Tamthilia ya Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)
- Musimenta, C. (2018). Maudhui na fani katika tamthilia za kiswahili: utafiti linganisifi wa tamthilia za *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi*.
- Muusya, J. K. (2019). Tathmini ya Ujumi Mweusi Katika Tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*.
- Mwaifuge, E. S. (2014). German Colonialism, Memory and Ebrahim Hussein's Kinjeketile.
- Mwangi, E. M. (2021). Swahili literature (fasihi ya kiswahili). *A companion to african literatures*, 79-99.
- Ngesa, A. K., Matundura, E., & Kobia, J. (2015). Mwingilianomatini katika tamthilia za Kiswahili: *Mashetani* na *Kijiba cha Moyo*.
- Ngunyi, S. K. (2017). *Uchunguzi Wa Vipengele Teule Vya Fani Katika Mashetani Wa Alepo* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).
- Njambi, M. M. (2023). Mwingiliano Matini kama Kunga ya Uandishi katika Riwaya za S. A. Mohamed: *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010). *Mwanga wa Lugha*, 8(1), 111-120.
- Njeru, B. N., Kobia, J., & Mugambi, A. (2022). Wahusika na Motifu ya Siri katika Nathari Teule za Fasihi za Kiswahili. *Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili*, 5(1), 234-249.

- Njogu, K., na Chimerah, R.M. (1999). Ufundishaji wa Fasihi. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Njoroge, H. G. (2007). Mwingilianomatini katika fasihi ya Kiswahili: *Tata za Asumina na Rosa Mistika* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).
- Nyabunga, V. A. (2005). *Uhakiki wa Bina- Adamu! (2002) na Musaleo! (2004) na K.W Wamitila* (Doctoral dissertation).
- Nyangweso, S. M., Nancy, D. A., & Sangai, M. E. (2017). Uteuzi na Changamoto zinazomwathiri Kiongozi wa Kike katika Jamii: Mfano wa Mhusika Mkuu Katika Tamthilia Teule za Kiswahili.
- Nzilu, M. D. (2018). Matumizi Ya Taswira Katika Tamthilia Za Said Ahmed Mohamed: *Pungwa, Kivuli Kinaishi na Mashetani Wamerudi* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).
- Nzuki, P. K. (2014). Mwingiliano wa fani na maudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.
- Obondo, P. A. (2023). *Utu wa Wahusika wa Kiuhalisiajabu Katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed* (Doctoral dissertation, JOOUST).
- Ochoki, J. M. (2005). *Sitiari, Jazanda Na Mwingilianomatini Katika Nagona Na Mzingile* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).
- Odhong, J. O., Amukowa, D. N., & Ambuyo, B. A. (2023). Mitindo ya Lugha Inayowabainisha Wahusika Wazimu katika Riwaya za Habwe. *Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili*, 6(1), 243-258.
- Okemwa, K.M (2017). “Mchango wa Fasihi Simulizi katika Fasihi Andishi: Mfano wa Visasili.
- Oketch, S. E., Ambuyo, B. A., & Makokha, R. (2020). Mifumo ya Kijamii katika Tamthilia Teule za Kiswahili. *Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili*, 2(1), 8-18.
- Okwena, S. (2018). Mtindo wa Jazanda katika Tamthilia ya Kijiba Cha Moyo. *Mulika Journal*, 36(1).
- Osore, M. K. (2016). Defamiliarizing Marriage in a Patriarchal Socio-Cultural Context: An Analysis of the Novels of Euphrase Kezilahabi and Said Ahmed Mohamed. *Kiswahili*, 79(1).
- Philipson, R. M. (1989). *Drama and national culture: A Marxist study of Ebrahim Hussein*. The University of Wisconsin-Madison.
- Ponera, A. S., & Kasiga, G. A. (2020). Mdhihiriko wa Kionjo cha Usangwini kwa Mhusika Willy Gamba katika Riwaya ya Njama. *Kioo cha Lugha*, 17(1).
- Pope, C. & Mays, N. (2020). *Qualitative Research in Health*. New Jersey: Wiley-Blackwell. 39

- Salem, S. (2013). Maudhui na Fani katika Tamthilia za Kiswahili: Utafiti Linganishiwa Tamthilia ya *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi*. Tasnifu ya Uzamifu katika Kiswahili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Haijachapisha), Dar es Salaam, Tanzania.
- Sarara, M. M. (1997). Maudhui katika Tamthilia za Said.AMohamed. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Nairobi. (Haijachapishwa), Nairobi, Kenya.
- Senkoro, F.E. M. K. (2011). Fasihi. Dar es Salaam: Kauttu LTD.
- Shivji, I. G. (2002). Haya ni Mahindi, sio Makana.
- Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa tamthilia: historia na maendeleo yake* (Vol. 2). Jomo Kenyatta Foundation.
- Wafula, R. M., & Njogu, K. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation.
- Waithiru, A. K. (2022). Tathmini ya Taashira za Wahusika Katika Tamthilia ya Sudana. *Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili*, 5(2), 124-130.
- Waithiru, A. K., Onyango, J. O., & Nabea, W. (2020). Tathmini ya kipengele cha taashira za wahusika katika tamthilia ya Kimani Njogu: Mfano wa Zilizala. *Editon Consortium Journal of Kiswahili*, 2(1), 34-47.
- Wamitila, K. W. (2003). Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia. Nairobi.Focus Publications Ltd.
- Wamitila, K. W., & wa Fasihi, U. (2002). Misingi na Vipengele vyake. *Nairobi: Phoenix Publishers*.
- Zahra, S. O. U. D. (2016). *Fani Katika Maulidi Ya Nuni* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO A: KIBALI CHA UTAFITI



**KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL**

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke

Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 8710901 Ext. 57530

Our Ref: C50/CE/25426/2014

DATE: 27th August, 2024

Director General,
National Commission for Science, Technology
and Innovation
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI

Dear Sir/Madam,

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION FOR NYANCHAMA FILISTER EUNICE - REG.
NO. C50/CE/25426/2014**

I write to introduce Nyanchama Filister Eunice who is a Postgraduate Student of this University. The student is registered for M.A degree programme in the Department of Kiswahili & African Languages.

Nyanchama intends to conduct research for a M.A Project Proposal entitled, "Athari ya Tamthilia ya Mashetani (1971) juu ya Tamthilia ya Mashetani Wamerudi (2016)."

Any assistance given will be highly appreciated.

Yours faithfully,

**PROF. ELIUD NJAGI
EXECUTIVE DEAN, GRADUATE SCHOOL**

EM/mc

